# UHUSIKA KATIKA MASHAIRI YA KISWAHILI: *MALENGA WA VUMBA, KICHOMI* NA *UTENZI WA FUMO LIYONGO*

**NA**

**MAKUTSA R. SAMBA**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA MINAJILI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI**

**SHULE YA SANAA NA SAYANSI JAMII**

**CHUO KIKUU CHA MASENO**

**©2018**

# IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa katika chuo kikuu kingine chochote kile, kwa mahitaji ya kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili.

______________________________ ______________________

**Makutsa Raphael Samba** **Tarehe**
**PG/MA/000051/05**
**(Mtahiniwa)**

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Maseno.

______________________________ ______________________

**Profesa Wangari Mwai** **Tarehe**
**Idara ya Fasihi**
**Chuo Kikuu cha Kenyatta**

______________________________ ______________________

**Daktari Deborah Amukowa** **Tarehe**
**Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika**
**Chuo Kikuu cha Maseno**

## SHUKURANI

Kwanza kabisa natoa shukurani za moyoni kwa Maulana Muumba kwa kunijalia siha na amani ya moyoni kwa muda wote nimekuwa masomoni. Pili, shukrani za dhati ziwafikie wasimamizi wangu Dkt. Amukowa Deborah na Profesa Wangari Mwai. Kazi hii haingepiga hatua yoyote wala kukamilika bila ushauri wao. Walisoma kazi hii na kuikosoa bila kukawia na kuniongoza kikamilifu. Zaidi ya hayo, walianzisha midahalo ya kiakademia ambayo ilinitumbukiza katika bahari ya sijui na kuibuka katika fahari ya ninafahamu. Midahalo hii iwe katika maandishi au kupitia mazungumzo ya ana kwa ana ilinisaidia sana katika kuimarisha kiwango cha utafiti huu. Shukrani zisizo na kifani ziwafikie huku nikiwatakia baraka za Mwenyezi Mungu na fadhili zake siku zote za maisha yenu.

Nawashukuru wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Maseno ambao walinifunza au kunipa mawaidha ya kiusomi kwa kipindi nilichokuwa masomoni. Hawa ni Mwenyekiti wa Idara ya Kiswahili Prof. Indede Florence, Msimamizi wa Shule ya Sanaa na Sayansi Jamii, Dkt. Kioli, Mkurugenzi wa Shule ya Shahada za Juu (SGS) Prof. Agure na mtangulizi wake Prof. Okinda. Shukurani za dhati zimwendee Profesa Simala Inyani wa tume ya Kiswahili ya Afrika Mashariki. Sina budi kuwashukuru Luvaha Judith na Jagero Juliet tulioshirikiana nao katika masomo ya shahada ya umahiri. Shukrani za kipekee zikufikie wewe Lydiah Amara kwa maelekezo na midahalo tuliyokuwa nayo kipindi chote cha masomo haya. Mawaidha yako yalinifaa sana na uwe wa manufaa kwa wengine kama ulivyokuwa kwangu.

Natoa shukurani kwa tume ya kuajiri walimu T.S.C. pamoja na Mwalimu Mkuu wa Shule ya Upili ya Esalwa Bwana Wycliffe Obuhuma kwa kuidhinisha likizo yangu ya masomo na mawaidha uliyonipa hasa kunihimiza kuendelea na masomo hadi upeo huu. Nawashukuru wahazili Lucy Mudome na Millicent Abwao wa Shule ya Upili ya Wasichana ya Bunyore walionisaidia kupiga chapa kazi hii kwani haingekuwa kamilifu bila uchapishaji. Mwisho, natoa shukrani za dhati kwa nyote mliochangia kwa njia moja au nyingine kufanikisha tasnifu hii. Langu ni kuwahimiza muwe mwanga na kielelezo bora kwa wasomi wengine kama mimi.

## TABARUKU

Kazi hii naitabarukia wazazi wangu marehemu Justin Allan Samba na mamangu Bi. Doris Ombonya Samba.

# IKISIRI

Uhusika katika ushairi wa Kiswahili ni kipengele ambacho hakitiliwi maanani na wahakiki wengi wa mashairi. Uhusika huu haujitokezi wazi kama ilivyo katika tanzu zingine za fasihi. Aghalabu huwa si dhahiri, huonekana kuwa tata kutokana na umbo na muundo wa utanzu huu. Uhusika katika ushairi upo ila hubainika kupitia vipengele vingine. Suala kuu la utafiti wetu ni vipengele vinavyodhihirisha uwepo wa uhusika katika ushairi wa Kiswahili. Azma ilikuwa kutathmini uhusika na usawiri wa wahusika mbalimbali kama wanavyojitokeza katika mashairi ya Kiswahili. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa ni: Kutathmini jinsi uhusika unavyojitokeza katika ushairi wa Kiswahili, kubainisha aina za uhusika katika mashairi ya Kiswahili na kuchunguza usawiri wa wahusika katika ushairi wa Kiswahili. Upeo wa utafiti huu ni uhusika katika ushairi kwa kurejelea diwani mbili na utenzi mmoja. Hivyo basi upeo wa mada ni usawiri wa uhusika katika tanzu tofauti za mashairi. Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Usimulizi kwa mujibu wa Manfred (2005). Mihimili mikuu ya nadharia hii ni dhana ya uhusika na usimulizi. Kwa mujibu wa nadharia hii suala la kimsingi ni kutathmini ni nani mrejelewa, anachukuwa sehemu ya nani, akiwa kama nani. Utafiti ulichukua muundo wa kiuchanganuzi. Data iliyokusanywa ilitathminiwa kimaelezo. Mbinu za ukusanyaji data zilikuwa unukuzi na uchunzaji kupitia orodha ya uchunzaji. Sampuli dhamirifu ilitumika kuteua diwani ya *Malenga wa Vumba* (1981), diwani ya *Kichomi* (1974) na *Utenzi wa Fumo Liyongo* (1973) kutoka Afrika Mashariki. Usampulishaji huu ulitumika  kwa sababu ulilenga tungo mahsusi, hivyo basi ufafanuzi mwafaka kutolewa kuhusu uhusika. Data iliyokusanywa ilifafanuliwa kwa kina kwa kuegemea dhana ya uhusika. Matokeo ya uchunguzi yamedhihirisha kwamba uhusika katika ushairi upo kwa kuwa mashairi hutungwa kutokana na mazingira anamoishi mtunzi na siyo kutoka kwenye ombwe. Utafiti unatoa mchango kuhusu suala la uhusika katika ushairi na fasihi kwa jumla. Utafiti huu ni miongoni mwa tafiti chache ambazo zimefanywa kuhusu uhusika katika ushairi wa Kiswahili. Aidha utawafaidisha wasomi wengi wakiwemo wahadhiri, walimu na wanafunzi wanaotafuta uelewa wa ushairi wa Kiswahili. Utafiti huu utawafaa wahakiki wengi wa fasihi ya Kiswahili. Utafiti unapendekeza utafiti linganishi wa wahusika katika ushairi na tanzu zingine za fasihi ya Kiswahili.

## ABSTRACT

Characterization in Kiswahili poetry is an aspect that has been given little attention by literary analysts. Characterization in poetry does not manifest itself vividly as it does in other genres of literature. It looks complicated because of the form in which it appears. Characterization in Kiswahili poetry is not clear. It seems not to exist in poetry yet it can be realized through other aspects. The aim of this study was to analyze characterization and portrayal of characters in Kiswahili poetry. The main objectives were: to analyze how characterization manifests itself in Kiswahili poetry, to explain types of characters in Kiswahili poetry and to examine portrayal of characters in Kiswahili poetry. The scope of this study is characterization in poetry basing on three texts: two anthologies and one epic from East Africa. In summary the scope for the research topic is portrayal of characters in different types of Kiswahil poems. The study was based on the Theory of Naratology by Manfred (2005). This theory is based on characterization and naratology. It examines how personality traits of fictional characters are constructed. According to Manfred analysis can be done by questioning, who characterizes who and is characterized as what. The study employed analytical research design carried out in the library. The study used secondary data that dealt with poetry. The method used to record data was observation, recording and filtering. From these, purposive sampling technique was used to select three texts of poetry. These were two anthologies: *Malenga wa Vumba* (1981) and *Kichomi* (1974) and one epic *Utenzi wa Fumo Liyongo* (1973). Purposive sampling technique was used because only the relevant texts were selected. The data collected was analyzed using elaborate explanation based on the aspect of characterization. The major findings of the study prove that characterization in poetry exists because poets compose poems based on real life experiences and not from a vacuum. The study is significant in that it will be useful in guiding analysis of characters and characterization in poetry and other genres in literary studies. The study is among the few done on Kiswahili poetry. This study will be of great benefit to scholars lecturers, teachers and students seeking to understand Kiswahili Poetry. This research recommends comparative research of characters in Kiswahili poetry and other genres in literature.

YALIYOMO

Ikirari ... ii
Shukurani ... iii
Tabaruku ... iv
Ikisiri ... v
Abstract ... vi
Yaliyomo ... vii
Maelezo ya Istilahi ... x
Orodha ya Michoro ... xi
**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI** ... 1
1.1 Usuli wa Utafiti ... 2
1.2 Suala la Utafiti ... 5
1.3 Maswali ya Utafiti ... 5
1.4 Madhumuni ya Utafiti ... 6
1.6 Umuhimu wa Utafiti ... 6
1.7 Upeo wa Utafiti ... 10
1.8 Misingi Ya Kinadharia ... 11
1.9 Hitimisho ... 17
**SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDISHI** ... 18
2.1 Utangulizi ... 18
2.2 Dhana ya Uhusika Katika Fasihi ... 19
2.3 Dhana ya Uhusika Katika Ushairi wa Kiswahili ... 23
2.4 Namna Uhusika Unavyojitokeza Katika Ushairi ... 30
2.4.1 Dhana ya Uhusika Nafsi ... 30
2.4.1.1 Uhusika wa Nafsi - Pekee ... 30
2.4.1.2 Uhusika wa Nafsi – Uwili ... 30
2.4.1.3 Uhusika wa Nafsi - Wingi ... 31
2.4.1.4 Uhusika wa Nafsi - Umoja ... 31
2.4.1.5 Uhusika wa Nafsi - Kikundi ... 32
2.5 Aina Za Uhusika ... 32
2.5.1 Uhusika Umbo ... 32
2.5.2 Uhusika Dhahiri ... 33
2.5.3 Uhusika Usio Dhahiri ... 34
2.5.4 Uhusika –Altero au Uhusika Husishi ... 36
2.6 Uumbaji wa Wahusika Katika Fasihi ya Kiswahili ... 38

2.7 Taswira ya Wahusika Katika Ushairi ........................................................................ 45
2.8 Uhusika Simulizi ........................................................................................................ 47
2.9 Usimulizi wa Nafsi Unavyoibua Taswira ya Wahusika na Vihusika ................................ 48
2.10 Hitimisho .................................................................................................................. 51
**SURA YA TATU: NJIA NA MBINU ZA UTAFITI** ............................................................ 54
3.1 Utangulizi .................................................................................................................. 54
3.2 Muundo wa Utafiti ....................................................................................................... 54
3.3 Eneo la Utafiti ............................................................................................................. 55
3.4 Sampuli na Usampulishaji ........................................................................................... 55
3.5 Mbinu za Ukusanyaji Data ........................................................................................... 59
3.6 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data .......................................................................... 60
3.7 Suala la Maadili ........................................................................................................... 61
3.8 Hitimisho ..................................................................................................................... 61
**SURA YA NNE: UHUSIKA KATIKA TUNGO TEULE ZA USHAIRI WA KISWAHILI** 62
4.1 Utangulizi .................................................................................................................. 62
4.2 Usimulizi Unavyoibua Uhusika Katika Ushairi Teule wa Kiswahili ................................ 63
4.2.1 Usimulizi Unavyoibua Wahusika Katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* ............................ 65
4.2.1.1 Fumo Liyongo ........................................................................................................ 67
4.2.1.2 Sultani ................................................................................................................... 73
4.2.1.3 Mamake Liyongo ................................................................................................... 75
4.1.2.4 Mama Mkwe wa Liyongo ........................................................................................ 78
4.2.1.5 Mwanawe Liyongo ................................................................................................. 79
4.2.1.6 Wagalla, Wasanye na Wadahalo ........................................................................... 82
4.2.1.7 Kijakazi Saada ...................................................................................................... 83
4.2.1.8 Askari .................................................................................................................... 84
4.2.1.9 Usimulizi Unavyoibua Uhusika wa nafsi katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*………….85
4.2.10 Usimulizi Unavyoibua Vihusika Katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* ........................... 88
4.3 Tathmini yaUsimulizi Unavyoibua Uhusika Katika Diwani ya *Kichomi* ........................... 92
4.3.1 Wakoloni ................................................................................................................... 92
4.3.2 Bushiri, Mkwawa, Kinjeketile, Mirambo na Mbumi .................................................... 94
4.3.3 Nyerere ..................................................................................................................... 95
4.3.4 Wesema na Mumewe Kasinge ................................................................................... 97
4.3.5 Kanana ...................................................................................................................... 98
4.3.6 Katili ........................................................................................................................ 100
4.3.7 Jirani ........................................................................................................................ 100
4.3.8 Sauti ........................................................................................................................ 100
4.3.9 Wajukuu ................................................................................................................... 101
4.3.10 Usimulizi UnavyoibuaVihusika Katika Diwani ya *Kichomi* ....................................... 102

4.4 Usimulizi Unavyoibua Uhusika Katika Diwani ya *Malenga wa Vumba* .......................... 109
4.5 Hitimisho ..................................................................................................... 111
**SURA YA TANO: AINA ZA UHUSIKA NA TASWIRA INAVYOIBUA UHUSIKA NAFSI**………………………………………………………………………...……112
5.1 Uhusika Nafsi Unavyoibua Uhusika Katika Ushairi ........................................................ 112
5.1.1 Uhusika wa Nafsi Unavyoibua Uhusika Katika *Malenga wa Vumba* ........................ 112
5.1.2 Uhusika wa Nafsi Unavyoibua Uhusika Katika Diwani ya *Kichomi* ........................ 118
5.2 Ujenzi wa UhusikaKupitiaTaswira Katika Ushairi wa Kiswahili .................................. 127
5.2.1 Taswira ya usikivu ..................................................................................... 129
5.2.2 Taswira ya Mguso ..................................................................................... 132
5.2.3 Taswira ya Mwonjo ..................................................................................... 134
5.3.4 Taswira ya Uoni ..................................................................................... 135
5.3 Lugha Inavyoibua Taswira ya Wahusika Katika Ushairi wa Kiswahili ........................... 140
5.3.1 Utumizi wa Misemo na Nahau Kuibua Wahusika Katika Ushairi ............................. 142
5.3.2 Utumizi wa Takriri Kuibua Wahusika Katika Ushairi .............................................. 144
5.3.3 Utumizi wa Sitiari Kuibua Wahusika Katika Ushairi ............................................... 145
5.3.4 Mishororo na Mishata Inavyoibua Uhusika Katika Ushairi ...................................... 146
5.4 Hitimisho ..................................................................................................... 148
**SURA YA SITA: MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO ...................... 150**
6.1 Utangulizi ..................................................................................................... 150
6.2 Muhtasari wa Tasnifu………………………………………………………………150
6.3 Matokeo ya Utafiti ..................................................................................................... 151
6.4 Mahitimisho ..................................................................................................... 154
6.5 Mapendekezo ..................................................................................................... 156
**MAREJEO** ..................................................................................................... 158
**KIAMBATISHO** ..................................................................................................... 164

## MAELEZO YA ISTILAHI

**Mashairi huru**-Mashairi ambayo hayana ulazima wa kufuata kanuni za kiarudhi.

**Mashairi jadi**-Mashairi yanayozingatia kanuni za utunzi za kimapokeo.

**Mhusika**-Binadamu yeyote, mnyama, ama umbo lililowakilishwa katika kazi ya sanaa.

**Mishororo**-Mistari katika ubeti wa shairi.

**Taswira**-Maneno yanayotoa picha ya kitu, hali, wazo au dhana juu ya jambo fulani. Kwa maneno mengine ni lugha ya picha.

**Uhusika**-Kumjenga mhusika kwa kumpa umbo, wasifu, tabia na kueleza matendo yake

**Uhusika dhahiri**-Mambo yanayotambulisha nafsi ya mtu au kitu ambacho ni kihusika

**Uhusika husishi**-Maelezo ya jinsi wahusika wanavyofikiria kuwahusu wahusika wengine katika matini.

**Uhusika-nafsi**– Nafsi ya kiumbe inayobainika kama mhusika ama kihusika katika masimulizi

**Uhusika-umbo**-Utambulisho wa mhusika ama kihusika kinachorejelewa

**Uhusika usio dhahiri** - Taarifa ambayo inalenga sifa au tabia bainishi za kiutu

**Umbo dhahiri**- Nafsi inayodhihirika kutokana na jinsi inavyoonekana

**Umbo dokezi** – Nafsi inayobainika kutokana na masimulizi yasiyokuwa ya moja kwa moja.

**Tenzi**-Utungo mrefu wa kishairi unaosimulia tukio fulani kwa matendo.

**Usawiri** – Picha zinazotokana na maelezo kuhusu umbo dhana au hali.

**Usimulizi**-Namna hadithi inavyowasilishwa kwa hadhira na msanii

**Wahusika**-Viumbe wa kifasihi wanaoumbwa na mwandishi ili wawe sauti yake katika kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira.

**ORODHA YA MICHORO**

Mchoro A: Usimulizi wa upeo wa kwanza A unajumuisha hadithi ya upeo wapili B….….Uk 11

Mchoro B: Maelezo ya mwandishi na ya wahusika, mazungumzo na matendo yaletayo msukumo wa kuelewa matendo ya mhusika yanayoibua uhusika………………………......................Uk29

# SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

Utafiti huu unahusu uhusika katika ushairi wa Kiswahili kwa kurejelea *Utenzi wa FumoLiyongo*, diwani ya *Malenga wa Vumba* na diwani ya *Kichomi.* Ushairi ni sanaa inayosawiri hali halisi ya maisha hivyo basi uhusika kupitia utunzi unapaswa kuwa kielelezo cha watu na vitu katika mazingira halisi.

Mlacha (2003), anaeleza uhusika kuwa ni uwezo wa msanii kuwahusisha watu vizuri kulingana na mawazo yake. Si lazima msanii atumie watu, anaweza kuhusisha vitu, wanyama na vitu visivyokuwa na uhai. Uhusiano huu unafanikiwa zaidi iwapo uumbaji wa mhusika utalingana na maisha halisi. Aidha anaeleza kuwa utungaji wa picha ya mawazo ya watu waliobuniwa kwenye hadithi, kiasi ambacho kwa msomaji wanaelekea kuwa hai ndio uumbaji wa wahusika.

Wamitila (2003), ameeleza dhana uhusika kuwa hali ya kumjenga mhusika kwa kumpa umbo, wasifu, tabia na kueleza matendo yake. Mhusika huyu anaumbwa ili kuwakilisha tathmini maalum ya watu au matendo ya mtu. Na mtu huyo anayezungumziwa sio kama mtu binafsi, bali mfano wa watu wa aina yake. Anasemauhusika ni mbinu na mikakati inayotumiwa na mtunzi kuwasawiri wahusika katika kazi yake. Mhusika ni kiumbe anayepatikana katika kazi ya fasihi na ambaye anafanana na binadamu wa kawaida kwa kiasi fulani na huumbwa na msanii. Ingawa wahusika wengi ni wanadamu, si lazima wote wawe watu, kuna wanyama na vitu visivyokuwa na uhai. Vitu visivyo na uhai ilmuradi hupewa sifa za kibinadamu mfano jiwe au ndege kupewa sifa ya kuongea. Katika kuwateua na kuwaumba wahusika watunzi huwapa sifa mbalimbali. Wahusika wanaweza kuchorwa kwa ukamilifu au wakadokezwa tu. Watunzi lazima

wawahusishe wahusika wao kupitia maelezo ya maumbile, vitendo, mazungumzo pamoja na athari ya hali hizi zote kwa fikra na hisia zao.

Katika ushairi haiwi rahisi kuchora wahusika kwa undani. Mashairi hutungwa kwa kutumia lugha ya mkato na hivyo haiwezekani kutoa maelezo mengi kuhusu mhusika kufikia kiwango cha kutambua undani wa mhusika ila kukisia tu kutokana na maelezo ya mtunzi. Katika mashairi mengi, wahusika hudokezwa tu. Kumjenga mhusika ni mojawapo ya majukumu muhimu ya mtunzi. Mtunzi huchukua jukumu la Uungu kwa sababu yeye huwa anaumba binadamu na vitu na kuweka katika ulimwengu walioandaliwa katika kazi ya fasihi. Mwanzoni mwandishi huweza kubuni mhusika kwa kuzingatia wajihi, rangi ya ngozi, mavazi au mtindo wa nguo na sauti. Mtunzi basi huweza kubuni nafsi ya mhusika na kihusika. Mtunzi hana budi kuchagua kati ya mambo kadhaa ili kuweka kihusika ama mhusika anayebuniwa katika hali ya kuaminika. Mtunzi anapomwelewa mhusika ama kihusika lazima pia aweze kumfanya msomaji amwelewe mhusika huyo ama kihusika hicho.

## 1.1 Usuli wa Utafiti

Ushairi ni fani maalum ya uwasilishaji maisha kisanaa kama vile mahusiano ya kijamii, imani, fikra, na hisia za jamii. Utafiti kwenye fasihi na sanaa jadi huzingatia fasihi simulizi na fasihi andishi. Tanzu za fasihi simulizi ambazo hufanyiwa utafiti ni nyimbo, hadithi, misemo, ushairi na sanaa ya maonyesho.  Utafiti katika fasihi andishi hulenga riwaya, tamthilia, ushairi na hadithi fupi. Ushairi wa Kiswahili una historia ndefu sana zaidi ya tanzu zingine kama vile riwaya, tamthilia na hadithi fupi. Ushairi unatofautiana sana na riwaya, tamthilia na hadithi fupi kiumbo na hata kifani. Asili ya ushairi ni nyimbo. Wimbo husisitiza hisia za aina moja ambazo hujengwa

kwa msaada wa mpangilio wa maneno na hata kuleta mahadhi, mizani na sifa zingine ambazo ni za kipekee kwa ushairi. Nyimbo ni maneno yanayotamkwa kwa sauti iliyo na mpangilio wa muziki. Uimbaji wa nyimbo unaweza kuambatanishwa na vyombo vya muziki ama usihusishwe.

Uhusika ni mbinu muhimu sana inayotumiwa na wasanii katika fasihi tangu kuchapishwa kwa utenzi uitwao *Odyssey*. Wasomi wanaamini ulitungwa na Homer (800 KK). Utenzi huu unaaminika kuwa kazi ya pili baaada ya *Illiad* iliyokuwa ya mwanzo kabisa ya kifasihi katika historia na maendeleo ya fasihi ulimwenguni. Butler (1969), katika tafsiri ya *Odyssey* anaeleza katika utangulizi kuwa *Utenzi wa Odyssey* uliweka msingi wa maandishi ya kinathari ya Kigiriki na Kizungu, na misingi ya usimulizi wa hadithi na uhusika.

Kutokana na maelezo haya utafiti unabainisha kuwa uhusika unapaswa kushughulikiwa katika ushairi kama ilivyo katika tanzu zingine za fasihi. Haipasi kudhani kuwa uhusika haupo. Wahakiki na wachambuzi wa mashairi wanapaswa kutilia maanani kipengele hiki.

Utafiti huu unafafanua uhusika kama utaratibu unaotumiwa na mtunzi kutambua tabia ya mtu kwa kumpa sifa mbalimbali, kuvipa vitu visivyo na uhai sifa za kibinadamu. Si lazima wahusika wawe watu panaweza kuwa na wanyama, wadudu na vitu. Wahusika wakielezwa vizuri hutambuliwa kwa urahisi na wasomaji. Wahusika hujitokeza kuwa wenye uhai, huonekana kuwa huru na wanajisimamia katika vitendo vyao. Wao huwa si vikaragosi, aghalabu wahusika hao huwa na maisha kamili, hukua, hubadilika na huweza kufuatiliwa kupitia tajiriba mbalimbali. Wahusika waliochorwa kikamilifu hueleweka kwa ndani na nje. Msomaji huweza kutambua mawazo na falsafa yake. Mwenendo wake huweza kubainika kutokana na mtagusano wake na

wahusika wengine. Wahusika hao humshangaza, humfurahisha na huzinata fikra au hisia za msomaji. Kwa upande mwingine wahusika wasiochorwa kwa undani huwa na sifa moja tu. Wahusika wa aina hii husaidia kukuza wahusika wengine. Aghalabu wahusika hawa hawakui, hawana maisha ya ndani na hivyo hawamshangazi msomaji. Wahusika waliochorwa kwa undani mara nyingi huonekana kuwa ajabu, hushangaza na hukumbukwa.

Utafiti huu uliangazia aina za uhusika katika mashairi, majukumu na dhima wanazopewa wahusika katikaushairi. Mtafiti kwa kutumia mawazo ya wahakiki na wachambuzi mbalimabali ameibua vipengele vinavyotumiwa katika kuchambua mashairi ili kufumbua swala la uhusika. Ili kujibu maswali makuu yaliyotaka kujua vipi uhusika unavyojitokeza katika ushairi, namna uhusika unavyoainishwa katika ushairi na jinsi watunzi wanavyowasawiri wahusika katika ushairi wa Kiswahili, utafiti huu ulifafanua namna ambavyo uchambuzi unawabainisha wahusika katika mashairi na tenzi.

Mashairi mengi husheheni masimulizi ya mtunzi kama ilivyo katika riwaya na tamthilia. Wahakiki na wachambuzi huchukulia kwamba kwa kuwa ni masimulizi na wahusika hawajitokezi moja kwa moja hapana haja ya kushughulikia uhusika. Suala kuu hapa ni kwanza masimulizi haya yanahusu watu au vitu alivyoviumba mtunzi. Pili yanasimuliwa na watu au viumbe ambavyo ameviumba mtunzi. Si lazima pawepo na watu halisi walioumbwa na kujitokeza bayana kama inavyodhihirika katika riwaya na tamthilia.

Utafiti huu umechunguza jinsi washairi huwaumba wahusika katika mashairi yao. Watunzi hutoa mifano ya watu wazuri na wabaya kwa kutumia wahusika wakiwa katika shughuli zao. Katika

ushairi mtunzi hutumia lugha ya mkato ilhali katika riwaya, tamthilia na hadihi fupi mtunzi hutumia lugha ya mjazo. Anapofanya hivi huweza kuingia kwenye nyoyo na akili ya hadhira yake. Wahusika hubuniwa kutokana na kile anachotaka kukifafanua msanii. Uteuzi na usukaji wa wahusika wake ndio unaomwezesha kupitisha ujumbe wake. Kama ilivyo kawaida ya wasanii, tungo zao hutokana na mwamko wa tukio, kisa ama hisia fulani. Mshairi huweza kujitia ndani ya joho akawa kuhani, ama kujipoteza ndani ya buibui na kuwa msemaji wa wanawake. Katika kufanya hivyo, mtunzi hutumia wahusika kubainisha fikra zake. Utafiti huu umechunguza utokeaji wa uhusika katika ushairi wa Kiswahili kwa kurejelea diwani mbili ambazo ni *Kichomi* na *Malenga wa Vumba* na *Utenzi wa Fumo Liyongo*.

## 1.2 Suala la Utafiti.

Uhusika ni kipengele cha fani lakini hakijitokezi waziwazi katika ushairi wa Kiswahili kama ilivyo katika tanzu zingine za fasihi. Uhusika katika ushairi huwa si dhahiri, huonekana kuwa tata kutokana na umbo na muundo wa shairi. Vipengele vingine hutiliwa maanani na wachunguzi kwa kufikiria kwamba hiki cha uhusika hakina uzito. Kuumba au kuwachora viumbe katika ushairi huwa katika fikra na mawazo ya mtunzi. Ni kupitia vipengele vingine uhusika katika ushairi unaweza kudhihirika. Utafiti huu ulitathmini uwepo wa wahusika kupitia vipengele vingine na namna wanavyojitokeza katika ushairi wa Kiswahili na hivyo kuondoa dhana kwamba uhusika katika ushairi si suala la kutilia maanani. Aidha kwa kupitia vipengele hivyo utafiti ulibainisha taswira ya wahusika katika ushairi wa Kiswahili na namna ambavyo uhusika hupambanuliwa. Hilo ndilo pengo ambalo utafiti huu ulinuia kuchangia kuziba.

## 1.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu umeongozwa na maswali yafuatayo:

1. Uhusika hujitokeza vipi katika ushairi wa Kiswahili?
2. Uhusika katika ushairi wa Kiswahili ni wa aina gani?
3. Wahusika  huumbwaje kupitia taswira katika ushairi wa Kiswahili?

## 1.4 Madhumuni ya Utafiti

Kwa jumla utafiti huu ulinuia kuzingatia kipengele cha uhusika katika ushairi wa Kiswahili kwa misingi ya uhalisi wake na utokeaji wake kama kipengele muhimu katika ushairi wa Kiswahili. Ili kufikia lengo hili utafiti umejikita katika madhumuni mahsusi yafuatayo:

1. Kutathmini namna uhusika unavyojitokeza katika ushairiwa Kiswahili.
2. Kupambanua aina za uhusika katika ushairi teule wa Kiswahili.
3. Kuchunguza namna taswira huumba wahusika katika ushairi wa Kiswahili.

## 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu umefanywa kwa misingi kuwa, kuna utata katika kueleweka kwa uhusika katika ushairi wa Kiswahili.Wahakiki hupuuza uhusika katika ushairi kutokana na muundo wa shairi. Wahusika katika ushairi hawatokei moja kwa moja. Ni jukumu la msomaji kumtambua mhusika na kutoa maelezo kumhusu kutokana na vile shairi linavyotiririka kutoka ubeti wa kwanza hadi wa mwisho. Katika ushairi wahusika hudhihirika kupitia uhusika wa moja kwa moja na ule usio wa moja kwa moja. Mwandishi anaweza kutoa maelezo ya moja kwa moja kuhusu mhusika au akamweleza mhusika kupitia vitendo vyake, maneno yake, fikra, hisia, marafiki, nguo zake na hata jina. Mada ya uhusika japo imefanyiwa utafiti katika fasihi uhusika ulioshughulikiwa ni ule wa tanzu nyingine za Fasihi kwa Kiswahili. Hivyo basi kwa muhtasari utafiti huu ulifanywa kwa sababu tafiti ambazo zimefanywa zilirejelea vipengele vingine vya ushairi wa Kiswahili.

Utafiti uligundua kuwa uhusika haushughulikiwi wakati wa kuchambua na kuhakiki mashairi. Watafiti wengi waliochanganua tanzu tofauti za fasihi wameshughulikia maudhui, muundo, dhamira, ujumbe, wahusika wanawake katika tanzu nyingine za Fasihi ya Kiswahili na vipengele vingine huku uchunguzi mchache ukifanywa kuhusu uhusika katika ushairi. Utafiti huu ulishughulikia uhusika katika ushairi na kudhihirisha kuwa upo na ni suala linalohitaji kupewa kipaumbele kama ilivyo katika tanzu nyingine za fasihi. Hivyo basi kupitia utafiti huu wanafasihi wataweza kuelewa udhahiri wa uhusika katika ushairi na kutilia mkazo katika uhakiki.

Dhana ya uhusika ni muhimu sana kwani hueleza misingi ya uumbaji wa wahusika na sababu za matendo yao mbalimbali katika kazi yoyote ya fasihi ushairi ukiwemo. Aidha uhusika katika ushairi hujitokeza kama dhana dhahania. Mashairi mengi huhusu vituko, matukio na masimulizi yanayohusu wanajamii. Kupitia vitushi, matukio na masimulizi hayo utafiti ulizindua wahusika na vihusika katika ushairi. Vituko, matukio na masimulizi hutendwa na watu na viumbe haiau hutokana na uhusiano wa watu na vitu katika mazingira kwa kuhusisha viumbe wenye uhai na vitu visivyo na uhai. Aidha uhusika hujitokeza kwa namna mbalimbali kama vile watu wanyama vitu au hali. Watunzi wa mashairi huwasawiri wahusika kwa njia tofauti kama vile wanawake wenye hekima, watu wakatili, au hata wanyama na vitu kama vile misitu na mapango.

Lugano (1989), Muindi (1990), Momanyi (1991), Muleka (2000) na Mlacha (2003) wamefanya utafiti kuhusu wahusika katika tanzu nyingine za fasihi. Hawakushughulika na utanzu wa ushairi. Lengo la utafiti huu lilikuwa kuchunguza na kupambanua uwepo wa uhusika katika ushairi wa Kiswahili mintaarafu njia za usimulizi na mbinu za uumbaji katika mashairi mbalimbali. Utafiti

huu umenuia kuonyesha na kutambulisha aina mbalimbali za uhusika zinazojitokeza katika mashairi ya Kiswahili. Hivyo basi kuwezesha utafiti zaidi kuhusu masuala mbalimbali ya uhusika katika fasihi ya Kiswahili.

Ni masuala mengine ya kifani yaliyotiliwa mkazo katika mashairi ya Kiswahili. Suala la uhusika limeangaziwa kwa uchache sana katika baadhi ya tasnifu za watafiti mbalimbali. Chacha (1977), Alichunguza maudhui mbalimbali yanayojitokeza katika mashairi ya Abdalla (1973). Hakukugusia suala la uhusika katika uchunguzi wake.Ili utanzu wowote wa fasihi uweze kukamilika uhusika ni kipengele ambacho hakina budi kushughulikiwa. Utafiti huu umeonyesha mapengo ambayo yamesababishwa na kutotilia mkazo suala la uhusika katika ushairi. Kutokana na hoja zilizojadiliwa, utafiti huu umedhihirisha aina za uhusika kwa kurejelea mashairi katika nyakati mbalimbali za historia. Yote haya yamewezekana kupitia dhana ya uhusika na usimulizi. Uwepo wa uhusika katika ushairi unadhihirisha kuwa kuna haja ya wahakiki na wachambuzi kuzingatia kipengele hiki cha fani wanapohakiki mashairi. Utafiti huu umedhihirisha maana ya uhusika kwa kuzingatia maoni ya wahakiki wa kazi za sanaa hususan fasihi na kubainisha uwepo wa uhusika katika ushairi wa Kiswahili.

Msanii huchagua umbo ambalo litawasilisha maelezo yake vizuri zaidi. Kila umbo lina sheria zake, lazima pawepo na wahusika katika riwaya ndipo hadithi iweze kueleweka. Katika tamthilia wahusika huwasilishwa kama waigizaji. Kutokana na jinsi wanavyohusiana na jinsi walivyoumbwa msomaji anaweza kueleza mhusika mkuu na wahusika wasaidizi na mahusiano baina yao. Uhusika unaojitokeza katika ushairi una upekee wa aina yake. Upekee huu ni ule wa

uhusika nafsi ambao uko katika matapo matano. Hivyo basi dhana ya wahusika wakuu na wasaidizi ni nadra katika ushairi.

Madhumuni ya kutunga mashairi ni kuwasilisha ujumbe kupitia wahusika na vihusika lakini kuna yale yasiyotegemea wahusika ili kuwasilisha ujumbe. Hata hivyo yapo mashairi ya masimulizi kama tendi ambayo hutumia wahusika kujenga maudhui yake. Uchambuzi wa mashairi ya aina hiyo lazima uzingatie pia dhima na taswira ya wahusika hao katika ujenzi wa matukio na maudhui ya utendi huo. Hali kama hizi zimewezesha utafiti huu kutoa mapendekezo kuhusu uhakiki wa mashairi kwa kuzingatia kipengele cha uhusika. Aina zote za ushairi zina uhusika lakini uhusika wenyewe sio bayana ama hautokei waziwazi katika mashairi yote ila katika utenzi na ngonjera.

Utafiti huu utawawezesha wahakiki kugundua upeo mpya wa uhakiki kwa sababu utawasaidia kuonyesha awamu mbalimbali katika utunzi kuhusu swala la uhusika katika ushairi. Hivyo basi pana haja ya watunzi kuwasawiri wahusika wao kulingana na mazingira. Aidha utafiti huu utachangia katika ukuaji wa fasihi ya Kiswahili na hivyo ni changamoto kwa utafiti mpana zaidi kuhusu swala la uhusika katika ushairi. Matokeo yanayotarajiwa ni kuibua mawazo mapya kuhusu kipaumbele katika maendeleo ambayo hutambua uhusika katika ushairi. Aidha matokeo hayo yataweza kuhamasisha wahakiki kuzingatia uhusika watakapokuwa wakihakiki mashairi. Aidha matokeo yataweza kubainisha ushairi kama utanzu wa fasihi andishi ulio na vipengele vyote vinavyozingatiwa katika uchambuzi wa kazi za fasihi.

Uumbaji huu wa wahusika umeshughulikiwa na kuelekezwa na dhana ya uhusika kama ilivyofafanuliwa katika Nadharia ya Usimulizi kwa mujibu wa Manfred (2005). Utafiti huu umejaribu kuziba baadhi ya mapengo yalioachwa na watafiti wa awali, hivyo basi kutilia maanani mwelekeo mpana kuhusu suala zima la uhusika katika utanzu wa ushairi wa Kiswahili.

## 1.6 Upeo wa Utafiti

Utafiti huu umechunguza uhusika katika ushairi kwa kurejelea diwani mbili na utenzi mmoja. Hivi ni kusema kwamba upeo wa mada ni usawiri wa uhusika katika tanzu tofauti za mashairi. Diwani hizi zimeteuliwa kimakusudi kwa kusheheni aina tofauti za mashairi na kwa kuzingatia kipindi cha utungaji. Uchunguzi ulishughulikia aina zote za mashairi. Kwa kuwa mashairi yapo ya aina nyingi ilibidi kuteua mashairi kutokavitengo viwili vikuu ambavyo ni mashairi-huru na mashairi ya arudhi. Diwani ziliteuliwa kwa kuzingatia aina za utunzi huku uteuzi wa mashairi ukizingatia baadhi ya mashairi kwenye diwani hizo. Diwani zilizoshughulikiwa ni *Malenga wa Vumba* (1981) na *Kichomi* (1974) na *Utenzi wa Fumo Liyongo* (1973). Mashairi yote yaliyochunguzwa ni kutoka Afrika Mashariki. Uteuzi huu ulisaidia kudhihirisha uwepo wa uhusika na kubainisha aina za uhusika katika ushairi.

Uhusika katika vipindi tofauti hutofautiana kutegemea mazingira ya wakati wa kuandika ama kutunga mashairi hayo. Masuala yaliyohusiana na mada pekee ndiyo yaliyorejelewa kubainisha aina za uhusika katika ushairi. Utafiti umechunguza uwasilishaji, usawiri na uumbaji wa wahusika katika ushairi ili kudhihirisha uwepo wa kipengele hiki cha fani katika ushairi. Utafiti huu umebainisha uhusika kama uwasilishaji wa wahusika watu, wanyama na vitu katika kazi ya fasihi. Uwasilishaji huu wa uhusika ni ule ambao hufasiriwa kwa msomaji kuwa wenye maadili,

hisia na sifa bainifu zinazojitokeza kutokana na yale wanayosema na kutenda kama atendavyo binadamu katika maisha halisi. Utafiti huu umefanywa maktabani na kwa kusakura mtandao kwa minajili ya kubainisha njia mbalimbali zilizotumiwa na watunzi tofauti kuumba wahusika katika tungo zao.

## 1.7 Misingi Ya Kinadharia

Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Usimulizikwa mujibu wa Manfred (2005) mihimili mikuu iliyozingatiwa nidhana ya uhusika na usimulizi. Manfred aliendeleza maoni ya Pfister (1977) kuhusu mbinu za uhusika. Mbinu hizi  zimechangia kufaulisha utafiti huu. Kwa mujibu wa Nadharia ya Usimulizi uelezaji wa hadithi katika utanzu wowote ule iwe ni katika matini, picha au maonyesho ya kisanaa ama jumla ya haya yote ni usimulizi. Hivyo basi tamthilia, sinema, futuhi ni usimulizi.

Manfred (2005),anaeleza kuwa matukio katika hadithi huhusu wahusika. Anafafanua kwa kusema matukio hujumuisha mambo asilia yanayotendeka na yale yasiyo asilia kama vile mafuriko na ajali. Pili, anasema, wahusika ndio vyombo vinavyosababisha matukio. Kisha, anamaliza kwa kusema wahusika huhusishwa wanapoathirika. Wanaweza kuathirika wanapokuwa wagonjwa au kunufaika kutokana na athari ya tukio. Dhana ya uhusika na usimulizi imetumika kutokana na uhusiano wake na mada ya utafiti huu. Lengo la kutumia mihimili hii lilitokana na maswali yafuatayo: Je, uhusika katika ushairi hujitokeza vipi? Je, uhusika katika ushairi huainishwa vipi? Je, watunzi huwasawiri vipi wahusika katika ushairi wa Kiswahili?

Vipengele vya usimulizi vimetumiwa na utafiti huu kubainisha, kuchunguza na kueleza uhusika unavyojitokeza katika ushairi. Utoaji maoni ya kibinafsi ni ule ambao mhusika mmoja husimulia wazi jinsi anavyojiona mwenyewe ilhali utoaji maoni kwa kando ni ule ambao mhusika mmoja huwasilishwa na mhusika mwingine kama mhusika dhahiri. Uwasilishaji wa ujumbe tofauti unaohusu mhusika fulani unaowasilishwa kwa hadhira na mhusika mwenyewe ama mhusika mwingine haustahili kuwa sawa. Aghalabu huwa si sawia na iwapo utakuwa hivyo basi, ni sehemu yake tu kwa kuwa huwa umefungamanishwa na hali za mhusika fulani.


Pfister (1977), amefafanua mbinu za uhusika kwa kusema kuwa zinaweza kutokana na mkusanyiko wa kanuni za maonyesho au tamthilia. Kwamba kigezo cha uainishaji kinatokana na swali iwapo ujumbe unaotumika kusawiri mhusika huwasilishwa na mmoja wa viumbe au unashirikishwa na nafsi ya mwandishi aliyedokezwa kama mhusika moja kwa moja. Amebainisha makundi manne yafuatayo: kwanza, ufanyizaji umbo dhahiri, pili, umbo dokezi, tatu, utunzi ulio dhahiri na nne, utunzi dokezi. Mbinu zote za uhusika wa umbo-dhahiri huwa za mazungumzo. Maumbo hayo yanaweza kuwekwa kwenye kategoria mbili. Kwanza ni utoaji maoni ya nafsi ambapo mhusika huweza kwa wakati mmoja kutumika kama mrejelewa na wakati uohuo akawa chombo cha kuwasilisha ujumbe. Pili ni utoaji maoni wa nje ambapo mrejelewa wa ujumbe unaowasilishwa si sawa na chombo cha uwasilishaji wa ujumbe. Utafiti huu umebainisha mashairi ambayo maoni ya nafsi yanamrejelea mhusika ambaye ni chombo kinachowasilisha ujumbe. Aidha utafiti umedhihirisha utoaji maoni wa nje kupitia mashairi ambayo mtunzi ametumia wahusika ama mhusika kama chombo cha kuwasilisha ujumbe wake kuhusu yanayojiri katika mazingira anamoishi.

Anasema usimuliaji wa hadithi unaweza kujitokeza katika viwango tofauti. Kwanza ni usimulizi wa upeo wa kwanza ambao ni usimulizi usiojumuishwa ndani ya usimulizi mwingine wowote. Pili ni usimulizi wa upeo wa pili ambao hujumuishwa ndani ya usimulizi wa upeo wa kwanza. Tatu ni usimulizi wa upeo wa tatu ambapo hapa usimulizi unajumuishwa ndani ya usimulizi wa upeo wa pili. Msimulizi wa upeo wa kwanza kianalojia ni msimulizi wa masimulizi ya upeo wa kwanza ilhali msimulizi wa upeo wa pili ni msimulizi wa masimulizi ya upeo wa pili.

Kutokana na maelezo haya ni dhahiri kwamba Pfister(1977) hakujihusisha na namna uhusika unavyojitokeza, aina ya wahusika au taswira ya wahusika ila amejikita katika mbinu za uhusika.Kuna mashairi ambayo yanasimulia matukio pasipo kujumuishwa ndani ya masimulizi mengine. Utafiti umebaini usimulizi ambao umejumuishwa ndani ya usimulizi mwingine ambao ni wa kwanza. Mwisho utafiti umedhihirisha usimulizi ambao umejumuishwa ndani ya usimulizi wa pili. Utafiti huu umebainisha kuibuliwa kwa uhusika kupitia usimulizi hivyo basi uwepo wa uhusika katika ushairi.

Kimsingi, Genette (1988), ameeleza muundo wa usimulizi jumuishi kwa kutumia mchoro wa vijiti kuwakilisha viumbe wakisimulia. Aidha ametumia usimulizi wa usemi kiputo. Puto ni mchoro unaofanana na mpira uliopulizwa na maelezo kutiwa ndani. Katika kielelezo cha 1 usimulizi wa upeo wa kwanza **A** unajumuisha hadithi ya upeo wa pili **B.**

**Mchoro A: Usimulizi wa upeo wa kwanza A unajumuisha hadithi ya upeo wa pili B.**




Usimulizi wa hadithi unaweza kufanyika kwa viwango vingi tofauti. Barth (1984, 1981) anaeleza kuwa kuna hadithi ndani ya hadithi ndani ya hadithi. Mchoro huu unatoa mpangilio wa kijumla anaoweza kutumika kuelezea hali nyingi changamano. Mojawapo wa hali kama hizi unaweza kutokea wakati mhusika katika hadithi anaanza kusimulia hadithi inayomhusu yeye mwenyewe hivyo basi kuibua usimulizi ndani ya usimulizi au hadithi ndani ya hadithi. Usimulizi asilia huwa sasa usimulizi wa nje na hadithi inayosimuliwa na mhusika simulizi huwa usimulizi wa ndani (Barth, 1981a, uk. 43)

Utafiti huu umeweza kuibua usimulizi uliofafanuliwa katika mchoro huu. Mtunzi wa shairi husimulia hadithi ambayo kwenye hadithi iyo hiyo kuna wahusika wengine. Wakati mhusika anasimulia matukio kwenye hadithi inakuwa hadithi ndani ya hadithi hivyo basi viwango tofauti vya usimulizi kuibuka kwenye hadithi moja. Hii inatokea tu kutokana na wahusika waliomo kwenye hadithi na kwa kufanya hivyo kuibua uhusika katika shairi.

Kulingana na Manfred (2005), tathmini ya uhusika huchunguza njia na mbinu za kuumba tabia za kibinadamu za wahusika dhahania. Anafafanua kwa kueleza kuwa swala la kimsingi ni kutathmini ni nani mrejelewa, na anachukuwa sehemu ya nani, akiwa kama nani. Utafiti huu

umedhihirisha kwa kutathmini wahusika ama vihusika virejelewa katika mashairi kwa kueleza tabia zao. Kuna wahusika walio na tabia za kikatili, kuna wale ambao ni wapole na wacha Mungu. Aidha utafiti umefafanua sehemu inayochukuliwa na wahusika ama vihusika hivi. Kuna sehemu mbalimbali zinazochukuliwa na wahusika na vihusika kama vile mwanamke, mtoto, maskini, tajiri, au hewa, msitu, maji na hali zingine zinazopatikana katika mazingira tunamoishi. Utafiti huu umefafanua sehemu zinazochukuliwa na wahusika na vihusika katika mashairi na kudhihirisha uhusika kama nani au nini.

Kuna njia kadha ambamo tathmini ya uhusika inaweza kushughulikiwa. Njia mojawapo ni kwa kuchunguza maelezo, mazungumzo na matendo. Mbinu mbili kuu za uhusika ni maelezo ya mwandishi kuhusu maumbile, sababu ya fikra na tabia za mhusika au kihusika chenyewe. Berger (1997), anadokeza kwamba, kupitia matendo ya mhusika, msomaji huweza kupata fahiwa, ni wa aina gani kwa kutafsiri hayo matendo kutegemea kanuni za kimaadili na thamani ya msomaji. Uhusika unaweza kutokana na namna wahusika wanavyojieleza kuwahusu wao wenyewe na hivyo kutumiwa kuelewa msukumo unaopelekea matendo ya mhusika. Kwa kufanya hivi tabia ya mhusika imefungamana na utu wake na hivyo kufanya matendo yake kukubalika.

Tathmini ya uhusika huzingatia maswala matatu ya kimsingi. Kwanza hutathmini uhusika wa usimulizi dhidi ya uhusika wa kinachohusishwa. Hapa hutambulisha msimulizi mrejelewa au mhusika mwenyewe. Pili hutathmini uhusika ulio dhahiri na uhusika usio dhahiri. Hapa hutathmini iwapo tabia za kibinadamu zinadhihirika kupitia maneno au zinaonekana kutokana na tabia za mtu. Tatu, ni uhusika wa nafsi (nafsi-peke, nafsi-uwili, nafsi-umoja, nafsi-wingi, nafsi-

kikundi) na uhusika rejelezi. Hapa hutathmini iwapo uhusika rejelezi unahusu msimulizi mwenyewe au unamrejelea mhusika mwingine.

Kutokana na ufafanuzi huu ni bayana kwamba usimulizi wote huwasilisha hadithi ambayo ni mfululizo wa matukio yanyowahusu wahusika. Hivyo basi usimulizi ni mfumo wa matukio yanayosababishwa na kuwaathiri wahusika. Ushairi ni usimulizi, hivyo basi ni kwa kutumia vigezo vya dhana hii ndipo usawiri mkamilifu wa uhusika katika ushairi umeweza kuonekana.

Utafiti umeweza kubainisha uhusika kwa mwongozo wa nadharia kwamba yanayosimuliwa katika shairi yanatokana na mhusika kupitia usimulizi wake ama anachokisimulia. Binadamu ndiye husimulia na masimulizi yanaweza kuhusu mhusika au kihusika. Kupitia utafiti huu imebainika wazi kuwa kuna uhusika dhahiri na uhusika usio dhahiri. Uhusika ulio dhahiri umebainika kupitia tabia na sifa za mhusika ama kihusika katika shairi, ilhali uhusika usio dhahiri umedhihirika kupitia maelezo kuhusu mwenendo wa mhusika ama kihusika kingine katika shairi. Utafiti vilevile umebainisha uhusika wa nafsi na uhusika rejelezi. Hapa utafiti tathmini imetolewa kuhusu matapo matano ya uhusika nafsi ambayo ni nafsi-peke, nafsi-uwili, nafsi-umoja, nafsi-wingi na nafsi-kikundi. Utafiti ulitathmini uhusika rejelezi kwa kubainisha mhusika ama kihusika kinachorejelewa iwapo ni msimulizi ama ni mhusika ama kihusika kingine katika shairi.

Tathmini ya uhusika inayochunguza mbinu na njia za kuumba wahusika na vihusika dhahania, na mbinu zote za uhusika wa umbo dhahiri, ambazo huwa za mazungumzo zilizotajwa hapo juu, zimesaidia utafiti huu kujibu maswali ya utafiti kwa kurejelea usimulizi kuhusu wahusika na

vihusika kama njia ya kutekeleza madhumuni yake. Tathmini ya uhusika  na mbinu za uhusika ni masuala yanayohusiana na maswali ya utafiti huu yanayochunguza iwapo uhusika katika ushairi upo kwa kuchunguza mashairi ya Kiswahili yaliyoteuliwa.

Mihimili ya uhusika kama ilivyofafanuliwa katika nadharia ya usimulizi ya Manfred(2005) ilifanikisha utafiti huu. Usimulizi unaeleweka na kutumika kuwa nadharia iliyo changamano na ufanisi wake kimatumizi na kiufasiri unategemea namna mtunzi anavyosimulia au kuwasilisha masimulizi ya wahusika. Namna mhusika anavyosimuliwa, njia na mbinu zinazomuumba hudhihirika kupitia usimulizi kwa kuwa ni kupitia kwayo aina za uhusika hubainika. Aidha tathmini faafu ya usawiri wa uhusika na mbinu za uhusika katika ushairi zimetambulishwa kwa kutumia mifano kutoka mashairi yaliyoteuliwa kutokana na diwani mbili na utenzi mmoja.

## 1.8 Hitimisho

Sura hii imeeleza usuli wa suala la utafiti na madhumuni ya kufanya utafiti huu. Aidha sura hii imeshughulikia upeo wa utafiti, misingi ya uteuzi wa mada ya utafiti. Maswali ya utafiti yameelezwa na madhumuni kubainishwa. Misingi ya kinadharia imefafanuliwa ambayo kwayo mihimili mikuu ya nadharia, dhana ya uhusika na usimulizi imeelezwa. Kutokana na mihimili hii vipengele vilivyoibua uhusika ni pamoja na aina mbalimbali za usimulizi, taswira mbalimbali na lugha. Vipengele vya usimulizi vinavyosawiri na kuibua uhusika ni usimulizi dhahiri na ule usio dhahiri. Kwa jumla imedhihirika kuwa ili uhusika kubainika lazima mtunzi aibue njia mwafaka za usimulizi. Njia zingine ziizotumika kuibua uhusika umbo, uhusika husishi na uhusika nafsi pia zimefafanuliwa. Hali hii inalifanya suala la uhusika kuwa faafu kufanyiwa utafiti. Dhana ya uhusika iliyofafanuliwa na Nadharia ya Usimulizi kwa mujibu wa Manfred (2005) pamoja na

Mbinu za Uhusika zilizobainishwa na Pfister (1977) ndizo zimeongoza utafiti huu. Sura hii imeonyesha msimamo wa utafiti kuhusu suala la uhusika katika ushairi wa Kiswahili. Uhusika unaweza kuibuliwa kupitia vipengele vingine na si lazima ujitokeze moja kwa moja.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDISHI

## 2.1 Utangulizi

Sura hii imetoa tahakiki mbalimbali kuhusu uhusika kwa jumla. Lengo likiwa kuhusisha tahakiki hizi na maswali na madhumuni ya utafiti huu. Mapitio ya maandishi yamegawanywa katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza imezungumzia dhana ya uhusika kwa jumla. Sehemu ya pili imejadili dhana ya uhusika katika usimulizi, hii ni kwa sababu mashairi mengi huwa ni masimulizi. Aidha imejadili uhusika umbo, uhusika dhahiri, uhusika usiodhahiri, uhusika nafsi na uhusika husishi. Dhana ya uhusika imefafanuliwa kama inavyoelezwa na wataalamu tofauti. Sura hii pia imehakiki yale yaliyoandikwa kuhusu wahusika na uhusika katika tanzu zingine za fasihi ya Kiswahili kwa lengo la kudhihirisha uwepo wa uhusika katika ushairi, pengo linalozibwa na utafiti huu.

## 2.2 Dhana ya Uhusika Katika Fasihi

Dhana ya uhusika imeshughulikiwa kama njia ya kuelewa chanzo chake na matumizi yake katika utafiti huu. Maoni ya wataalamu mbalimbali kuhusu dhana ya uhusika kama njia ya kuelewa suala la uhusika na kuonyesha umuhimu wake katika utafiti huu yametolewa. Utafiti huu umetoa tathmini ya uhusika kwa kuchunguza njia na mbinu za kufinyanga tabia na sifa bainishi za watu na vitu kupitia wahusika na vihusika kibunifu kupitia ushairi wa Kiswahili.

Fasihi ni sanaa kutokana na matumizi ya pekee ya lugha na vipengele vingine vya fani. Kwa pamoja lugha na vipengele hivi huipa fasihi sura maalum na kuyafanya maudhui yake yafikie

hadhira lengwa katika hali na umbo linalovutia. Hali hii ndiyo huiwezesha fasihi kutuingia, ikatuchoma na kutufikirisha zaidi. Aidha lugha ndiyo nguzo ya utamu wa fasihi. Katika misingi hiyo, uendelezaji wa fasihi; hasa kupitia uhakiki unapaswa kuzingatia pande zote mbili za sarafu; yaani lugha na vipengele vingine vya fani hujenga maudhui hayo. Uchunguzi huu umelenga kuzingatia kipengele cha usimulizi na mchango wake katika kubainisha wahusika hususan katika baadhi ya mashairi katika diwani ya *kichomi, Malenga wa Vumba* na *Utenzi wa Fumo Liyongo.*

Dhana ya uhusika imeelezwa kwa namna mbalimbali. Aristotle (322 KK) alifafanua uhusika kama suala muhimu katika Nadharia ya Tanzia Katika Ushairi. Alieleza kuwa mbali na ploti, fikra, ufafanuzi wa maana ya maneno, nyimbo na maonyesho, mhusika huchukua nafasi ya pili muhimu. Mhusika ndiye nguzo ya ploti. Ni kutokana na msukumo wa hisia za ndani zilizoungana katika hali inayozua mgogoro kwa namna ambayo huathiri mfululizo wa matukio yanayosababisha huruma na woga kwa hadhira. Maelezo haya yanabainisha kuwa ni kutokana na uhusika katika utunzi ndipo ujumbe kutokana na shairi huweza kumuathiri msomaji au msikilizaji wa shairi kwa kumfanya kuhuzunika au aweze kufurahi. Wataalamu wa lugha wamefafanua dhana hii mhusika katika njia tofauti. Kuna wale wanaeleza wahusika kuwa watu au vitu vinavyosababisha matukio fulani kutokea au kutendeka. Msokile (1993) amebainisha wahusika kama vitu, wanyama au watu katika kazi ya sanaa. Pia mimea, mashetani na mazimwi yanaweza kuchukua nafasi ya wahusika.

Wamitila (2003), anafasili dhana hii kuwa uumbaji wa wahusika. Aidha neno hili hupewa au huitwa viumbe au vyombo katika kazi za fashi. Anasema kuwa uhusika hutumiwa kuelezea mbinu na mikakati inayotumiwa na mwandishi kuwasawiri wahusika katika kazi yake.Mhusika

katika fasihi ni kiumbe wa hadithini aliyebuniwa na msanii ili kuendeleza hoja na maudhui yake katika kazi yake. Mhusika husaidia katika kuendeleza mada nzima anayoizingatia msanii hususa kwa kufululiza vitushi na visa mbalimbali katika kazi ya msanii ili kuwafikia wasomaji au wasikizi wake. Aghalabu, kila kazi ya fasihi huwa na mhusika au wahusika na huwa wamebuniwa na msanii ili kuchukuana na anachotaka kukifafanua. Wamitila K. (2008) anatoa hoja kuwa wahusika ni watendaji wa matukio na matendoyanayokuza na kuendeleza dhamira na maudhui ya kazi za kifasihi. Ni vielelezo vinavyowakilisha viumbe wanaopatikana ulimwenguni.

Utafiti huu unabainisha kuwa ufanisi wa uwasilishaji wa ujumbe wa msanii mbali na kutekelezwa na lugha, hutekelezwa pia na uchaguzi pamoja na usawiri wa wahusika wake. Mhusika hupewa maneno, dhana, na hulka ambazo ni muhimu katika kujenga hadithi, dhamira na maudhui ya kazi ile. Kuwepo kwa mhusika katika kazi ya fasihi hutegemea hasa uwezo wa mtunzi wa kumuumba na kumsawiri. Mhusika huyo huenda akawa anawakilisha watu anaowafahamu mtunzi ambao pengine walimvutia kwa maumbile na tabia zao. Huenda akawa kiumbe ambaye mtunzi aliwasikia wenzake wakizungumzia au amesoma katika maandishi mengine. Vile vile huenda mhusika wake akawa mtu asiye na sura maalum, asiyeishi katika maisha halisi kwa sura na hata kwa umbo, lakini akawa ni kiumbe cha kubuni alichokiumba mtunzi kutokana na tajiriba yake maishani. Kwa hivyo mhusika ni kielelezo au kiwakilishi cha aina fulani ya watu waishio katika hali halisi ya maisha. Ndiposa Mohamed (1984:45), anatoa hoja kuwa wahusika Dude na Zuberi katika riwaya ya *Asali Chungu*(1980), wamehusishwa kwa maisha halisi ya jamii yake. Mathalan Dude ni mnyonge anayeonewa, basi anawakilisha wanyonge wanaoonewa; Zuberi ni bwana mkubwa mwonevu anayeonea, basi anawakilisha waonevu wanaoonea. Dude huyu si dude maalum kwa maana ya dude yeyote aishie

Madongoporomoka, bali ni Dude wa hadithi anayejaribu kukopa tabia ya mtu au watu wanaopatikana katika jamii ya mwandishi. Hivyo basi pana ile dhana ya kwamba vitendo wanavyowakilisha wahusika hawa ni vya kuaminika. Pana aina mbali mbali za wahusika tunaoweza kuona katika fasihi kulingana na tabia zao na jukumu lao hadithini. Katika fasihi ya Kiswahili twaweza kutaja kwamba pana aina mbili kuu za wahusika - wahusika bapa na wahusika duara. Hawa hawapatikani katika ushairi kutokana na muundo wa shairi kwa sababu mashairi hutumia lugha ya mkato hivyo basi kuwa vigumu kuwachora wahusika hawa.

Aristotle (322, KK) anafafanua mhusika kwa kuegemeahulkaya mtu hivyo basi kuzua sababu ya uteuzi au maadili. Kwake yeye mhusika anastahili kuwa mwema kwa vitendo na maneno. Hawana budi kuwa watoshelevu na hakika kutegemea tabaka la watu lililowakilishwa. Aidha wahusika ni sharti wawe halisi katika maisha na wenye mwenendo usiobadilika na iwapo utakuwa wa kubadilika basi ubakie vivyo hivyo wa kubadilika. Mtazamo wa Aristotle kuhusu maana ya mhusika umeegemea sana uelezi ikilinganishwa na ule wa uelekezi wa wasomi wengine. Abrams (1993) anaeleza wahusika kuwa wanadamu waliowasilishwa katika kazi ya kidrama au tamthilia ama usimulizi ambao hufasiriwa na msomaji kuwa wenye maadili, hisia na sifa bainifu zinazojitokeza kutokana na yale wanayosema na kutenda. *Utenzi wa Fumo Liyongo* ni masimulizi ya shujaa Liyongo, ambaye ndiye mhusika mkuu. Hivyo basi Abrams anawaona wahusika katika misingi ya matendo na mazungumzo ya watu. Mwenendo wa mhusika utaweza kuelezwa kutegemea hisia, matamanio na maadili kama unavyobainika katika kuzungumza na matendo yake.

Mtunzi anaweza kuwa mhusika na vile vile asiwe mhusika. Anakuwa si mhusika inapokuwa yale anayosema kwa hakika hayamhusu yeye bali anakuwa msimulizi tu wa mambo hayo. Aidha aweza kuwa mhusika iwapo yale yanayosemwa yanamhusu. Hivyo basi katika ushairi mtunzi huweza kuwa mhusika wakati anachukua nafasi ya usimulizi. Kupitia usimulizi taswira ya mtunzi huweza kujitokeza mbali na wale wahusika anaowasimulia. Suala la wahusika halina budi kuzingatiwa katika ushairi.

## 2.3 Dhana ya Uhusika Katika Ushairi wa Kiswahili

Mutiso (1982) alichunguza ushairi na kujikita kwenye maudhui katika *Malenga wa Mvita*. Katika uchunguzi wake hakushughulikia uhusika kwa namna yoyote ile. Ni kupitia wahusika ndipo maudhui huweza kubainika. Utafiti huu umeweka wazi suala la uhusika ili ieleweke kwamba pasipo na wahusika maudhui hayawezi kubainika.

Mwai (1988), katika uchunguzi wake wa mabadiliko katika ushairi wa Kiswahili alijikita katika utanzu wa Ushairi-huru. Alichunguza kipindi cha mabadiliko kwa kutazama maendeleo ya ushairi kutoka umbo lake la awali (jadi) hadi kuibuka kwa ushairi-huru. Anaeleza kuwa ushairi ni dhana inayomaanisha utungo wa aina yoyote usio wa nathari. Ushairi, hivyo basi hujumuisha miundo yote ya utunzi na unaweza kugawanywa katika maumbo kama vile tendi na tarbia. Anaendelea kusema kuwa, hatua za maendeleo ya kisanaa katika ushairi zina uhusiano wa kimantiki na wazungumzaji wa Kiswahili wa Afrika Mashariki. Anasema Ushairi-huru uliibuka si kutokana na kukereketwa kwa watunzi chipukizi waliotaka kuonyesha umahiri wao na hivyo kukiuka arudhi za utunzi zilizowekwa na wanajadi. Ushairi-huru uliopo sasa ni utanzu mpya uliozuka kutokana na mabadiliko na ukuaji wa jamii ya wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili

Afrika Mashariki hususan baada ya uhuru. Hakueleza namna wazungumzaji hao wanavyoibuliwa katika ushairi. Ufichuzi huu ni muhimu sana kwa utafiti huu kwa sababu umeshughulikia uhusika katika ushairi unaozingatia arudhi za utunzi na ule usiozingatia arudhi za utunzi. Utafiti huu ulitathmini namna uhusika unavyojitokeza na kupambanua aina za uhusika kutokana na maudhui yanayobainika kupitia wahusika. Aidha utafiti ulichunguza namna taswira huumba wahusika katika ushairi huru ambao ni utanzu mpya uliozuka kutokana na mabadiliko na ukuaji wa jamii ya wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili.

Mulokozi (1989) ameeleza na kupambanua mambo makuu yanayoumba shairi, hasa la Kiswahili. Anasema kuwa mambo hayo ni fani, maudhui na muktadha. Anaeleza kuwa kwa kawaida mshairi hatungi ili kueleza maudhui fulani kutokana na muktadha fulani au kwa ajili ya muktadha fulani. Shabaha hiyo ya mshairi hutimizwa kwa kutumia fani na hudhihirika kifani. Hivyo ingawa maudhui hutawala fani kwa maana ya kuwa mtunzi huanza na wazo ambalo yeye hulitafutia fani ya kulieleza, lakini fani vilevile huathiri maudhui hayo, maana maudhui yamo ndani ya fani na hudhihirika kifani. Hivyo ili kulichambua shairi kwa muktadha wa uumbaji wa wahusika sharti kwanza tuviainishe na kuvielewa vipengee vya kifani ambavyo ni muundo, wahusika, na mtindo. Anasema mashairi ya kawaida hayategemei sana wahusika ili kuwasilisha ujumbe wake hata hivyo yapo mashairi ya masimulizi kwa mfano tendi ambayo hutumia wahusika kujenga maudhui yake. Uchambuzi wa mashairi ya aina hiyo lazima uzingatie pia dhima na taswira ya wahusika hao katika ujenzi wa matukio na maudhui ya utendi huo. Anaeleza kuwa ushairi hauelezi tu, bali hudhihirisha, huonyesha kisha husawiri uhusika. Ni kupitia uhusika ndipo maelezo yanaweza kutolewa yakadhihirika, yakaonyesha na kumsawiri mhusika ama kuwasawiri wahusika. Ushairi huwajumuisha wahusika wawili au zaidi kihisia katika tukio

linalowagusa wote, ukawatosa katika dimbwi la uchungu, au furaha, hasira, au ridhaa na kuwatoa tena.

Kutokana na maelezo haya ni dhahiri kuwa Mlokozi(1989) amegusia uchambuzi wa mashairi kwa muktadha wa uumbaji wa wahusika kwa kuviainisha vipengee vya kifani tu. Hakujishughulisha na vipengele vingine kama vile usimulizi na taswira kutathmini namna uhusika unavyojitokeza au jinsi vinavyoibua uhusika. Utafiti huu ulidhamiria kudhihirisha hali hizi zilizoelezewa kwa kuthibitisha uumbaji wa wahusika upo katika ushairi ili kufanikisha madhumuni ya kuchunguza taswira ya wahusika katika ushairi wa Kiswahili. Uumbaji ulibainika kupitia masimulizi ya mtunzi yaliyosawiri wahusika kupitia taswira za  usikivu, mguso, uoni na vionjo.

Momanyi (1991) alifanya utafiti kuhusu Matumizi ya Taswira Kama kielelezo cha Uhalisi Katika *Al-Inkishafi*. Taswira aliyoshughulikia inahusu wahusika na vihusika lakini hakubainisha namna taswira mbalimbali zinavyoibua uhusika na vihusikakatika kazi yake nahivyo kuacha pengo lililohitaji kushughulikiwa. Utafiti huu umedhihirisha utokeaji wa uhusika, usawiri wa uhusika na aina za uhusika katika ushairi kupitia vipengele vingine kama vile usimulizi.

Simala (1991) alichunguza Fani Katika Utenzi wa Wadachi Kutamalaki Mrima. Katika kazi yake alishughulikia vipengele vya fani kwa jumla. Uhusika ni kipengele kimoja cha fani alichokishughulikia japo hakubainisha ni kwa namna gani  kipengele hiki kinavyoibuliwa. Utafiti huu umebainisha kuibuliwa kwa uhusika kupitia vipengele vingine kama vile usimulizi na uzungumzi nafsi.

Indede (2011) alishughulikia taswira ya mwanamke katika wasilisho lake. Katika wasilisho hilo alitazama tu utata wa mwanamke katika (mazingira) mashairi ya kisasa. Hivyo basi ameshughulikia mhusika mwanamke katika mashairi na siyo jinsi uhusika wa mwanamke unavyoibuka katika ushairi. Hakuchunguza vipengele vinavyosababisha utokeaji wa mhusika mwanamke au namna anavyoumbwa katika ushairi wa Kiswahili. Utafiti huu umechunguza kuibuliwa kwa uhusika kupitia vipengele vingine kama vile usimulizi na lugha.

Uhusika umeshughulikiwa katika uchunguzi wa watafiti hawa lakini maswala waliochunguza hayakujikita katika uumbaji wa wahusika mbalimbali au uhusika unavyoibuliwa katika ushairi. Kutokana na mchango wa tafiti hizi, utafiti huu umeweza kudhihirisha uwepo wa uhusika katika ushairi wa Kiswahili kwa kuchunguza vipengele mbalimbali vinavyoibua uhusika katika ushairi wa Kiswahili ili kujaza pengo lililoachwa.

Wasomi wamefafanua dhana hii mhusika kwa njia tofauti. Aristotle (322 KK) anaeleza mhusika kwa kufafanua aina ya binadamu hivyo basi kuzua sababu ya uteuzi au maadili. Kwake yeye mhusika anastahili kuwa mwema kwa vitendo na maneno. Hawana budi kuwa watoshelevu na hakika kutegemea tabaka la watu lililowakilishwa. Aidha wahusika ni sharti wawe halisi katika maisha na wenye mwenendo usiobadilika na iwapo mwenendo huo utakuwa wa kubadilika basi ubakie vivyo hivyo. Kwa mujibu wa maelezo haya msanii yeyote wa kazi za fasihi alihitajika kuwasilisha kazi iliyohusu wahusika wenye maadili mema tu ili wawe vielelezo kwa jamii. Fasihi ni kioo cha jamii hivyo basi katika jamii kuna watu wema na wabaya na fasihi inastahili kuangaza vitendo vya watu hawa wote bila kubagua. Wanaotenda mema waweze kuigwa na

wale wanaotenda maovu waweze kumulikwa pamoja na matokeo ya matendo yao maovu ndipo jamii iweze kujifunza kutokana na uhusika wao. Mtazamo wake kuhusu maana ya mhusika umeegemea sana uelezi ukilinganishwa na ule wa uelekezi wa wasomi wengine.

Abrams (1981) anaeleza wahusika kuwa watu waliowasilishwa katika kazi ya kidrama au tamthilia ama usimulizi ambao hufasiriwa na msomaji kuwa wenye maadili, hisia na sifa bainifu zinazojitokeza kutokana na yale wanayosema na kutenda. Anawaona wahusika katika misingi ya matendo na mazungumzo ya watu. Mwenendo wa mtu fulani utaweza kuelezwa kutegemea hisia, matamanio na maadili kama unavyobainika katika kuzungumza na matendo yake. Kwa mujibu wa mwenendo usiobadilika wa mhusika, Abrams na Aristotle wanakubaliana kuwa mwenendo huo wa mhusika unahitajika kuwa imara kijumla, usiwe ule unaobadilika vivi hivi. Abrams anaongezea kwa kusema kuwa, mhusika anaweza kupitia mabadiliko makubwa kutokana na mfumo wa polepole wa kufanya jambo ama kutokana na mgogoro. Utafiti huu kupitia vipengele vya usimulizi, taswira mbalimbali na lugha umeweza kuibua uhusika kutokana na mabadiliko mbalimbali wanayopitia. Aidha mgogoro unaweza kuibuka tu kupitia masimulizi ama mtagusano kati ya wahusika. Ni kupitia masimulizi na mitagusano ndipo hulka na sifa za wahusika zinaweza kubainika. Utafiti huu ulichunguza masimulizi na mitagusano hii ndipo uhusika ukaweza kuibuliwa.

Miruka (1994) anasema neno mhusika limetumika kumaanisha tofauti iliyoko katika mazungumzo ya watu, tabia, matendo na maingiliano yao na watu wengine. Ufafanuzi huu unamweleza mhusika kuwa kile kinachomfanya mtu mmoja kuwa tofauti na mwingine. Maoni ya wataalamu hawa yanachukulia mhusika kuwa binadamu tu wala si vitu au viumbe wengine.

Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kubainisha aina za uhusika katika ushairi wa Kiswahili. Uhusika siyo ule unaohusu binadamu tu.Utafiti huu umebainisha kuwa mbali na wahusika binadamu kuna vihusika na viumbe wengine katika ushairi wa Kiswahili.

Foster (1972) anabainisha kati ya mhusika bapa na mhusika duara. Mhusika bapa ni yule anayetambulika kwa tabia moja na huwasilishwa pasipo na maelezo mengi kumhusu. Hapa inamaanisha kuwa, toka mwanzo hadi mwisho, wahusika hawa wameumbwa kwa kuzingatia sifa moja na kuishi na sifa hizo bila kubadilishwa na wakati, mazingira au uhusiano wao na wengine. Wanatumiwa kama chombo kilichotayarishwa kutimiza lengo, bila kujali hali za kawaida za kimaisha. Mhusika mviringo kwa upande mwingine ni yule changamano katika mwenendo na hisia. Hawa ni wahusika ambao wana desturi ya kubadilika kitabia, mawazo au kisaikolojia. Maisha yao yanatawaliwa na hali halisi za maisha. Hivyo wanavutia zaidi kisanii, kwani wanasogeza hadithi na kuielekeza kwenye hali ya kutendeka au kukubalika na jamii. Mtaalamu huyu ameshughulikia wahusika katika tanzu za fasihi zinazotoa maelezo marefu kumhusu mhusika.  Hakugusia uhusika katika utanzu wa ushairi unaotumia lugha ya mkato. Utafiti huu umechunguza uibuaji wa uhusika katika ushairi kupitia vipengele vya usimulizi, taswira na lugha ndipo wawe vyombo vya msanii ili kutimiza malengo aliyodhamiria msanii.

Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kutathmini uhusika unavyojitokeza katika ushairi wa Kiswahili. Uhusika umeweza kutekelezwa kwa kutoa maelezo ya moja kwa moja na ufafanuzi kuhusu mhusika mathalan maelezo kuhusu tabia au tambo lake. Maelezo mengine yametokana na yanayosemwa na mhusika. Hivyo basi utafiti umeweza kuchanganua fikra na hisia za mhusika. Matendo ya mhusika dhidi ya wahusika wengine katika shairi yameweza kutoa taswira

ya fikra, hisia, athari na namna mhusika anavyoathiriwa na wahusika wengine hivyo basi kuibua uhusika. Kuelewa hisia na fikra za mhusika inamwia rahisi msomaji kumwelewa mhusika. Matendo ya mhusika na jinsi yanavyoathiri na kuathiriwa na wahusika wengine yameweza kuelezwa ili kutoa taswira kamili ya mhusika.

Mbali na ufafanuzi wa uhusika uliotolewa na wataalamu, uhusika unaweza kumaanisha dhana dhahania zinazowasilishwa katika kazi za kidrama na za masimulizi. Dhana zilizo na sifa adimu na zinazoweza kuingiliana ama kuhusiana na mawazo au hoja kama ilivyo kwa binadamu walio na maadili na sifa za kihisia zinazoweza kuonekana. Aidha lugha ya kifasihi huwezesha dhana zisizo na uhai kutekeleza haya. Ili kufanikisha madhumuni ya utafiti huu uhusika umetumiwa kama dhana ya kurejelea viumbe, vitu na hali. Hivyo basi utafiti umetumia virejelewa hivi kumaanisha wahusika kwa kuchunguza matendo au vitendo vyao dhidi ya viumbe au wahusika na vihusika vingine na namna wanavyoathirika au vinavyoathirika kutokana na matendo ya viumbe vingine au mazingira.

Kutokana na maelezo haya inaeleweka kuwa mhusika ni mshiriki katika kazi ya sanaa. Aidha uhusika ni sifa na thamani zinazoweza kuelekezwa kwa mshiriki kwa kuzingatia matendo, fikra na mazungumzo au yote kwa pamoja. Ieleweke kuwa mshiriki katika kazi ya sanaa si lazima awe binadamu bali vyombo vinaweza kutumiwa, mawazo na maswala kuwa viwakilishi vya binadamu. Hivi ni kusema kwamba tunahuisha dhana zisizo za kibinadamu. Mbali na mwandishi kufichua ukweli na kujaribu kufikia uhalisi mwandishi atumie kipawa chake kuchora wahusika na mazingira yanayokubalika katika jamii ya wakati wake kwa sababu yana ule uhalisi

unaoaminika. Uhakiki uliofanywa katika utafiti huu ulizingatia kipengele cha aina za uhusika na namna ambavyozinajitokeza katika ushairi wa Kiswahili.

## 2.4 Namna Uhusika Unavyojitokeza Katika Ushairi

### 2.4.1 Dhana ya Uhusika Nafsi

Uhusika huu hujitokeza katika mfumo wa uzungumzi nafsi wa ndani ama kwa kupitia taarifa halisi kupitia usimulizi wa nafsi ya kwanza. Uhusika nafsi huhusishwa na mikakati ya kujiondolea aibu, kujitakia makuu na masuala mengine yanayomhusu mhusika. Massamba (1983) amegawa aina za uhusika katika ushairi katika matapo matano.

#### 2.4.1.1 Uhusika wa Nafsi - Pekee

Massamba (1983) anasema katika uhusika wa namna hii mtunzi mwenyewe huwa anaongea na nafsi yake. Inaweza kuwa ni kwa madhumuni ya kuuasa moyo wake, kujifariji ama kujipa imani katika kutenda jambo. Mathalan katika ubeti wa tano katika shairi *Narudia nitokako*(Boukheit, 1981, uk. 44) uhusika huu unadhihirika pale ambapo msimulizi anasema;

Shati langu dio vazi, nalivaa kwa ghadhiba,
Kisha nichochee moto, nipike chai ya baba,
Chai mbali ya watoto, nayo nipike ya shiba
Nauasi mkataba, nirudie nitokako.

#### 2.4.1.2 Uhusika wa Nafsi – Uwili

Katika uhusika huu Massamba (1983) anasema kuwa kuna watu wawili wanaojibizana. Majibizano yanaweza kuwa kati mtunzi na mtunzi mwingine. Aidha panaweza kuwa na watu zaidi ya mmoja katika upande mmoja na watu zaidi ya mmoja katika upande mwingine hali

kadhalika. Mradi panakuwa na pande mbili zinazojibizana. Uhusika huu unadhihirika zaidi na mara nyingine unatumika katika ngonjera na malumbano. (Boukheit, 1981, uk. 41) ametumia uhusika huu katika shairi 'Ufunguo wa maisha'. Mtunzi amewasilisha masimulizi ya pande mbili katika utungo. Nafsi neni ni baba ilhali nafsi nenewa ni mwana hivyo basi kuibua uwili wa nafsi.

Baba: Mwanangu njoo karibu, nikupe ya manufaa,
Uyajue ya wajibu, uepukwe na balaa,
Usije kupata tabu, dunia ina hadaa,
Katika ya manufaa, mojawapo ni elimu.

Mtoto: Usidhani meduwaa, nakusikiza hababu,
Bongoni metapakaa, uliyofuwa dhahabu,
Ujinga ngezuwa baa, na mangi yangenisibu,
Kutojuwa kuna tabu, elimu ni manufaa.

### 2.4.1.3 Uhusika wa Nafsi - Wingi

Katika uhusika huu msimulizi huzungumza kwa niaba ya kundi fulani la watu ambalo yeye ni mmoja wao. Hapa mtunzi hutumia nafsi ya kwanza wingi na huwa anazungumzia jambo linalomhusu yeye na hao ambao yeye ni mmoja wao. (Boukheit, 1981, uk. 41), katika shairi *'Uhaba wa kazi'* nafsi neni ni mwanamke akiwasilisha maoni ya wanawake:

Baba mbele mama nyuma, yamekuwa simulizi
Muradi sote twasoma, soteni tuwe walezi,
Wake haturudi nyuma, tunataka mapinduzi,
Maisha ya siku hizi, watu ni bega kwa bega.

### 2.4.1.4 Uhusika wa Nafsi - Umoja

Katika uhusika huu mambo ayasemayo mtunzi huwa yanaelekezewa nafsi moja tu. Mambo haya yanaweza kuwa ni maonyo, maelekezo au mawaidha mbalimbali, au pengine yaweza kuwa ni

sifa za huyo mtu. (Boukheit, 1981, uk. 40), katika shairi '*Ishi tashufu ghulamu'* ubeti ufuatao anamwelekezea kijana maonyo:

Watupita kwatukwatu, mijiatu kuiliza
Na kuwadharau watu, kujiona wapendeza,
Vyaja kutoka viatu, urudi hali ya kwanza,
Dunia yazongomeza, ishi tashufu ghulamu.

### 2.4.1.5 Uhusika wa Nafsi - Kikundi

Katika uhusika huu mhusika huwa ni kikundi cha watu. Hivi ni kusema kwamba msimulizi huwa ni kikundi cha watu. Aidha msimulizi aweza kuwa mmoja wa washiriki walio wengi. (Boukheit, 1981. uk. 30) katika shairi 'Bidhaa zakosa soko' ametumia uhusika huu.Kuna matumizi ya viambishi viwakilishi vya nafsi ya wingi mathalan 'tu' katika maneno kama vile 'tuliyozaa'katika ubeti ufuatao:

Mazao tuliyozaa, mema yenye nang'aniko,
Yavutia matufaa, maembe na matomoko,
Maghalani yamejaa,tama tembe haiko,
Zatupa misukosuko, bidhaa kukosa soko.

Uhusika nafsi umedhihirika kupitia usimulizi wa mtunzi. Kutokana na maelezo ya mtunzi msomaji anapata taswira ya yule aliyeelekezewa au kitu kilichoelekezewa masimulizi. Kutokana na masimulizi msomaji anabaini iwapo yanamrejelea mshairi mwenyewe, hivyo basi kuibua uhusika simulizi wa nafsi.

## 2.5 Aina Za Uhusika

### 2.5.1 Uhusika Umbo

Uhusika wa aina hii hutaka kujua utambulisho wa uhusika unaorejelewa. Manfred (2005) anaeleza kuwa katika uhusika-umbo kinachochukua sehemu ya uhusika huwa haswa mtu au kitu

au hali. Katika kiwango cha uhusika usio dhahiri anayechukua nafasi ya mhusika anaweza kuwa mtu, mnyama, kitu au hali yenyewe inayorejelewa. Kinachojitokeza katika uhusika huu ni kwamba kinachorejelewa ni mtu au kitu au hali.

Kulingana na Pfister (1991) mbinu zote za uhusika wa umbo dhahiri ni za mazungumzo. Amegawa mbinu hizi katika kategoria mbili. Kwanza ni utoaji maoni ya nafsi ambamo umbo huwasilisha na kupokea habari. Pili, ni utoaji maoni ya kando ambapo anayesababisha habari kutolewa si sawa na anayetoa maoni hayo. Maoni ya kibinafsi ni yale ambayo umbo hueleza dhahiri namna linavyojiona ilhali utoaji maoni kwa kando ni pale ambapo umbo moja huchukua uhusika dhahiri wa umbo lingine. Amefafanua maoni ya nafsi kwa kuyagawa kati ya yale ya uzungumzi-nafsi na ya usemezano. Ameyagawa hivikwa sababu kila moja ya aina hizi mbili za uhusika wa nafsi dhahiri zina viwango tofauti vya uaminifu. Japo uzungumzi-nafsi na usemezano kwa pamoja huwa umefungishwa na mwelekeo wa umbo fulani ambao waweza kuwa umebadilishwa kimakusudi. Maoni ya nafsi na usemezano huwa na vipengele vilivyobadilishwa kimakusudi kama vile malengo mbalimbali maalum na uchaguzi wa kimantiki unaochukuliwa na umbo kuelekea lingine katika usemezano na ambalo hushawishi umbo hilo kutoa tafsiri potofu ya matendo na malengo yake.

## 2.5.2 Uhusika Dhahiri

Kwa mujibu wa Manfred (2005), uhusika dhahiri hujitokeza pale hadhira huonyeshwa mambo yanayotambulisha nafsi ya mtu au kitu ambacho ni kihusika. Amefafanua njia tano tofauti za uhusika dhahiri. Kwanza ni kupitia unenaji, kinachofafanua mhusika ni kile anachosema na jinsi anavyozungumza.  Pili ni fikra za mhusika ambapo mambo yanayojitokeza kupitia fikra na hisia

zake za ndani huweza kufafanua ni mhusika wa aina gani. Tatu, mhusika anaweza kufafanuliwa kutokana na athari yake kwa wenzake. Hivyo basi yanayojitokeza kwa mhusika kutokana na athari yake anapotanagamana na wahusika au vihusika. Wahusika wengine wanahisi ama kudhihirisha tabia gani kutokana na mhusika au kihusika fulani. Nne, matendo ya mhusika yanaweza kutupa ufafanuzi wa mhusika na tano, jinsi anavyoonekana au kinavyoonekana machoni pa wasomaji au watazamaji. Ubeti ufuatao unadhihirisha uhusika dhahiri. Mshairi anasema;

Mfano. 1 Lau kwamba waelewa, lililo mwangu moyoni,
Katu hungalitobowa, kueleza hadharani,
Apendaye hana dawa, mwenye kupendwa haoni
Haoni wala hasikii, hafui wala hashoni,
Hendi wala hakimbii, haogi na hatamani,
Kazuia kii kii, wangasema majirani
Majirani wanganena, kumtia midomoni,
Na hata habari hana, musemayo asilani,
Yuko tuli amebana, awatazama machoni.
(M. Kamal Khan, (Mh.). *Tujifunze Mashairi*, Uk 53.)

Ubeti huu unaibua uhusika wa yule anayerejelewa. Kutokana na sifa na mwenedo wake hawezi kubadilika kwa kuwa yeye ameshafanya uamuzi. Fikra na hisia za ndani za msimulizi zinafafanua mhusika anayesononeka. Kuna maelezo ya wahusika wengine katika kutangamana kwao na mrejelewa. Maelezo ya wahusika wengine yanadhihirisha wanaavyohisi kuhusu huyu mhusika hali inayowafanya kumsema.

### 2.5.3 Uhusika Usio Dhahiri

Manfred (2005) anaeleza uhusika usio dhahiri ni taarifa ambayo inalenga sifa au tabia bainishi za kiutu za mhusika ambaye anaweza kuwa mzungumzaji mwenyewe ama mhusika mwingine yeyote. Mara nyingi uhusika usio dhahiri huwa na taarifa za maelezo kama vile sentensi zilizo na vitenzi kama vile ‘kuwa’ na ‘ana’ zinazotambua, kuweka katika kategoria, kuhusisha ama

kukadiria kiwango cha mtu. Ameeleza kuwa hukumu za uhusika zinaweza kuelekezewa tabia au sifa bainishi za kiutu za ndani, za nje au hata za mazoea.

Kulingana na Manfred (2005) uhusika usio dhahiri ni uhusika nafsi ambamo maumbile ya mtu ama tabia yake inadhihirisha tabia au sifa-bainishi za kiutu za mhusika kwa njia ya kuzungumza ama kwa matendo yake. Tabia au sifa bainishi za kiutu katika ubeti ufuatao zinadhihirisha mhusika ambaye amekataa kwenda shule hali inayomfanya msimulizi kumshauri aende shule ili asije kupata tabu siku za usoni. Mshairi anasema katika ubeti wa kwanza;

Mpenzi wangu Memomo, nyonda wangu una nini?
Vipi waiza kisomo, wataka uwe gizani?
Hebu simama kwa kimo uhudhurie shuleni,
Kila muiza kisomo, ajijengea ujinga.
(Aziz Abdallah Kiwillo na Khan 1981:9)

Tabia zisizo za kimazungumzo za mhusika zinaweza kudhihirisha uhusika wa mtu. Tabia au mwenendo wa kimazungumzo wa mtu kama vile anavyozungumza ama anavyosimulia katika hali mbalimbali huweza kueleza uhusika wa mtu, kama vile kiwango chake cha elimu kutokana na lafudhi au istilahi anazotumia au ni wa tabaka fulani katika jamii. Aidha aweza kuwa msema ukweli, mwenye tabia mbaya ama mkwepaji. Uhusika usio dhahiri unaweza kubainika kutokana na mavazi ya mhusika, maumbile kama vile kinundu na mazingira waliochagua kama vyumba vyao, magari yao au wanyama wanaowafuga. Maelezo ya Manfred (2005) na Pfister (1991) yanahusiana na masuali ya utafiti huu ambayo yalitaka kujua iwapo uhusika katika ushairi upo, aina ngapi za uhusika na namna waandishi wanavyosawiri ama kuwafinyaga wahusika katika tungo zao.

Utafiti huu ulibaini kuwa uhusika katika ushairi upo kwa kusoma mashairi yaliyodhihirisha uhusika nafsi ambamo maumbile ya mtu ama tabia ilidhihirisha tabia ua sifa za mhusika huyo kwa njia ya kuzungumza ama kwa matendo yake. Kupitia kuzungumza msomaji aliweza kutambua tabia ya mhusika mathalan mtu katili mwenye kiburi au mzinifu. Aidha utafiti ulibaini wahusika tajiri, wenye ulemavu, masikini kupitia uhusika usio dhahiri kutokana na maelezo kuhusu maumbile na hata mavazi yao.

### 2.5.4 Uhusika –Altero au Uhusika Husishi

Uhusika huu hujitokeza wakati wahusika wanapotoa maelezo jinsi wanavyofikiria kuwahusu wahusika wengine katika matini. Taarifa yoyote dhahiri ya mtu kumhusu mhusika mwingine vilevile ni uhusika nafsi usio dhahiri kwa sababu hutuangazia mwelekeo na maadili ya mtu huyo. Uhusika husishi umeelemewa sana na utabaka katika jamii. Hii inatokana na hali mbalimbali za jamii. Hivyo basi mhusika kutoka tabaka moja liwe la chini au la juu anaweza kuwa na fikira fulani kuhusu mhusika mwingine aliye katika tabaka tofauti na lake. Inaweza kutokea katika sehemu za kazi au katika mazingira ya nyumbani wanakoishi wanajamii, malengo madhubuti ya mhusika na uwajibikaji hususan kama suala lenyewe linahusu masuala ya umma.


Katika utafiti huu uhusika husishi ulidhihirika. Hali tofauti za wahusika na vihusika zilijitokeza. Mashairi yaliyosheheni wahusika kutoka matabaka tofauti yalifafanuliwa. Mathalan wahusika kutoka tabaka la chini wakisimulia kukasirishwa kutokana na dhuluma za wahusika walio katika tabaka la juu. Unyanyasaji wa wahusika wa jinsia ya kike ulidhihirika kupitia usimulizi wa wahusika wanawake. Kutokea kwa hali hizi ni dhihirisho kuwa uhusika katika ushairi upo.

Uhusika wa nafsi ulidhihirika katika mashairi mengi. Mshairi aghalabu hutunga katika mfumo wa uzungumzi nafsi wa ndani. Aidha mshairi hutunga kupitia usimulizi wa nafsi ya kwanza. Mshairi hutunga kuhusu masuala yanayomhusu, hivyo basi ujumbe mwingi uliyomo kwenye mashairi ni ule unaomgusa kwa njia moja ama nyingine. Kutokana na hali hii hapana budi uhusika wa nafsi kudhihirika katika utafiti huu.

Uhusika simulizi unamrejelea msimulizi na sharti utokane na nafsi fulani. Hadithi yoyote katika hali yoyote ile inapowasilishwa sharti pawe na yule anayesimulia matukio hayo. Katika kusimulia matukio hayo yule msimulizi ni mhusika. Katika masimulizi kuna mfululizo wa matukio yanayohusu mhusika ama wahusika. Hivyo basi uhusika simulizi hudhihirika katika ushairi kwa sababu ni mfululizo wa matukio yanayohusu mhusika ama wahusika.

Uhusika umbo hutambulisha mhusika ama kihusika kinachorejelewa. Katika uhusika huu masimulizi huweza kutoka kwa mhusika mmoja akirejelea mhusika ama kihusika kingine. Kwa kufanya hivi kuna umbo linalosimulia ama kuna kihusika kinachorejelewa. Mshairi ambaye husimulia hadithi hutambulisha umbo analolirejelea. Msimulizi anapotambulisha umbo katika tungo huwa anadhihirisha uhusika hivyo basi uwepo wa uhusika katika ushairi suala ambalo utafiti huu ulidhamiria kubainisha.

**Kielelezo cha 2 : Maelezo ya mwandishi na ya wahusika, mazungumzo na matendo yaletayo msukumo wa kuelewa matendo ya mhusika yanayoibua uhusika.**




Uchambuzi wa mashairi lazima uzingatie pia dhima na taswira ya wahusika hao katika ujenzi wa matukio na maudhui ya utendi huo. Ushairi hauelezi tu, bali hudhihirisha, huonyesha, husawiri uhusika. Ushairi huwajumuisha wahusika kihisia katika tukio linalowagusa wote, ukawatosa katika dimbwi la uchungu, furaha, hasira au ridhaa na kuwatoa tena. Kwa kufanya hivi ushairi unadhihirisha uwepo wa uhusika.

## 2.6 Uumbaji wa Wahusika Katika Fasihi ya Kiswahili

Maoni ya msanii na mtazamo wake kuhusu jamii yake ndio huthibitisha usawiri wa wahusika, hususan katika lugha na mawasiliano kisanii baina ya wahusika, kwa kuwa ni mazingira ya

kijamii ndio hujenga orodha ya kisanii ya mwanafasihi. Msanii huunda mikakati namna ya kuwasawiri wahusika, pia hujihusisha na jamii husika. Suala hapa ni kwamba matini na umbo husukwa ipasavyo na mtunzi ili kuunda maana kutoka katika ulimwengu wake. Styan (1960:69) anasisitiza hoja kwamba, ili kazi ya sanaa iweze kutia fora, msanii lazima atumie mtindo kama chombo ambamo ndimo mhusika atapewa mawazo ili kuyawasilisha kwa jamii. Kwa muktadha huu wahusika ndio vyombo vya kupitisha mawazo au ujumbe kwa jamii.

Uwezo wa msanii kuwahusisha watu vizuri kulingana na mawazo yake ni mojawapo ya sifa za usanii mzuri. Uhusiano huu umefanikiwa zaidi iwapo uumbaji wa wahusika utalingana na maisha halisi. Utungaji wa picha ya mawazo ya watu waliobuniwa kwenye hadithi, kiasi ambacho kwa msomaji wanaelekea kama ni hai hasa kwenye mipaka ya hadithi hiyo, ndio uumbaji wa wahusika. Wamitila (2003)amefafanua zaidi na kueleza kuwa ni kumjenga mhusika kwa kumpa umbo, wasifu, tabia na kueleza matendo yake. Mhusika huyu anaumbwa ili kuwakilisha tathmini maalum ya watu na matendo ya mtu. Na mtu huyo anayezungumziwa sio kama mtu binafsi, bali mfano wa watu wa aina yake. Hata hivyo, kila msanii ana mbinu zake za kuumba wahusika wake. Wakati mwingine, badala ya kutumia mbinu moja, wasanii wengine hutumia mbinu mbili au zaidi. Kutokana na maelezo haya mhusika anyezugumziwa ni binadamu. Ufafanuzi huu unazungumzia binadamu kwa sababu fasihi ni kioo cha jamii na jamii inayorejelewa hapa ni ya wanadamu au watu wala siyo vitu. Ni binadamu tu ndiye huwa na tabia na matendo fulani yanayoweza ama kukubalika au kukataliwa kama yasiyofaa katika jamii. Hivyo basi si watu tu huwa wahusika ila kuna vihusika ambavyo huumbwa ili kuwakilisha tathmini ya vitu na mifano ya vitu kama hivyo katika jamii.

Katika tenzi na mashairi ya jadi kinachozingatiwa sana ni zile arudhi za mashairi. Wahakiki wanapochambua mashairi haya huzingatia sana arudhi kama kwamba ndio muhimu katika utunzi wa mashairi. Mathalan, Mohammed (1977) anajishughulisha na mtindo, lugha na uchaguzi wa maneno yaliyotumiwa na mshairi katika diwani ya *Sauti ya Dhiki* (Abdillatif:1975). Mutiso (1982)alichunguza umbo, lugha, mtindo na maudhui mbalimbali katika diwani ya *Malenga wa Mvita* (Bhalo : 1971). Kipengele cha uhusika hakithaminiwi japo huwa kipo. Kujitokeza kwa mashairi huru kumebadilisha hali hii na kuhitajika uhakiki ulio tofauti unaojumlisha uhusika kama kipengele cha kuhakikiwa. Hivyo basi kwa kuwa ushairi huu hauzingatii arudhi basi hayatahitaji uhakiki kama si maudhui na dhamira tu. Utafiti huu ulichunguza uhusika katika mashairi haya kwa kuwa maudhui na dhamira ya mwandishi inaweza kueleweka kupitia uhusika. Mawazo mengi huhusu jamii na dhamira huwa ni kwa minajili ya watu wala si viumbe wasiohai.

Kezilahabi (1974)ameeleza kuwa shairi ni mtungo unaoeleza hisi za ndani za binadamu kwa mpangilio fulani wa maneno. Anasema awali ya hivi huzuka mawazo ya mshairi. Mawazo yake huletwa ama na mazoezi fulani katika mazingira yake ya kibinadamu au na uwezo wake wa kubuni au kufikiria hali hiyo akilini mwake. Kezilahabi (keshatajwa) ameandika kuhusu swali linalohusu maana ya maisha. Sauti inayosikika katika mashairi yake ni sauti ya mazungumzo na mnong'ono. Nafsi neni ni msanii mwenyewe akiwakilisha watu wa tabaka tofauti katika jamii. Kwa sauti hii ameweza kushikana mikono na kusalimiana na watu ambao wamekwisha kufa, ameweza kuwashangilia Machakulo, kusema machache na kina Rehema, Hadijah na kuzungumza na wajukuu. Hawa wanawakilisha watu wa kawaida katika jamii tunamoishi na ahera tusikokujua ila kufikiria tu. Amejali sana utumiaji wa picha au taswira katika ushairi. Taswira tofauti zimetumika ili kutoa picha halisi ya hali ilivyo. Ametumia taswira za uoni, na pia za mguso, aidha ametumia taswira ya usikivu. Ni kupitia taswira hizi mwanadamu anaweza

kupata picha na kutafakari maana yake.  Huu ndio uhusika kwa sababu ni kupitia wahusika ndipo ujumbe kuhusu makundi mbalimbali ya watu unaweza kupitishwa.

Wataalamu wengi wamefanya tafiti zao katika riwaya na tamthilia kuhusu uumbaji wa wahusika. Obura (1991) alichunguza usawiri wa wahusika wasichana na wanawake katika vitabu vya shule za msingi. Mule (1991) alichunguza namna wanawake wanavyowasilishwa katika tamthilia za Kiswahili zilizoandikwa na waandishi wanawake nchini Kenya na Tanzania. Kazi hizi zimechunguza uumbaji wa wahusika katika tanzu za tamthilia na riwaya. Katika kazi za watafiti hawa wanawake wameumbwa kama viumbe dhaifu walio na majukumu maalum tofauti na yale ya wanaume. Watafiti hawa hawakutathmini namna wahusika wanawake wanavyotokea katika ushairi, hivyo basi wamechangia tu utafiti huu kwa kuwa madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kuchunguza uhusika na usawiri wa wahusika na namna wanavyowasilishwa katika ushairi wa Kiswahili.

Mohammed (1977) katika tahakiki yake ya diwani ya *Sauti ya Dhiki* alijishughulisha na fani,hususan fani iliyotumiwa kuifinyanga *Sauti ya Dhiki* hata ikasibu kuwa sauti ya dhiki kweli yenye kuathiri msomaji au mwanafasihi yeyote. Anasema kuwa mshairi hawezi kuwa mshairi mzuri kama hajatekwa na kariha, au ghamidha au ghadhabu au yote kwa pamoja kabla hajaandika. Anajishughulisha na mtindo au muundo, lugha na uchaguzi wa maneno. Japo vipengele hivi vinaumba wahusika,  ameeleza namna vilivyotumika katika kufanikisha kazi ya fasihi kama vilekimaudhui tu. Hakutaja chochote kuhusu uhusika katika tungo za Abdilatif. Utafiti huu ulijishughulisha na uhusika ilikujaza pengo lililoachwa kutilia mkazo yale matokeo

ya utafiti wake kwa sababu mtindo au muundo, lugha na uchaguzi wa maneno unaweza kudhihirika kupitia wahusika.

Mugambi (1982), anasema kuwa sanaa ya fasihi ina ncha nne, kwanza kuna msanii, pili kuna mazingira, tatu kuna sanaa yenyewe na nne kuna hadhira. Mwandishi wa fasihi katika fani yoyote ile iwe ni tamthilia, riwaya au hata shairi huziandama ncha hizi nne. Mwandishi aweza kuzingatia sana fasihi yake kimuundo hivi kwamba hayajali yale mazingira yahusuyo maisha ya jamii kwa jumla. Mhakiki wa kazi hiyo atalazimika kuzingatia nadharia ya umuundo ili kubainisha mbinu ambazo mwandishi amezitumia katika tamthilia. Mbinu hizi zaweza kudhihirishwa katika uchoraji wa wahusika aidha kwa majina ya majazi, matumizi ya tamathali za semi, na matumizi ya vikengeushi. Utafiti huu umezingatia mbinu hizi kudhihirisha usawiri wa wahusika katika ushairi hususa ngonjera. Aidha mbinu zilizotumika katika utafiti huu ni usimulizi wa nafsi, taswira za mguso, uoni, usikivu na istiara.

Madhumuni ya utafiti huu nikuchunguza taswira ya wahusika katika ushairi wa Kiswahili. Utafiti ulidhamiria kuonyesha jinsi msanii alivyowaumba wahusika katika mashairi ya aina hii kwa kuwa uumbaji na usawiri wa wahusika ndilo swala kuu. Hivyo basi msomaji wa shairi anapata picha kamili ya mhusika au wahusika anaokutana nao katika mazingirahalisi.Msanii amewasawiri wahusika kuchukuwa sehemu tofauti ili kuonyesha hali inavyotokea katika hali halisi. Amedhihirisha tabia na matendo ya wahusika wanaoshiriki, mathalan polisi anayelinda sheria isivunjwe meneja na kijana anayetaabika kutafuta kazi. Hakimu amesawiriwa kutoa uamuzi ambao mara nyingi unatokana na hekima yake na siyo kutokana na kupokea rushwa.

Wazee wamesawiriwa kuchukua sehemu ya wazazi wanaoshughulika kwa ajili ya watoto wao kutopata kazi katika jamii.

Mutiso (1982), katika utafiti wake alichunguza umbo, lugha, mtindo na maudhui mbalimbali katika *Malenga wa Mvita* katika diwani ya Bhalo (1971). Alilinganisha kazi ya Ahmad na kazi nyingine za washairi wa Kiswahili wa Afrika ya Mashariki. Katika maelezo yake anafafanua maudhui kwa kusema kuwa ukweli kuhusu maisha ndicho kiini cha shairi lolote. Kama shairi likishindwa kutuonyesha ukweli fulani kuhusu maisha halina faida yoyote kwetu sisi wasomaji. Japo utafiti wake haukughusia uhusika, utafiti huu ulifaidika si haba kutokana na ufafanuzi huu kwa kuchunguza maudhui mbalimbali yanavyochangia kufafanua uhusika katika mashairi. Maudhui yanaweza kudhihirika kupitia uhusika ama masimulizi na matendo ya wahusika. Ni kwa kuchunguza usimulizi wa mafundisho kama haya na kama yanafuatwa au kutofuatwa katika shairi ndiposa kuibua uhusika. Utafiti uliweza kutambua washairi waliochukua sehemu ya uhusika ili kusimulia maovu katika jamii na kuhimiza uhusika wenye maadili, hivyo basi kuibua uhusika wenye maadili kupitia masimulizi.

Msokile (1993), amefafanua misingi mbalimbali inayozingatiwa katika kuhakiki ama kulichambua shairi lolote lile. Ameorodhesha vipengele hivyo kimojawapo kikiwa ni fani na maudhui kama vitu visivyotenganishwa. Anasema fani ni kipengele katika kazi ya sanaa. Ametoa mfano wa uhakiki wa shairi 'Ua la Moyoni' kutoka *Diwani ya Akilimali*. Akilimali (1970), na 'Siafu Wamekazana' kutoka *Mashairi ya Saadani* Saadani(1976). Kuhusu wahusika katika shairi 'Ua la Moyoni' anasema, hili linaonyesha kutumia wahusika wa aina mbili,

anaendelea kusema shairi hili lina wahusika watu na vihusika kama vile ua, kisha anasema uhusika wa ua katika undani wake unasimama badala ya  mtu ambaye ni mpenzi wa kike.

Katika shairi 'Siafu Wamekazana' anaeleza wahusika wanaotumika kwa nje ni wanyama kama vile nyoka na siafu. Aidha, anasema hiki ni kiwakilishi cha wahusika binadamu: nyoka ni mkoloni (mzungu), siafu ni Watanzania (weusi). Kuna shimo ambaloanasema ni nchi ya Tanzania. Anaeleza kuwa mwandishi amewajenga wahusika wake kwa njia za kitashihisi. Uhusika wa aina hii unatupa hisia ya hali ilivyo. Ni dhahiri kwamba amejaribu kuto

Madhumuni ya kwanza ya utafiti huu ni kutathmini uhusika kama unavyojitokeza katika ushairi wa Kiswahili. Katika shairi hili uhusika unaojitokeza ni wa hisi. Mtunzi ametumia taswira ya hisi kuibua uhusika. Hatuwaoni wahusika ama vihusika tunahisi uwepo wa wahusika na vihusika tu.Hivyo basi kupitia taswira ya hisi uhusika unaweza kuibuliwa. Mshairi anaibua wahusika wanyama na kihusika shimo katika shairi. Uhusika uliotumika umewakilisha hali halisi katika mazingira tunamoishi. Utafiti huu umefaidika sana na ufafanuzi huu wa uhusika na hivyo kudhihirisha uwepo wa uhusika katika ushairi wa Kiswahili kinyume na inavyofikiriwa na wahakiki wa mashairi. Uhusika unadhihirika kupitia taswira mbalimbali na hivyo kuziba pengo liliochwa na watafiti watangulizi katika utanzu huu.

Njogu (2004), anaeleza kuwa ushairi unaweza kutendwa kimazungumzo na watu wawili au zaidi ama kutungwa na mshairi mmoja ambaye huwapa wahusika wawili au zaidi maneno ya kuzungumza. Hata hivyo katika hali ambapo kuna mtendaji mmoja sauti nyingine inaweza kusikika chini kwa chini kutoka kwa mtendaji hivi kwamba yule mtendaji hujitokeza kama sauti

tofauti. Utafiti huu unabaini kuwa hizi sauti mbili zinazojihusisha katika majibizano ndizo zinazoibua uhusika. Ni kutokana na taswira ya usikivu msomaji wa shairi anaweza kueleza hulka yamhusika. Anasema kuwa kuna aina tatu za ushindani wa ushairi kama ifuatavyo: Kwanza ushairi usio wa usemezano, pili, ushairi wa usemezano ambao ni wa majibizano hasa baina ya washairi wawili na tatu ushairi wa usemezano hasa kati ya wahusika wawili waliowasilishwa hivyo kiuamilifu kutokana na utunzi wa mshairi mmoja. Hali hii ya usemezano huweza kuumba wahusika kutokana na yale wanayosema ama kujibizana. Msomaji anaweza kupata picha ya msemaji kutokana na mazungumzo yake na vile anavyomjibu mwenzake. Ni bayana ushairi wa mazungumzo na matendo ulikuwa wa mazungumzo kabla ya riwaya ya kwanza kuandikwa na hali inaendelea vivyo hivyo.

Kutokana na maelezo haya utafiti huu  umedhihirisha kuwa mazungumzo huendelezwa na wahusika wakizungumza kuhusu viumbe au vihusika vingine. Kupitia mazungumzo uhusika huibuliwa,  hivyo basi utafiti kukimu maudhui ya kwanza yaliyotaka kutathmini uhusika namna unavyotokea katika ushairi teule wa Kiswahili. Uhusika katika utafiti huu unaibuliwa na namna mitagusano mbalimbali inavyodhihirika kati ya wahusika.

## 2.7 Taswira ya Wahusika Katika Ushairi

Kwa mujibu wa maelezo kuhusu dhana ya uhusika, wahusika ni muhimu katika kazi ya fasihi kwa sababu huwa ni wazungumzaji wa msanii. Wahusika hupewa sifa zinazowasaidia kutekeleza kitendo au matendo fulani nayo matendo hayo huelekezwa kwenye maudhui na dhamira. Taswira ya wahusika huwa ni mwangwi au fumano la kijamii. Hivyo basi wahusika katika shairi

hujitahidi kupunguza masafa kati ya hali halisi katika jamii na msanii. Hapa ni pale ambapo watunzi hutoa taswira ya kama kwamba wao ni viumbe wanaoishi katika jamii halisi.

Fikra za msanii kuhusu jamii huwasilishwa na mhusika. Hivyo mhusika anapoongea au kujadili jambo, huwa anatoa kauli anayoifikiria msanii. Hivyo mhusika anapewa uwezo wa kufikiri na kutatua matatizo kulingana na maoni ya msanii na jinsi mhakiki anavyoelewa. Mhusika asiyefikiri si mhusika tena na sababu kubwa ni kwamba yeye ni mtu anayewakilisha watu iwe wenye fikra mbovu au nzuri, finyu au pana, fikra hizo bila shaka zinamuathiri msomaji. Msomaji huweza kutoa fasiri yake kulingana na namna anavyoelewa kazi husika ya kisanaa. Binadamu huchunguzwa na kuelezwa kutokana na fikra zake za kifalsafa kuhusu kazi, fikra za kisaikoloja na mambo mengine mengi. Haya huangaliwa kama aina ya matendo yake kwa upana ambayo yamekusanywa kutokana na uhusiano wake kijamii kupitia taswira ya wahusika.

Wasanii huiangalia dunia wanamoishi na watu wa jamii zao. Hapo ndipo yanapozaliwa mawazo kutokana na hali halisi waionayo wasanii. Msanii hutumia lugha kuweza kutoa fikra, rai au falsafa zake akizingatia wahusika ambao huwekwa katika mazingira yanayostahili kwa msomaji, hisi tofauti na mafundisho muhimu ili pale anapostahili aweze kukosoa. Utafiti huu umechunguza namna watunzi wanavyotumia maandishi na usimulizi kuwaelewa na kuwakuza watu. Mwandishi hufanya hivi kwa kujenga picha ya watu na vitu katika dunia wanamoishi, hivyo basi kukimu maudhui ya tatu ambayo ni kuchunguza taswira ya wahusika katika ushairi teule wa Kiswahili.

## 2.8 Uhusika Simulizi

Uhusika huu hutaka kutambulisha uhusika wa kirejelewa. Hivyo basi katika uhusika huu kinachorejelewa ni msimulizi. Manfred (2005) anaeleza usimulizi kuwa ni chochote kinachosimulia hadithi ama kuwasilisha hadithi iwe ni katika matini, picha, utendaji au hata jumla ya yote haya. Hivyo basi riwaya, tamthilia, sinema na vibonzo ni hadithi. Anafafanua kwa kusema kuwa hadithi ni mfululizo wa matukio yanayohusu wahusika. Matukio ni pamoja na yale halisi na yasiyo halisi kama vile mafuriko na ajali za magari. Wahusika huhusika wanapokuwa mawakala yaani vyombo vinavyozua matukio au waathiriwa pale wanapokuwa wagonjwa kutokana na hali mbalimbali katika mazingira kama vile ajali ama wanaopata manufaa kutokana na matukio hayo yanapowaathiri kwa njia moja ama nyingine.

Manfred (2005) anabainisha mhusika kwa kusema kuwa siyo mtu katika hali halisi ila ni kiumbe kwenye karatasi. Barthes (1975) anaeleza mhusika kuwa ni kiumbe kilichoumbwa na mwandishi ambaye anadhihirika tu katika matini ya kidhahania, katika kiwango cha kutenda ama katika kiwango cha maandishi bunia. Anasema neno umbo hutumika kama kisawe cha mhusika lakini wananadharia wengine hutumia kuelezea msimulizi. Ili kujibu swali ni nani anayezungumza? Au ni sauti ya nani iliyomo kwenye matini? Barthes (1975) anaeleza msimulizi ni yule anayezungumza au sauti ya mzungumzaji katika usimulizi. Yeye ni chombo ama wakala anayewezesha mawasiliano. Katika mashairi mengi hii sauti ndiyo husikika. Maelezo haya ya usimulizi na sauti ya mzungumzaji yamesaidia utafiti huu katika kuchunguza uhusika katika mashairi ya Kiswahili yaliyoteuliwa. Katika ushairi aina zinazoweza kumwelekeza msomaji au mhakiki kutambua mhusika au uhusika ni ufafanuzi kumhusu mhusika kwa kutoa maelezo yanayorejelea kimo chake, ama matendo yake. Iwapo ni kihusika maelezo yatatolewa kuhusu

hali ya kihusika hicho kama vile msitu wenye miti mirefu ama mto wenye kina kirefu. Aidha mwandishi anaweza kutumia ufafanuzi wa yale yanayosemwa na mhusika kuhusu mhusika aukihusika kingine katika shairi ili kuchanganua fikra na hisia za mhusika au kihusika. Mwandishi anapochanganua fikra na hisia zamhusika msomaji anaweza kumwelewa mhusika kwa kupambanua tabia na sifa za mhusika anayezungumziwa.

## 2.9 Usimulizi wa Nafsi Unavyoibua Taswira ya Wahusika na Vihusika

Mohamed (1995) anaeleza usimulizi wa nafsi ya tatu kuwa ni ule unaompatia mhusika mmoja nafasi ya kusimulia hadithi badala ya msimulizi mwakote kuisimulia yote. Katika usimulizi huu mwandishi anasimulia akitumia nafsi ya tatu lakini anajikita zaidi katika mhusika mmoja tu. Anajibana na kujipunguzia anayoyafahamu kwa kudhihirisha ufahamu wa mhusika mmoja peke yake. Yote anayoyajua ni kumhusu huyo mhusika na haonyeshi kuwafahamu wahusika wake wengine. Kwa hivyo, mawazo, mwelekeo na msimamo wa mhusika huyo mmoja ndio mwandishi anaoutambua kwa undani. Hapa mwandishi huwa amejipunguzia uhuru wake wa kuyaeleza yote anayoyajua kuihusu hadithi yake. Mhusika anayepewa nafasi hiyo aweza kuwa mhusika mkuu au mhusika mwingine yeyote hadithini.

Kuhusu usimulizi wa nafsi ya kwanza anasema, mwandishi hupotelea ndani ya mmoja wa wahusika wake ambaye husimulia hadithi yote. Mbinu hii si rahisi kama inavyoonekana, kwani mwandishi anapaswa kuwa makini asitumie neno ‘ni’ au ‘mimi’ mara nyingi ili asije akawachosha wasomaji wake. Japo mbinu hii hutumika kwa nadra katika fasihi ya Kiswahili, usimulizi huu humbana sana mwandishi kwani kuna mambo mengi sana ambayo hawezi akayaeleza bayana. Mathalan, mawazo ya wahusika wake wengine hayatatufikia vilivyo.

Itaonekana kuwa katika hali hii tunalazimika kutazama mambo kupitia kwa mtu mmoja, tunayemtegemea kutueleza mambo ambayo hatuyashuhudii wenyewe. Mwandishi anaweza kuamua kutumia mazungumzo baina ya wahusika, barua au mbinu nyingine ili kutupanulia mtazamo wa kazi yake. Carpenter na Neumeyer (1974: 184), kuihusu mbinu hii wanasema, wasomaji wanagenzi huweza wakachukulia kuwa msimulizi wa nafsi ya kwanza ana mawazo sawa na ya mwandishi. Si lazima iwe hivyo na wakati mwingine mawazo yake ni kinyume kabisa na yale ya mwandishi mwenyewe. Kwa hivyo ni makosa kuyaoanisha mawazo ya msimulizi wa nafsi ya kwanza na yale ya mwandishi kwani msimulizi kama huyo ni mhusika kama wale wengine hadithini na wala si lazima awe msemaji wa mwandishi.

Hata hivyo, mbinu hii ina faida zake. Wakati mwingine mwandishi hutaka tuutazame ulimwengu wake kupitia mhusika maalum, kama vile kijana mdogo, mama mzee. Tuyaelewe maisha kupitia mitazamo ya aina fulani ya wahusika. Kwa baadhi ya wasomaji, hadithi inayotumia usimulizi wa nafsi ya kwanza huwa hai zaidi kwani huifanya hadithi ifanane na maisha ya kila siku. Aidha katika usimulizi huu mwandishi huficha mambo ambayo msimulizi wake hayatambui mpaka pale ambapo yatahitajika katika maendeleo ya ploti, hasa katika hadithi za upelelezi.

Wahusika wanaweza kuumbwa kwa kutumia njia au mbinu yoyote ile, kati ya zilizotajwa au kwa kuchanganywa. Baada ya wao kuumbwa, msomaji anaweza kupata picha ya makundi tofauti ya wahusika, kutokana na hadithi moja au nyingine. Makundi hayo yanatokana hasa na uumbaji wa wahusika baada ya msomaji huyo kufanya mtengo wa wahusika (sifa, tabia na matendo yao) katika sehemu mbalimbali. Njia zinazotumiwa kufanya uchambuzi na mtengo wa picha za wahusika ni kwa kutumia ufafanuzi, mlinganisho na hatimaye mgawanyo.

Ufafanuzi ni njia ya kuzifahamu tabia za watu mbalimbali na matendo yao. Msomaji anamwelewa wazi mhusika huyo kulingana na maudhui ya hadithi, baada ya kulisoma shairi zima. Ili hadithi kuwa nzuri na kueleweka, lazima wahusika wafafanuliwe vyema. Mlinganisho hufanywa baada ya ufafanuzi wa msanii. Msomaji hulinganisha tabia na matendo ya wahusika katika shairi husika. Mgawanyo hutokana na ufahamu wa tabia na matendo ya wahusika ambapo msanii huwagawanya wahusika katika makundi mbalimbali ya wahusika. Msanii huwagawanya ili kuwafananisha kitabia au kimatendo. Kuna wahusika ambao tabia zao au matendo yao huweza kufanana au kutofutiana kwa njia moja au nyingine.

Attenbernd na Lewis, (1963); Carpenter na Neumeyer (1974) wanasema kuna baadhi ya waandishi ambao wanaitumia mbinu hii ya uhusika nafsi saikolojia kwa namna tofauti kidogo, na badala ya kutueleza tu mambo kuhusu hadithi, wanadokeza pia msimamo wao. Katika hali hii, mwandishi anaeleza mawazo au msimamo wa mhusika, anachanganua matendo yake na hata kufafanua bayana kinachoyazua matendo hayo. Zaidi ya hayo, anaweza hata kutoa tathmini ya wahusika wake kwa kufafanua hulka zao

Kutokana na uhuru wake, mwandishi anaweza kutoa maelezo yote na kuingiza mambo mapya bila lazima ya kueleza jinsi alivyoyapata. Uelewaji wa kazi hiyo kwa upande wa wasomaji huwa umerahisishwa kwani msimulizi atatamba kote kule hadithi inatukia na kuyaweka wazi matukio yote. Mwandishi anapotumia mfumo tulioutaja wa kutoa msimamo wake mara kwa mara anawakumbusha wasomaji kuwa ndiye ameibuni na wala wayasomayo si matukio ya kikweli; hasa iwapo wanamfahamu mwandishi mwenyewe. Kwa upande mwingine, matukio yanaposimuliwa bila kutolewa maelezo na mwandishi, kuna uwezekano mkubwa sana wa

wasomaji kutekwa na matukio hayo yanayojipambanua yenyewe bila kumkumbuka mwandishi. Mbinu ya msimulizi kutoa msimamo wake kuwahusu wahusika au matendo yao inamfanya aingilie kati badala ya kuwaachia wasomaji nafasi ya kutafakari na kujiamulia wenyewe. Utafiti huu ulibaini msimulizi huyu kuwa mhusika pale anapoingilia kati. Hivyo basi kumpa msomaji kazi rahisi ya kutafakari na kujiamulia.

Taswira ya vihusika ni mbinu ya mtunzi kuumba vitu visivyokuwa na uhai katika kazi yake ya sanaa kwa kutumia maelezo na ufafanuzi kiasi kwamba msomaji hupata fahamu ya kile kinachozungumziwa. Kutokana na maelezo na ufafanuzi wa mtunzi utafiti umeweza kutathmini uhusika kama unavyojitokeza katika ushairi wa Kiswahili. Kwamba uhusika ni jumla ya vihusika na wahusika katika kazi ya sanaa. Mtunzi hutoa taswira ya kile anachozungumzia. Mshairi anapotoa taswira ya kile anachozungumzia madhumuni ya tatu ya utafiti ambayo ni kuchunguza taswira ya wahusika katika ushairi wa Kiswahili yanadhihirika. Aidha jibu kwa swali uhusika katika ushairi wa Kiswahili hujitokeza vipi, limejibiwa kwa kuwa uhusika hujitokeza kama jumla ya wahusika na vihusika. Swali la tatu vilevile limejibiwa kwa kuwa mtunzi anatoa taswira ya kile anachozungumzia kwa kutuchorea picha ya kihusika ili kufafanua anachotaka kueleza.

## 2.10 Hitimisho

Kinachojitokeza katika mapitio ya maandishi haya ni kuwa uhakiki wa awali wa uhusika katika ushairi ni mchache. Wahakiki waliozihakiki kazi za ushairi walijikita sana katika fani hali ambayo imechangia katika kuelewa maendeleo ya ushairi. Dhana ya uhusika imejitokeza kama kipengele muhimu katika ushairi. Kupitia kwayo, msomaji huweza kuvutiwa na kutaka kuendelea kusoma shairi. Kwa upande mwingine, maelezo ya watafiti wa mashairi ya Kiswahili

yameonyesha kuwa dhana ya uhusika katika ushairi haijashughulikiwa kwa ukamilifu. Hivyo basi, inabainika wazi kuwa kuna pengo lililopaswa kuzibwa ambalo linahusu uumbaji wa wahusika hasa kwa kutumia vipengele vya usimulizi, uhusika umbo, uhusika dhahiri na uhusika nafsi kwa kubainisha namna vinavyoibua uhusika katika ushairi wa Kiswahili.

Uhusika katika fasihi umejadiliwa na wataalamu kadha kama Aristotle (322 KK), Mulokozi na Kahigi (1976), Massamba (1983), Abrams (1993),Njogu (2004). Jambo linalodhihirika ni kwamba uhusika katika ushairi hutofautiana na ule wa tanzu zingine za fasihi kwa kuwa haujitokezi waziwazi. Aidha katika ushairi kihusika au mhusika huwa tu pale ili msomaji aweze kutoa maelezo yanayomhusu au yanayokihusu kihusika. Aghalabu katika ushairi hujitokeza kama nafsi. Dhana ya uhusika ina maana moja katika fasihi, wao ni wazungumzaji wa msanii. Wahusika ama vihusika hupewa sifa zinazosaidia kutekeleza kitendo au matendo fulani nayo matendo hayo huelekezwa kwenye maudhui na dhamira.

Uhusika unaojitokeza katika ushairi una upekee wa aina yake tofauti na tanzu zingine za fasihi. Utafiti huu basi umedhihirisha maana ya dhana hii kwa kutilia maanani maoni ya baadhi ya wataalamu katika nyanja hii ya fasihi. Tathmini ya uhusika kama unavyojitokeza katika ushairi wa Kiswahili umeelezwa, aidha aina za uhusika katika ushairi zimejadiliwa na hoja kutolewa. Aina za uhusika katika ushairi zinapozingatiwa uhakiki na uchambuzi wa mashairi unaweza kuimarika kwa kuzingatia kipengele hiki. Utafiti huu umechukua mwelekeo wa kumuona mhusika kama mzungumzaji wa msanii. Mhusika na kihusika hupewa sifa ili kutekeleza maudhui na dhamira ya msanii, hivyo basi kutupa picha halisi ambayo ni taswira ya ulimwengu tunamoishi. Hata hivyo pengo linalojitokeza ni kwamba japo uhusika unamaanisha

wazungumzaji wa msanii haubainiki wazi katika ushairi. Utafiti huu ulidhamiria kubainisha uhusika kupitia vipengele mbalimbali vinavyoibua uhusika katika ushairi. Kipengele cha usimulizi na usemezano kimetumika kuibua uhusika.Aidha taswira ya mguso, uoni, vionjo na usikivu imetumika kuibua uhusika katika ushairi. Kipengele cha lugha vilevile kilitumika kuibua taswira ya wahusika hivyo basi kuziba mapengo yaliyoachwa katika tafiti za awali kuhusu suala la uhusika katika ushairi wa Kiswahili.

# SURA YA TATU

# NJIA NA MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii imetoa maelezo kuhusu muundo wa utafiti, njia na mbinu zilizoshirikishwa katika kukusanya data kuhusu uhusika wa ushairi kwa kuegemea Nadharia ya Usimulizi kwa mujibu wa Manfred (2005). Ukusanyaji wa data kutoka kwenye makala teule umefafanuliwa. Sura hii kwa jumla imegawanywa katika sehemu zifuatazo: Muundo wa utafiti, Njia za Utafiti, Idadi Lengwa, Sampuli na Usampulishaji na Mbinu za Ukusanyaji Data. Aidha sura hii imeeleza kwa kina jinsi data ilipatikana, uchambuzi na uchanganuzi wa data iliyokusanywa.

## 3.2 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ulichukua muundo wa kiuchanganuzi ambao ni uchunguzi wa kithamano. Uchunguzi wa kithamano ulifanywa kwa vile data zilizokusanywa ziliainishwa na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo. Mugenda (1999), anaeleza kuwa utafiti wa kithamano hutumia mpangilio na mbinu za utafiti ambazo hazitoi takwimu bali hutoa maelezo kiuchanganuzi. Richardson (1994), anasema njia mahsusi zinazotumika katika uchunguzi wa kithamano ni kusoma na utathmini wa makala. Utafiti ulihitaji kusoma kwa kina diwani mbili na utenzi mmoja. Hivyo basi utafiti huu ulipata data yake kwa kutathmini makala mbalimbali ili kuzifanyia uchanganuzi. Katika kutathmini makala data muhimu kuhusu utafiti iliweza kupatikana. Mugenda (1999), anaeleza kuwaili kutoamaelezo mufti kuhusu mada inayoshughulikiwa katika utafiti wa aina hii aghalabu hutegemea aina ya swali linaloulizwa na uchanganuzi wa data. Tarakimu zinazohusisha swala fulani hujaribu kutoa utatuzi kutokana na chanzo na athari ya jambo fulani hivyo basi kuwezesha

kuafikia madhumuni ya utafiti. Aidha katika kutathmini makala mihimili ya nadharia hurahisisha data muhimu kuhusu utafiti kupatikana.

## 3.3 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti lililoshughulikiwa ni la kimuktadha ambalo ni ushairi ambao ni utanzu wa fasihi. Usomaji ulizingatia nyakati za utunzi wa mashairi mbalimbali. Usomaji ulidhamiria kubainisha kinachofanya uhusika katika ushairi wa Kiswahili kujitokeza kwa namna ya pekee tofauti na tanzu zingine za fasihi. Tanzu nyingine za fasihi ni riwaya, hadithi fupi na tamthilia. Aidha kupitia usomaji kigezo cha usimulizi kilitumiwa kuainisha uhusika katika ushairi. Usomaji vilevile uliwezesha kubaini kuwa ushairi unatofautiana na tanzu nyingine kutokana na utumizi wake wa lugha ya mkato. Uhusika uliweza kupambanuliwa kutoka mashairi kupitia vipengele vya usimulizi. Kutokana na upambanuzi wa mashairi tofauti uliofanywa utafiti uliweza kutathmini namna uhusika unavyojitokeza, aina za uhusika na namna taswira huumba wahusika katika ushairi wa Kiswahili.

## 3.4 Sampuli na Usampulishaji

Utafiti huu ulitumia sampuli ya kimakusudi kuteua diwani mbili na utenzi mmoja miongoni mwa diwani tano na tenzi tatu za watunzi mbalimbali. Sampuli ya kimakusudi ni mbinu ya sampuli inayomkubalia mtafiti kutumia vipengele ambavyo vina maelezo yanayohitajika kulingana na maelezo ya uchunguzi wake. Kwa mujibu wa Enon (1998), anaeleza kuwa, uteuzi lengwa ni ule wa mtafiti wa kwenda moja kwa moja kwenye chanzo cha data anazozihitaji. Mtafiti alitalii tenzi na diwani za Kiswahili, na kuchagua *Utenzi wa Fumo Liyongo,* diwani ya *kichomi,* na diwani ya *Malenga wa Vumba.* Aliona Utenzi huo na diwani hizo, zitajibu maswali ya utafiti huu.

Vipengele vya kutafitiwa vilichukuliwa kwa sababu vina habari ama sifa zinazohitajika. Sampuli ya uteuzi safu isio na utaratibu ilitumiwa ili kupata uwakilishi ufaao kutoka kwenye vikundi vidogo vitatu vya mashairi. Mugenda (1999), anaeleza kuwa katika sampuli safu isiyo na utaratibu vipengele huteuliwa kwa namna kwamba sampuli itajumuisha vikundi viwili au zaidi. Katika utafiti huu ni vikundi vitatu ambavyo viliteuliwa kutoka utanzu wa ushairi. Hivyo basi katika safu ya mashairi ya arudhi mtafiti alichagua diwani ya *Malenga wa Vumba*, diwani ya *Kichomi* kutoka safu ya mashairi huru na *Utenzi wa Fumo Liyongo* kutoka safu ya tenzi. Sababu ya kuteuliwa nakala hizi ni kuwakilisha aina tofauti za mashairi. Utafiti ulichunguza mashairi manane ya arudhi, mashairi huru kumi na manne na utenzi mmoja.

*Utenzi wa Fumo Liyongo* uliteuliwa kwa sababu ndio utenzi wa zamani mno na maarufu uliowahi kutungwa katika mazingira hayo ya Uswahilini. Utenzi huu una matukio, vituko na masimulizi yanayohusu wahusika na vihusika. Japo kuna tenzi zaidi ya kumi, utenzi huu uliteuliwa kwa kusheheni mbinu na aina za uhusika zilizohitajika ili kuwakilisha tenzi.

Diwani ya *Malenga wa Vumba* iliteuliwa kwa kuwa imesheheni aina nyingi na bahari tofauti za mashairi yanayohusu matukio, vituko na masimulizi ya mtunzi kuhusu wahusika tofauti. Diwani hii iliteuliwa kuwakilisha mashairi ya arudhi au ya kimapokeo kama vile tarbia na ngonjera. Ni mashairi nane yaliyochaguliwa.

Diwani ya *Kichomi* iliteuliwa kwa kuwa ndiyo diwani ya kwanza ya mashairi-huru iliyowahi kutungwa iliyosheheni matukio, vituko na masimulizi ya mtunzi kuhusu wahusika na hali mbalimbali ili kuwakilisha mashairi huru, haya ni mashairi yasiyozingatia arudhi za ushairi.

Wakati wa kutungwa *Utenzi wa Fumo Liyongo* na mashairi mengine kama yale yaliyomo kwenye *Malenga wa Vumba* ushairi ulizingatia sana arudhi. Hivyo basi ni wale tu walioweza kutunga kwa kuzingatia sheria hizo waliweza kutunga tenzi zilizoweza kukubalika wakati huo. Ilikuwa vigumu sana kwa mtu yeyote kutunga hata kama alikuwa na ujumbe maalum wa kupitisha almuradi hakuwa na ujuzi wa utunzi. Hali hii iliwabana watunzi wengi waliokuwa na ujumbe wa kupitisha kwa jamii ikawa ni watu maalum waliokuwa mahiri katika tenzi na mashairi ya arudhi tu waliweza kutunga. Uhakiki wa mashairi nyakati hizo ulijikita katika arudhi ama sheria za kutunga mashairi. Kilichozingatiwa kwa dhati ni iwapo mshairi alifuata sheria za kutunga ndipo shairi likaitwa shairi. Iwapo palikuwa na kasoro katika sheria hizo basi shairi hilo lilichukuliwa kuwa si shairi hata kama lilikuwa na ujumbe mzito uliohusu jamii.  Mashairi kumi na manne yalichaguliwakutoka kitengo hiki ili kutathmini namna uhusika, aina za uhusika na kuchunguza namna taswira inavyoumba wahusika katika mashairi.

Ushairi huru kama unavyojulikana sasa ni ushairi usiozingatia sheria za kutunga. Kilicho cha muhimu katika ushairi huu ni ujumbe. Waasisi wa aina hii ya ushairi walionelea si vyema kujifunga tu katika sheria za kutunga ndipo mtunzi aweze kutunga mradi kulikuwa na ujumbe ambao ulihitajika kupitishwa kwa lugha ya mkato. Hivi ni kusema kwamba kwa kuwa ushairi ni sanaa ya lugha inayotumia lugha isiyokuwa ya nathari hapana makosa kama ujumbe utapitishwa kwa kutumia hiyo lugha ya mkato pasipo kufuata sheria za kutunga mashairi. Hivyo basi kutokana na mabadiliko haya  uhakiki wa vipengele vyote uhusika ukiwemo hauna budi kwenda sambamba. Uhakiki usizingatie tu arudhi za kutunga mashairi bali ushughulikie masuala mengine kama vile uhusika katika mashairi yao.

Data husika ilikusanywa kwa kuzingatia wakati na aina ya mashairi. Kwa kutumia kigezo cha wakati utafiti uliteua mashairi yaliyotungwa kale kwa kutaka kubainisha uwepo wa uhusika. Aidha utafiti ulitaka kubainisha tabia za wahusika  na namna wahusika wanavyoumbwa tangu awali katika ushairi wa Kiswahili. Tenzi ni kati ya mashairi ya kale sana, hivi ni kusema kwamba utafiti ulitumia *Utenzi wa Fumo Liyongo* (1973) ambao ni mojawapo wa tenzi zinazojulikana kuwa za kwanza kabisa kutungwa katika historia ya ushairi wa Kiswahili. Diwani ya*Malenga wa Vumba* (1981)inajumuisha aina nyingi nabahari mbalimbali za mashairi. Mashairi yote katika diwani hii yametungwa kwa kuzingatia arudhi za ushairi.Utafiti ulishughulikia mashairi haya kutathmini namna uhusika unavyojitokeza, kupambanua aina za uhusika na kuchunguza namna taswira huumba wahusika na vihusika.

*Kichomi* (1974) ni diwani iliyo na mashairi-huru. Ushairi wa aina hii ulichipuka katika karne ya ishirini. Haya ni mashairi yasiyozingatia arudhi za utunzi wa ushairi. Kwa kuwa yanakubalika kuwa mashairi, hapakuwa na budi kuteua mojawapo ya diwani katika kumbo hili la mashairi lililo na diwani zaidi ya kumi. Diwani ya *Kichomi* ndiyo ya awali kabisa iliyojumuisha mashairi huru mengi yanayohusu maswala mengi ya kijamii, hivyo basi kupelekea kuteuliwa ili kubainisha uhusika kwa kuchunguza namna uhusika unavyojitokeza katika mashairi haya. Kwa jumla utafiti huu ulichunguza mashairi ishirini na manane kutoka vikundi vitatu vya mashairi. Hivi ni kusema kwamba utafiti ulichunguza aina zote za mashairi katika nyakati tofauti na mazingira tofauti.

Katika uchunguzi na usomaji wa nadharia mbalimbali dhana ya uhusika kwa mujibu wa Manfred (2005) imejitokeza faafu kutumika katika utafiti huu. Kupitia kwayo utafiti umeweza kuchunguza uhusika unavyodhihirika katika mashairi kupitia usemezano, tabia za wahusika na njia ya usimulizi. Kwa kufanya hivyo utafiti umeweza kuibua matapo kadha ya uhusika katika ushairi wa Kiswahili na kudhihirisha kuwa uhusika katika ushairi upo na unastahili kushugulikiwa kama kipengele muhimu mbali na vipengele vingine wakati wa kuchambua na kuhakiki mashairi. Kupitia vipengele hivi, utafiti umeweza kugundua njia zote za uumbaji wa uhusika katika ushairi wa Kiswahili, hivyo basi malengo ya utafiti kuafikiwa.

## 3.5 Mbinu za Ukusanyaji Data

Utafiti huu ulitumia njia ya historia, maktabana mtandao ili kupata data za maelezo ambazo ziliwezesha kutimiza madhumuni ya utafiti.Ili kupata maelezo kuhusu uhusika mtafiti aliweza kusoma diwani mbili na utenzi mmoja. Aidha mtafiti alisoma majarida, vitabu na makala yaliyokuwa na maelezo kuhusu uhusika katika ushairi na uhusika kwa jumla. Aidha mtandao ulifaa sana kwa utafiti huu kwani maelezo na maswala mengine muhimu kuhusu uhusika katika fasihi kwa jumla yalipatikana. Utafiti ulipata maana mbalimbali za uhusika na namna ambavyo watunzi husawiri wahusika katika utanzu wa ushairi.

Kifaa kilichotumika ni orodha ya uchunzaji. Orodha ya uchunzaji iliwezesha kushughulikia mbinu zote zilizoibua uhusika kwenye mashairi yaliyoshughulikiwa. Njia hii iliwezesha data kupatikana hivyo basi kutekeleza malengo ya utafiti huu. Uchunguzi ulishughulika na data inayohusiana na mada ya utafiti na ambayo ingewezesha kutoa uamuzi na mapendekezo kwa mujibu wa kazi za ushairi zilizoshughulikiwa.Usomaji wa mashairi uliandamana na unukuzi wa

mashairi ambayo uhusika ulionekana kutokea kwa kurejelea vipengele vya dhana ya uhusika ambavyo ni usawiri wa wahusika na njia ya usimulizi. Idadi lengwa iliyoshughulikiwa ilikuwa mashairi ishirini na matatu. Njia hii imewezesha utafiti huu kukusanya data mufti inayolenga uhusika katika ushairi kwa kubainisha na kudhihirisha uwepo wa uhusika katika ushairi. Aidha mbinu hii ilimwezesha mtafiti kujadili aina za uhusika na ufundi wa mtunzi katika kufinyanga uhusika huo katika mashairi ya Kiswahili.

Utafiti uliweza kuzua data iliyohitajika kupitia aina tatu ya mashairi kwa kutumia orodha ya uchunzaji. Mtafiti alifanya upekuzi wa kina kwa kazi za wasomi na watunzi wengine wa mashairi. Kulingana na Mugenda (1999), njia ya usomaji wa makala, kunukuuu na kuzihakiki humpa mtafiti uwezo wa kurejelea makala hizo kwa urahisi iwapo pametokea kosa. Baada ya kusoma na kuhakiki mtafiti alitumianjia ya uchunzaji ili kuhakikisha kuwa data iliyohitajika ilitumika.

## 3.6 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

Uchanganuzi wa data ulifanikishwa baada ya data kuratibiwa katika makundi kwa kutumia mkabala wa kiuchanganuzi. Data zilipatikana kwa kudurusu diwani teule na utenzi mmoja ili kuchunguza uwepo wa uhusika, usawiri wa wahusika na aina za uhusika katika ushairi. Vipengele vinavyorahisisha kudhihiri kwa uhusika katika ushairi kama vile tabia za wahusika na usimulizi vilirahisisha kufafanua uhusika katika ushairi. Maswali na malengo ya utafiti yalizingatiwa katika kuratibu data katika matapo ili kujitokeza na maelezo ambayo yalizingatia hali halisi mintaarafu dhana ya uhusika, suala la utafiti na maswali ya utafiti.Uchanganuzi wa kimaelezo ulifanywa ili kuchanganua data zilizokusanywa maktabani. Ili kufanikisha utafiti,

tathmini mwafaka imetolewa kuhusu utafiti pamoja na kuangaza mianya ambayo imejitokeza. Kwa jumla uchambuzi na uchanganuzi huu umesaidia kupambanua uhusika unavyojitokeza, aina za uhusika na taswira ya wahusika katika ushairi wa Kiswahili.

## 3.7 Suala la Maadili

Kazi yote iliyomo humu ilifanywa na mtafiti mwenyewe chini ya usimamizi wa waelekezi wake. Utafiti huu haujafanywa katika chuo kikuu kingine chochote kile. Nukuu zote zimezingatia kanuni za unukuzi za ukusanyaji data kwa kuorodhesha vitabu, makala na majarida ya waandishi mbalimbali waliorejelwa. Masuala ya maadili yalizingatiwa vilivyo hivi kwamba utafiti huu ni halisi. Data zilizokusanywa ni kwa minajili ya utafiti huu kwa mujibu wa kitengo cha maadili katika utafiti katika Chuo Kikuu cha Maseno.

## 3.8 Hitimisho

Sehemu hii imejadili njia na mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu. Sampuli dhamirifu imetumika katika uteuzi wa diwani mbili na utenzi mmoja miongoni mwa diwani na tenzi nyingi. Mashairi nane yalichaguliwa kutoka diwani ya *Malenga wa Vumba*, kumi na manne kutoka diwani ya *kichomi* na *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Njia ya usimulizi imejitokeza kama mbinu ya kutumika kubainisha aina za uhusika na tabia za wahusika. Kupitia njia ya usomaji makala, utafiti huu umeweza kupata data inayotosha kujibu maswali ya utafiti huu. Njia hii imedhihirika kuwa inayofaa na kupitia kwayo malengo ya utafiti yaliyokusudiwa yameweza kudhihirika. Wingi wa data iliyokusanywa ulitosha kujibu maswali ya utafiti na kutosheleza madhumuni yake. Data hizi kwa pamoja zimepangwa kama inavyojitokeza katika sura inayofuata.

# SURA YA NNE

# UHUSIKA KATIKA TUNGO TEULE ZA USHAIRI WA KISWAHILI

## 4.1 Utangulizi

Sura hii imechambua kwa kubainisha, kuchuguza na kueleza njia zilizotumiwa na watunzi katika uumbaji wa wahusika katika diwani ya *Malenga wa Vumba* (1981), diwani ya *Kichomi* (1974), na *Utenzi wa Fumo Liyongo* (1973). Uchambuzi katika sura hiiumegawanywa katika sehemu tatu kuu. Utafiti umeelekezwa na mihimili ya uhusika iliyojikita katika usimulizi na vipengele vya uhusika kwa mujibu wa Manfred (2005). Vipengele vilivyozingatiwa ni uhusika-umbo, uhusika usio-dhahiri, uhusika dhahiri, uhusika-nafsi na uhusika husishi. Utafiti ulizingatia vipengele hivi ili kufikia madhumuni ya utafiti ambayo ni utokeaji wa uhusika katika ushairi wa Kiswahili.

Ili kufanikisha sehemu hii, mifano ya uhusika imetolewa kwa kila kipengele. Maelezo kuhusu vihusika na wahusika yametolewa kufafanua jinsi uhusika katika ushairi wa Kiswahili unavyojitokeza. Mbinu za usimulizi zinazoibua uhusika zimetolewa mifano. Kupitia njia hii uhusika unaotokana na usimulizi umeweza kuelezwa na kubainishwa ili kujibu swali kuhusu utokeaji wa uhusika katika ushairi wa Kiswahili. Madhumuni yalikuwa kutoa sifa za wahusika na vihusika katika ushairi. Ni baada ya kutambua wahusika na vihusika na kutoa sifa zao ndipo majukumu yao huweza kubainika.

Sehemu ya pili imeshughulikia aina za uhusika kwa kueleza jinsi aina hizo zinavyojitokeza katika mashairi teule ya Kiswahili. Ili kupata picha kamili ya vipengele vilivyoshughulikiwa,

maelezo juu ya dhana ya uhusika yametolewa kwa lengo la kuleta uelewa wa suala la uhusika. Mkondo uliochukuliwa kutambulisha uhusika kupitia usimulizi na njia zingine zimewekwa wazi kama njia ya kutimiza madhumuni ya utafiti huu.

Sehemu ya tatu imeshughulikia taswira ya wahusika. Njia ya usimulizi iliyotumiwa na watunzi katika mashairi kama njia ya kuibua uhusika imechunguzwa huku mifano maridhawa ikitolewa. Katika kubainisha uhusika, sura hii imetanguliza kueleza vipengele vinavyochangia kudhihirika kwa uhusika katika ushairi. Vipengele mbalimbali kama vile usimulizi, uhusika kiumbo, uhusika usio dhahiri, uhusika dhahiri, uhusika nafsi, na uhusika-altero au husishi ndivyo vinavyochangia kubainika kwa uhusika katika ushairi. Aidha katika uumbaji wa wahusika kipengele cha lugha hutumika. Uumbaji wa wahusika umeelezwa kwa njia ya uwasilishaji ambapo mtunzi ametumia uwasilishaji ulio dhahiri, uwasilishaji katika matendo, uwasilishaji kutokana nahisia za mhusika anapomrejelea mhusika mwingine, au uwasilishaji kutokana na uhusiano wake na wahusika wengine.

## 4.2 Usimulizi Unavyoibua Uhusika Katika Ushairi wa Kiswahili

Kuna mbinu nyingi za usimulizi ambazo mwandishi anaweza kuzitumia kuiwasilisha kazi yake katika maandishi. Aina za usimulizi hutofautiana kwa jinsi ambavyo zinazua athari tofauti kwa wasomaji. Kuna baadhi ambazo hutuongoza kumulika hisia zetu kwa msimulizi ilhali zingine hutuashiria kuangaza nadhari yetu kwa kile kinachosimuliwa. Msimulizi anaweza kuwa mhusika katika shairi au mtunzi wa shairi lenyewe. Kwa hivyo, mwandishi hupaswa kufanya uteuzi wa mbinu mwafaka ya usimulizi atakayoitumia kutegemea yale anayonuia kuyasisitiza katika kazi yake. Kupitia mbinu ya usimulizi iliyotumika, uhusika huweza kubainika.

Leberman na Forster(1968) wanasema usimulizi wa nafsi ya tatu unaweza kuangaliwakwa njia nne. Njia ya kwanza ni usimulizi maizi. Wasomi hawa wanasema msimulizi anazijua siri zote za wahusika na anaweza kujua tungo tangu mwanzo hadi mwisho kila wakati. Njia ya pili ni usimulizi tinde ambapo msimulizi anaeleza hisi, mawazo na mambo yanayojulikana na mhusika mmoja au wachache tu miongoni mwa waliomo katika hadithi. Njia ya tatu ni usimulizi horomo ambapo msimulizi hutoa habari tu na kuacha wahusika wa hadithi wazungumze wenyewe bila yeye kuingilia na kutoa ufafanuzi au maoni yake. Kisha njia ya nne ni usimulizi penyezi unaohusu utoaji wa mawazo kuhusu wahusika, matukio na hata ulimwengu wa tungo kwa jumla na msimulizi.

Mlacha (1991) anauona usimulizi kama uhusiano uliopo baina ya msimulizi na hadithi yenyewe. Namna ambavyo msimulizi anaingiliana na hadithi, na nafasi yake katika uwasilishaji wa hadithi ndiyo hutuelekeza kufahamu usimulizi wake. Njia nzuri ya kuelewa hali hii ni kutambua ni nani anayetuwezesha kuipokea hadithi yenyewe; yaani matukio mbalimbali yanawasilishwa kwetu kupitia kwa macho ya nani? Kimsingi, kuna maswali kadhaa ambayo huweka wazi zaidi mbinu iliyotumika katika usimulizi. Ni vizuri kuelewa ni nani anayeisimulia kazi hiyo na ana mtazamo gani? Ana uhusiano gani na matukio ya hadithi husika? Jambo la muhimu katika swali hili ni uelewaji wa uhusika wa msimulizi. Anashiriki katika hayo matukio au la? Ni muhimu vile vile kuchunguza kama mtazamo wake wa matukio hayo ni wa kuaminika. Hayo ni baadhi tu ya masuala muhimu ambayo humsaidia msomaji wa kazi hiyo kuelewa msimulizi wake pamoja na mchango wake katika kuikamilisha.

Njia za usimulizi zimeupa utafiti huu uzito katika uchambuaji wa uhusika katika ushairi wa Kiswahili. Ni kupitianjia hizi ndipo utafiti uliweza kuibua uhusika katika ushairi. Utafiti umetathmini uhusika unavyojitokeza katika ushairi wa Kiswahili kwa kuchunguza mbinu za usimulizi zinazoibua uhusika katika ushairi hivyo basi madhumuni ya kwanza ya utafiti; kutathmini uhusika unavyojitokeza katika ushairi wa Kiswahili kuafikiwa. Uchunguzi wa taswira ya wahusika katika ushairi wa Kiswahili umewezesha madhumuni ya tatu ya utafiti kuafikiwa. Utafiti vilevile umejibu swali kuhusu kujitokeza kwa uhusika na usawiri wa wahusika katika ushairi wa Kiswahili. Utafiti umetoa maelezo kuhusu jinsi watunzi wanavyosawiri wahusika katika ushairi wa Kiswahili.

### 4.2.1 Usimulizi Unavyoibua Wahusika Katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*

Attenberndna Lewis (1963) wanasema usimulizi ni ule mkabala ambao hutuwezesha kuyatimiza yanayotendeka na kusikia yanayozungumzwa katika kazi ya fasihi. Yanayotendwa na yanayozungumzwa huwezeshwa na wahusika.

Hawthorn (1985) anasema usimulizi maizi ni ule ambao mwandishi hueleza hadithi ambayo aghalabu haimhusu yeye. Msimulizi huamua na kueleza yale anayotaka tufahamu na kuacha yale ambayo hataki kutujuza. Msimulizi huingia katika akili ya mhusika hivyo basi anaelewa mawazo ya mhusika.

Utenzi ni ushairi unaosimulia tukio fulani kwa matendo. Usimuliaji wa tukio huambatana na matendo ambayo hufanywa na mhusika. Ama kwa hakika, utendi andishi wa Kiswahili una sifa zake pambanuzi za kifani ambazo huweza kutumika kuzitofautisha na tendi nyingine zisizo

za Kiswahili. Wamitila (2008) anaeleza fani kuwa ni dhana inayotumiwa kuelezea muundo au mpangilio wa kazi fulani ya kifasihi au hata sehemu zake. Anaendelea kufafanua kuwa fani huelezea mbinu na mtindo wa kuyawasilisha yaliyomo au maudhui. Njogu na Chimerah (2008:312) wanasema, fani ni usanifu wa kazi ya fasihi. Wanaendelea kufafanua kwamba, fani ni vipengele mbalimbali vya sanaa na jinsi kazi hiyo inavyojengwa ili kupata maana yake. Hivyo basi katika utendi tunapoangalia fani tunaangalia vipengele mbalimbali vya sanaa ya utendi wa Kiswahili ama mbinu au mtindo anaoutumia msimulizi kuwasilisha mawazo yake kwa hadhira.

Ama kwa hakika *Utenzi wa Fumo Liyongo* unakidhi sifa za kuitwa utendi wa Kiswahili kutokana na kubeba sifa pambanuzi za kifani za utendi wa Kiswahili. Utendi wa Kiswahili una sifa pambanuzi kadha za kifani ambazo kwa hakika zinajitokeza katika *Utendi wa Fumo Liyongo:* Mbali na hizo sifa zingingine za kifani kama vile majigambo, matumizi ya fomula ya ufunguzi na ufungizi, matumizi ya Kiswahili cha kale, matumizi ya beti utendi wa Kiswahili una sifa ya kuchanganya wahusika wanadamu na wasio wanadamu. Msokile (1993:32 ) anaeleza kuwa wahusika ni watu, wanyama au vitu katika kazi ya kisanaa ya kifasihi. Kwa mfano *Utenzi wa Fumo Liyongo* unachanganya wahusika binadamu ambao wanaongozwa na Fumo Liyongo na Sultani na wafuasi wake lakini pia msimulizi amechanganya wahusika wengine wasio binadamu kama vile msitu, miti na jela.

Utendi unaweza kuhusu tukio lolote la kijamii ambalo laweza kuwa la kishujaa au lisiwe la kishujaa.Fumo Liyongo ni shujaa kama alivyoelezwa na Kijumwa (1973). Mwandishi amesimulia habari za shujaa huyu kwa njia ya maandishi katika umbo la kishairi. Anatujuzakuwa vyanzo vinaonesha kuwa Liyongo aliishi Pwani ya Kaskazini mwa Kenya kwenye maeneo ya

Pate na Ozi.Alikuwa shujaa, manju wa ngoma, malenga na mwindaji hodari. Ubeti wa 230 unaeleza kwa muhtasari maisha ya shujaa Fumo Liyongo. Utafiti huu ulishughulikia wahusika wafuatao: Sultani, mamake Liyongo, mama mkwe wa Liyongo, mwanawe Liyongo, Wagalla, Wasanye na Wadahalo kwa pamoja, kijakazi Saada na askari. Utafiti umedhihirisha jinsi mtunzi alivyowaumba wahusika wake kwa kutumia mbinu ya uwasilishaji dhahiri kupitia usimulizi. Hii ni mbinu ambayo mwandishi husimulia kuhusu mhusika hivyo basi msomaji huweza kumwelewa kimaumbile na hata kitabia. Katika utenzi huu, masimulizi yamekuza sifa za wahusika kadha ambazo hazina budi kuzingatiwa.

#### 4.2.1.1 Fumo Liyongo

Kijumwa (1973), kupitia usimulizi maizi, anatupa taswira ya mhusika Liyongo kwa kubainisha sifa, hulka na maumbile yake. Usimulizi maizi humwezesha mwandishi kuieleza hadithi ambayo, mara nyingi, yeye haimhusu; yaani haishiriki lakini, akiwa muumbaji wake, anaelewa kila kitu kinachotendeka hadithini. Maumbile, sifa na matendo ya Liyongo yameelezewa waziwazi kiasi ambacho baada ya hapo tunaongezewa mambo machache sana kumhusu yeye. Mshairi ameweza kumuumba kwa kutumia njia ya ufasiri wa moja kwa moja. Njia hii husaidia kumfanya msomaji asipate tabu kufahamu kiini cha kisa, wazo au dhamira kwa kumtumia mhusika toka mwanzo. Liyongo ni mhusika ambaye amewasilishwa dhahiri kiasi kwamba msomaji anaweza kumwelewa umbo lake, kiini cha kisa na dhamira ya utenzi wenyewe. Katika beti zifuatazo mtunzi anamsimulia Liyongo ifuatavyo:

Mfano 1. Liyongo kitamakali
akabalikhi rijali
akawa mtu wa kweli (ubeti 6)
na haiba kaongeya.

Kimo kawa mrefu
Mpana sana mrefu
Majimbo kawa maarufu (ubeti 7)
Watu huja kwangaliya.

Katika beti hizi mshairi anatudondolea maelezo yanayobainisha wajihi wa Liyongo. Huu ni usimulizi maizi ambapo msimulizi anatusimulia hadithi ambayo haimhusu yeye, wala hana uhusiano wowote na yale anayosimulia. Mtunzi ni chombo tu cha kutufahamisha kuhusu yale yanayomhusu mhusika. Anasimulia yale anayotaka msomaji afahamu kumhusu Liyongo. Sifa za mbinu hii ni uwezo wa mwandishi kutamba na kueleza masuala mbalimbali; katika usimulizi huu mtunzi anaweza kutumia mhusika mmoja, akabadilisha na kutumia mhusika mwingine. Mwandishi ana uhuru kiasi kwamba tunamtarajia kuelewa hata mawazo ya wahusika wake. Kwa hivyo, msimulizi huingia katika akili ya mhusika na akatufafanulia mawazo yake, akatueleza hata kile ambacho mhusika anakikumbuka, na pia msimamo wake kuhusu maswala mbalimbali.

Katika ubeti wa sita mtunzi anasimulia kuhusu utokeaji wa mhusika huyu jinsi alivyokua, akawa ghulamu wa kupendeza na alivyoendelea kuishi. Katika ubeti wa saba mtunzi anasimulia kimo chake. Anasema kuwa alikuwa mtu mrefu tena mpana kumaanisha kuwa lilikuwa jitu. Alipata umaarufu kutokana na kimo chake. Taswira tunayoipata kutoka kwa maelezo haya ni ya jitu lenye nguvu ambalo kimo chake ni cha pekee katika mazingira anamoishi. Ukubwa wake unaambatana na ushujaa mwingi, jambo ambalo linamfanya kuogopewa sana na Sultani wa Pate na watu wote kwa jumla. Kutokana na maelezo ya umbo lake ni dhahiri kwamba sifa za Liyongo si za binadamu wa kawaida ila ni mhusika wa kubuni tu. Huu ni uhusika umbo. Mtunzi anatambulisha uhusika unaorejelewa kwa sababu kinachochukua sehemu ya uhusika hapa ni mtu kwa jina Liyongo. Ni mhusika wa fasihi aliye na sifa zilizopigwa chuku.

Katika ubeti wa 12 msimulizi anamfananisha na simba kuelezea ujasiri wake. Hakuogopa kutembea usiku wa giza au mchana wa jua. Kwake yeye hapakuwa na tofauti. Katika ubeti wa 13 mtunzi anasimulia sifa ya ushujaa aliyokuwa nayo Liyongo. Huu ni uhusika dhahiri kwa sababu mtunzi ameonyesha sifa zinazotambulisha nafsi ya mhusika. Anasimulia mazungumzo ya mfalme kwa Wagalla akiwaeleza kuhusu ushujaa wa Liyongo namna alivyoweza kuwazuia watu mia moja wasiweze kukimbia. Athari ya mhusika Liyongo kwa wahusika wengine inaelezwa. Aidha anaeleza matendo yake na jinsi anavyoonekana.

Ni mwanamume swahihi
kama simba una zihi
usiku na asubuhi (ubeti12)
kutembeya ni mamoya.

Mfalme kawambiya
Wagalla kiwasifiya
huwegema watu miya (ubeti 13)
wasiweze kukimbiya.

Mbali na sifa ya ushujaa Liyongo alikuwa mfumaji stadi kwa kutumia mshale. Alikuwa na hekima kwa kutambua fikra za Wagalla na kufahamu mipango yao ya kumuangamiza. Hivi ni kusema kwamba alikuwa mtambuzi kwa sababu aliweza kutabiri yale yaliyokuwa yamepangwa. Sifa hizi zinadhihirika katika usimulizi uliomo kwenye beti zifuatazo, 63, 65 na 67. Ufumaji unadhihirika wakati zamu yake ya kuukwea mkoma inapofika. Liyongo hakuukwea mti huo ila alitumia mshale kufuma na kuangusha makoma mengi yaliyokuwa yameiva. Kutokana na kitendo hiki kilichokuwa kinyume na matarajio yao Wagalla walitawanyika na kila mtu kushika njia yake. Huu ni uhusika dhahiri kwa kuwa unajitokeza kupitia fikra za ndani za Liyongo na athari yake kwa wahusika wengine.

Uhusika wa Liyongo unabainika kupitia usimulizi maizi kuwa alikuwa na uwezo wa kutenda yale yasiyowezekana. Anakabiliana na genge la Wagalla lililohongwa ili kumwangamiza akiwa juu ya mkoma. Hakuukwea mkoma baada ya kuhisi walikuwa na njama ya kumuua akiwa juu. Uhusika wa Liyongo kama mfumaji stadi unadhihirika kupitia usimulizi katika beti zifuatazo:

Liyongo akiuona
ni mrefu mno sana
yakamwelea maana (ubeti 63)
yake alowadhania.

Akawambia ngojani
akatowa mkobani
chembe katia ngweni (ubeti 65)
makoma kiwanguliya.

Wakanena kwa moyoni
amuwezao ni nani
huyu hawezekani (ubeti 67)
ni kutaka kwangamiya.

Mtunzi anasimulia ushujaawa Liyongo, jagina aliyesifika sana na hata kuwaogofya watu kutoka janibu zilizopakana na Pate. Kwa kuzingatia utenzi huu uhusika dhahiri wa Liyongo unaonekana kupitia usimulizi maizi. Tunaonyeshwa mambo yanayotambulisha nafsi ya mhusika kupitia unenaji wa Sultani kumhusu Liyongo, fikra na hisia za ndani za Liyongo na athari yake kwa wahusika wengine.

Mtunzi amemsawiri Liyongo kama mhusika mwenye matumaini. Sifa hii inabainika baada ya Liyongo kukamatwa na kutiwa gerezani na utawala wa sultani. Hapakuwa na budi kwamba atauawa hivyo basi kitwana akatumwa kumuuliza kile ambacho angetaka kutendewa kabla ya kuipa dunia buriani. Hili halikumkatisha tamaa wala kumvunja moyo. Anaomba wamwandalie tamasha ya kucheza ngoma iitwayo mwao pamoja na gungu nje ya jela alimokuwa amezuiliwa.

Ni katika tamasha hii ndipo umahiri wake katika uimbaji unadhihirika. Huu si uimbaji wa kawaida kwa sababu mbali na kuimba kuna gungu. Huu ni utunzi wa shairi lililo na mizani mingi. Anatunga shairi huku akicheza mwao kiasi cha kuwaacha watazamaji wamepigwa na butwaa. Ngoma inapochezwa anatumia fursa hii kwa ujasiri kukata minyororo iliyotumiwa kumfunga. Anajitokeza ngomani kwa mshangao na furaha kwa wote waliokuwa wakicheza ngoma. Wakati ngoma ikiendelea alishughulika kukata minyororo kwa kuikereza kwa tupa. Baadaye jioni hiyo anatoroka na kukimbilia upande wa bara unaopakana na bahari si mbali sana na Wagalla ambako aliweka makao yake. Mtunzi ametumia uhusika usio dhahiri kwa sababu tabia isio ya kimazungumzo inadhihirika. Hekima na busara ya kutaka kutoroka kwa kutumia ujanja inaonekana anapoomba kuandaliwa ngoma. Usimulizi huu umo katika beti zifuatazo:

Wakamtuma kitwana
Kwa Liyongo akanena
Kufa shaka hapana (ubeti 95)
Menituma kukwambiya

Watamani jambo gani
Menituma sulutani
Utapewa kwa yakini (ubeti 96)
Ili uage duniya.

Akajibu usikhini
kamwambie Sultwani
mwao nimetamani (ubeti 98)
na gungu liwe pamoya.

Ushujaa wa Liyongo unadhihirika kupitia usimulizi kuhusu kifo chake. Kijumwa (1973), amemwasilisha Liyongo kama mzazi asiyekuwa na shauku kwa mwanawe anapomfichulia siri kuhusu nguvu zake. Mwanawe anamwangamiza baada ya kutambua siri. Liyongo alimwandama muuaji hadi katikati mwa mji ambapo palikuwa na kisima alipoanguka. Pale kisimani alipiga goti na kutia mshale kwenye uta kama alivyokuwa akifanya akiwa hai. Watu wa pale mjini

waliogopa kuteka maji kwa siku tatu kisimani walipomwona Liyongo pale. Waliogopa wakidhani alikuwa hai na angeweza kuwafuma kwa mshale. Hali hii inapelekea wenyeji kumrai mamake aende azungumze naye ili awaruhusu kuteka maji. Ni mamake tu ndiye aliyetambua kuwa Liyongo alikuwa ameaga dunia baada ya kuzungumza naye na asiweze kumjibu.Usimulizi huu unapatikana katika beti zifuatazo :

Kamtia kitovuni
naye ulele kwa tani
achamka hamuoni (ubeti wa 152)
kijana amekimbiya.

Babake akishutuka
chembe uta akishika
kwa haraka akatoka (ubeti wa 153)
nde muyi kaendeya.

Akapija ondo lake
kapatika chembe chake
kama hai ada yake (ubeti wa 154)
chembe utani katiya.

Na hapo nami tasema
ni karibu na kisima
watu hawakusimama (ubeti wa 155)
kwa wote walikimbiya.

Kupitia usimulizi maizi uhusika dhahiri unaibua kinyang'anyiro cha madaraka, ushujaa, usaliti na kufanyiana njama. Hivyo basi kubainisha wahusika ambao sifa zao ni dhahiri na zinaweza kuelezwa baada ya kusoma shairi.

Uhusika wa Liyongo unadhihirika kupitia matendo ya kishujaa aliyoonyesha. Liyongo ameshehenezewa sifa tele. Ni mtu mwenye nguvu nyingi ajabu, vilevile ana uwezo wa kufuma barabara na kuangusha makoma mengi yanayowatosheleza wote. Hii ndiyo sababu watu wote

waliompenda na wale waliomchukia walisikitika alipokufa kama inavyoelezwa katika ubeti ufuataao:

Mui walisikitika
hakuna wa kutosheka
kwa Liyongo kutoweka (ubeti 226)
imeanguka paziya.

#### 4.2.1.2 Sultani

Usimulizi unatupa taswira ya mtu dhalimu asiyekubali upinzani kutoka kwa yeyote yule. Anatumia kila mbinu na hila kumuangamiza yeyote anayethubutu kupinga utawala wake. Aidha ni haini kwa kuisaliti dola yake anapomsaka Liyongo ili kumwangamiza. Anapopanga njama ya kumwangamiza Liyongo ambaye ni binamu yake kwa ajili ya madaraka ni dhahiri kuwa ni mtu hatari. Mtunzi anasimulia woga wa Sultani katika ubeti wa saba, tisa na kumi. Ni bayana kuwa Sultani alichelea kuwa Liyongo angeweza kupindua utawala wake na kuchukua hatamu za uongozi. Taswira ya Liyongo kupitia usimulizi wa mfalme ni mtu wa kutisha kiasi cha kumfanya mtu asiweze kwenda haja ndogo hata kama alikuwa na nia. Anaweza kusababisha mtu kuzimia na hata kufa kwa kumkodolea macho. Huu ni mtazamo wa mfalme ambao ni ithibati kuwa aliogopa mno uwepo wa Liyongo katika hiyo dola aliyokuwa akitawala.

Mfano 2. Mfalume kawambiya
Wagalla kiwasifiya
Humwegema watu miya (ubeti wa 7)
Hawawezi hukimbiya.

Ghafula kikutokeya
Mkojo hukupoteya
Tapo likakuiliya (ubeti wa 9)
Ukatapa na kuliya.

Mato kikudoleya
ghafula utazimiya
Kufa kutakurubiya (ubeti wa 10)
Kwa khaufu kukungiya.

Uhusika wa Sultani ni wa hila kwa sababu haja yake ni kumpata Liyongo ili amwangamize. Sultani aliwatumia Wagalla kumshawishi Liyongo kurejea Pate kwa kisingizio kuwa milki ya Wagalla haikuwa salama. Liyongo aliingia mtegoni na kukubali kurejea Pate hali inayomfanya kukamatwa na kutiwa gerezani. Sultani amesawiriwa kama mhusika mjanja aliyefaulu kupata windo lake. Kwa kuwa amefurahi kupata windo lake lisiloweza kujinasua kama afanyavyo panya baada ya kushikwa na paka anamtaka Liyongo aeleze kile ambacho angependa atendewe kabla ya kuuawa. Sultani anatuma ujumbe kupitia kwa kitwana kwenye masimulizi yaliyomo katika ubeti wa 95 na 96.

Wakamtuma kitwana
kwa Liyongo akanena
la kufa shaka hapana (ubeti 95)
menituma kukwambia.

Watamani yambo gani
menituma sultwani
utapewa yakini (ubeti 96)
ili uwage duniya.

Ukatili wa Sultani unabainika kupitia masimulizi ya wakuu wa mji alikoishi Liyongo. Huu ni usimulizi maizi kwa kuwa mwandishi anatumia mhusika mwingine kueleza yale yaliyo kwenye fikira zake. Wanaeleza kuhusu ghadhabu ya Sultani iwapo wangefichua siri kuhusu mpangowa kumnasa Liyongo. Taswira tuipatayo hapa ni ya mtu asiyekuwa na huruma hata kwa wazalendo na wale aliowatunuku madaraka iwapo watatenda kinyume na matarajio yake. Kwake yeye kuua si kazi ngumu tena hajali ila alitenda kama alivyoazimia. Usimulizi katika ubeti wa 83 unadhihirisha sifa hii. Katika masimulizi yafuatayo mtunzi anasema:

Sultani kabaini
mashaha walo muyini
kawambia kwa sirini (ubeti wa 80)
pija gungo huwambia.

Kwa wanaume na wake
Liyongo mumwalike
naazimu nimshike (ubeti wa 81)
ni siri nimewambiya.

Na habari kisikiya
Liyongo akikimbiya
nani mezomwambiya (ubeti wa 82)
tawaua kwa umoya.

Naye huyu sultani
kuua hawezekani
akinena kwa yakini (ubeti wa 83)
hutimiza mara moya.

Usimulizi maizi umetumiwa kutambulisha hulka ya Sultani kama ulivyotumiwa kumtambulisha Liyongo. Ametumia mbinu ya uwasilishaji dhahiri hivyo basi inakuwa rahisi msomaji kumwelewa mhusika huyu na kubaini kuwa ni mfalme wa Pate anayepanga njama ya kumwangamiza Liyongo. Ana hofu ya kunyang'anywa madaraka baada ya kuona jinsi Liyongo anavyopendwa na watu wengi. Sultani anatumia hila ambapo Liyongo anasalitiwa namwanawe. Mtunzi amewasawiri wahusika wawiliwanaohasimiana kwaajili ya madaraka. Kwa jumla uhusika dhahiri na uhusika usio dhahiri umedhihirika katika utenzi huu. Mtunzi ametoa maelezo kupitia usimulizi wake mwenyewe na usimulizi wa wahusika wengine.

### 4.2.1.3 Mamake Liyongo

Hulka ya mamake Liyongo inatambulishwa kupitia usimulizi maizi. Ni mama mwenye huruma anayempenda mwanawe. Ana mapenzi ya dhati kwa mwanawe aliyefungwa gerezani hivyo basi,mara kwa mara aliandaa chakula ili apelekewe. Mtunzi anaeleza huzuni na masikitiko Aliyokuwa nayo mama mtu alipong'amuakuwa chakula alichokuwa akiandaa hakikumfikia mwanawe ila kililiwa na askari wa gereza.

Mfano 2. Na tume wa sultani
akitoka kijumbani
kaja tume wa nyumbani (ubeti wa 99)
chakula akamweteya.

Na mamake kwa hakika
kuti kizuru kipeka
asikari humpoka (ubeti wa 100)
chakula wakailiya

Chakula wakimweteya
asikari huikiya
siku hiyo kamwambiya (ubeti wa 101)
mama unisalimiya

Liyongo anapogundua tabia ya askari ya kumpokonya mtumishi chakula chake, anawaza namna anavyoweza kuwakabili. Anamweleza mtumishi kimafumbo na kishairi ili askari wasielewe anachosema. Anatuma ujumbe kwa mamaye ampikie mkate wa wishwa na katikatiatie tupa. Alitaka mamaye afanye hivi makusudi kwa sababu mkate wa wishwa haukuwa na thamani hivyo basi mtumishi asingepokonywa na askarikama walivyokuwa wamezoea. Mkate wa aina hii uliliwa na watu wa hadhi ya chini. Mama anafanya kama alivyoelekezwa. Liyongo anapoletewa huo mkate anaipata hiyo tupa ambayo anaitumia kukereza minyororo iliyotumiwa kumfunga na kutoroka gerezani. Mamake hakutaka kumvunja mwanawe wala kuuliza sababu ya kuomba apelekewe tupa. Alitii na kutenda jinsi mwanawe alivyotaka. Tunapata taswira ya mama anayejali maslahi ya mwanawe. Kupitia usimulizi tunaona mapenzi ya dhati kati ya mzazi na mwana. Mamake Liyongo alimthamini mwanawe na kumtimizia yote aliyohitaji kama mwanawe. Haya yanadhihirika katika beti zifuatazo:

Mama tupa akatiya
kitambaa metatiya
kwa furaha mno ghaya (ubeti 110)
sana kawafurahiya.

Kanena kwa ushairi
enenda kamuhubiri
mama afanye tayari (ubeti 222)
haya nimezokwambiya.

Kulla nyimbo zizidipo
na ngoma zitakatapo
alikizitinda hapo (ubeti 223)
pingu na minyoo piya.

Taswira ya mama mwenye huzuni inabainika kufuatia kifo cha mwanawe kupitia usimulizi kwenye ubeti ufuatao.

Sana wakahuzunika
Na matanga wakaweka
Kisa mamake katoka (ubeti 227)
kana ada kutembeya.

Taswira ya wenyeji waliojaa wasiwasi wasijue la kufanya inadhihirika kupitia usimulizi, Liyongo anapokufa pale kisimani. Wamesawiriwa kama watu walioamini kuwa Liyongo hangeweza kufa.

Nao hayakueleya
Liyongo ameifiya
kwa khaufu kuwangiya (ubeti228)
hawakumkurubiya.

Watu hawa hawakuwa na uhakika iwapo Liyongo alikuwa amekufa au alikuwa hai kutokana na jinsi walivyomuona pale kisimani. Walidhani angeweza kuwashambulia. Walishindwa kumshawishi aondoke pale ili waweze kuteka maji. Ilibidi wamsihi mamaye kuzungumza naye. Mama anamrai kwa nyimbo ndipo anagundua kuwa si hai ni mfu. Mama akiwa na huzuni anaandaa matanga ya mwanawe na kumzika. Masimulizi haya yanapatikana katika beti zifuatazo:

Shauri likawa moya
kheri mama kumwendeya
mamake kisikiliya (ubeti 189)
atamsikitikiya.

Make Liyongo hakika
matanga aliyaweka
watu wakasikitika (ubeti 224)
kwa Liyongo kuifiya.

Hivyo basi katika utenzi huu mtunzi kupitia usimulizi anatupa taswira ya mamaye Liyongo kuwa alimwelewa mwanawe. Anapofia pale kisimani wenyeji wanashindwa kuteka maji wakiamini kuwa angali hai na anaweza kuwadhuru. Wanamtuma mamaye kwenda kumrai aondoke pale ili waweze kuteka maji. Hali hii inadhihirisha imani waliokuwa nayo kwa mamaye, kwamba ndiye pekee aliyeweza kumshawishi mwanawe. Aidha inajitokeza wazi hapa kuwa Liyongo alimtii na kumheshimu mamake japo mamake alimuogopa pia. Usimulizi huu unaibua uhusika dhahiri kwa kuwa ni kupitia usimulizi tunapata kujua tabia na mienendo ya watu waliowasilishwa.

### 4.1.2.4 Mama Mkwe wa Liyongo

Taswira ya bibi Mgalla mwenye kisasi kwa mjukuuwe inabainika kupitia usimulizi. Kutokana na dhuluma ya mjukuu wake dhidi ya Liyongo mama alikataa kumkimu baada ya kukimbilia kwake. Alimuacha taabanihivi kwamba anaaga dunia kwa kukosa mahitaji ya kimsingi kama vile chakula. Haya yanaelezwa katika beti zifuatazo:

Mfano 3. Yule mwana nikwambie
hakwenenda kwa bibiye
kwa mama Liyongo yeye (ubeti 218)
Galani alikimbiliya.

Mtunzi anasimulia alikokimbilia mwanawe Liyongo ili kujisitiri baada ya kutekeleza mauaji. Anaeleza kuwa alikwenda kwa nyanya yake wa kuukeni. Alitarajia kupata makaribisho kutoka kwa bibiye huyo lakini haikuwa hivyo.

Watu akitahayari
kwa ile yakwe amri
watu wakimtiriri (ubeti 219)
mayuto yakamngiya.

Kijana huyu aliona haya na kuogopa kuingiliana na watu kutokana na kitendo chake. Hali hii ilimfanya kujuta kwa sababu watu walimuona kuwa mtu mbaya hivyo basi kumuambaa.

ule mamake kijana
hakumpenda tena
kimwamba na kunong'ona (ubeti 221)
mno akamtundukia.

Kawa tena hampendi
kwa chakula hamtundi
kakamzidi mayondi (ubeti 222)
huzuni zikamngiya.

Mtunzi anasimulia jinsi mwana huyo msaliti alivyokosa mapenzi ya mama, akawa hapewi chakula. Hali hii ilimfanya kuzidiwa na majonzi na huzuni. Mtunzi ametumia uwasilishaji dhahiri kuibua taswira ya bibi asiye na mapenzi kwa mjukuuwe. Kupitia usimulizi maizi msomaji anabaini uhusika wa bibi kutokana na maelezo ya mtunzi yanayodhihirisha sifa zake. Hakumsamehe mjukuu wake.

### 4.2.1.5 Mwanawe Liyongo

Kupitia usimulizi maizi taswira ya mwanawe Liyongo inabainisha mtu mwenye tamaa ya uluwa. Mhusika ambaye yuko tayari kutenda uovu wa kumwangamiza baba mzazi kwa ajili ya mali ya ulimwengu huu. Baada ya kutekeleza hicho kitendo kiovu Sultani anamcheka kwa kejeli, hapati

chochote na anakufa kwa masikitiko makubwa. Katika beti zifuatazo, mtunzi anasimulia kisa hiki kupitia usimulizi maizi, anaeleza jinsi Sultani alivyomshawishi mwanawe Liyongo kumwangamiza babake na maisha ya mwana huyo ya baadaye. Haya yanadhihirika mtunzi anaposimulia hivi katika beti zifuatazo:

Mfano 4. Akanena mueteni
mwane Liyongo yani
aye hapa hadharani (ubeti 208)
nina neno t'amwambia.

Amekufa baba wako
akaangua kiteko
kwakwe kamwe sikitiko (ubeti 210)
kabisa halikungiya.

Katika masimulizi yanayohusu mashujaa, nguli au majagina aghalabu husalitiwa na watu wa aila yao. Utenzi huu si tofauti hivyo basi sifa hii ya usaliti wa mwanawe inadhihirika Liyongo anapomfichulia mwanawe siri ya nguvu zake. Hakujua kwamba angeweza kuitumia siri hii kumwangamiza. Katika ubeti wa 152 anasimulia hivi:

Kamtiya kitovuni
Naye ulele kwa t'ani
Achamka hamuoni (ubeti wa 179)
Kiyana amekimbiya.

Kupitia usimulizi, taswira ya kijana inadhihirisha sifa yaujinga. Ujinga wake unadhihirika pale anapokubali kutekeleza mauaji ya babake mzazi. Ni mjinga kwa sababu hata baada ya kutekeleza uovu huo hakutimiziwa ahadi alizopewa. Sifa yake nyingine ni kushawishika haraka bila kufikiria madhara ya matendo yake. Anapotekeleza mauaji dhidi ya baba mzazi kwa kuahidiwa kuozwa binti ya sultani na kuteuliwa waziri ni ithibati ya ukatili uliopituka. Anashawishika upesi na bila huruma anamdunga Liyongo kwa sindano ya shaba kitovuni. Hana hekima wala busara anapokubali kutenda maovu kwa ahadi ambazo hana uhakika kama zitaweza kutimizwa au la.

Mbinu anayotumia Sultani hapa ni ya Ki-Machiavelli kwani baada ya mwanawe Liyongo kutekeleza mauaji, Sultani anamfukuza bila ya kutimiza ahadi alizokuwa amempa. Hivyo basi anakuwa funzo kwa wengine katika jamii. Usimulizi huu unadhihirika katika beti zifuatazo:

Mfano 5. Au wewe wakiyuwa
nambiya sifanye tuwa
uwaziri utapewa (ubeti 127)
takuoza bintiya.

Baada ya kutekeleza uhayawani huu taswira ya kijana kwa msomaji ni ya mtu anayejutia kitendo chake. Hakuna anayemkaribia hivi kwamba ametengwa na wenzake. Ni kutokana na hali hii ya upweke ndipo anaamua kukimbilia kwa mamake mzazi. Aliishi kwa kujificha kwani aliona haya hali ilyomfanya kutotoka nje na kusalia ndani ya nyumba. Aliugua maradhi yasiojulikana na hatimaye kuaga dunia. Haya masimulizi ya kusikitisha yanadhihirika katika beti zifuatazo:

Kaingiya mayutoni
katindikia nyumbani
hata wenzi hawaoni (ubeti 220)
hamu imezomngiya.

Siku chache katimiya
maradhi yakamngiya
yasiyo muondokeya(ubeti 223)
naye kisa kaifiya.

Mtunzi ametumia uwasilishaji dhahiri kwa kusimulia yaliyompata mhusika. Uwasilishaji huu unaibua uhusika dhahiri. Uhusika unajitokeza kutokana na namna nafsi ya mhusika inavyotambulishwa. Nafsi ya mwana huyu inatambulika kutokana na athari yake kwa wahusika wengine. Kutokana na kitendo chake cha kutekeleza mauaji dhidi ya babake mzazi watu wote walimchukia. Kitendo cha wenzake kumuambaa kinamfanya mwana huyu kujihisi mpweke kisha kuugua maradhi yasiyojulikana na hatimaye kuaga dunia.

#### 4.2.1.6 Wagalla, Wasanye na Wadahalo

Uhusika wa Wagalla, Wasanye na Wadahalo kupitia usimulizi unatupa taswira ya watu ambao ni wakatili. Watu hawa wanahongwa ili kutekeleza mauaji dhidi ya watu wengine mradi wamepewa pesa. Kwa hivyo, Kijumwa (1973), amewachora kama watu wasiokuwa na hekima na wasiowajibika. Haya yanadhihirika katika beti zifuatazo:

Mfano 6. Mfalume changaliya
mwituni mekimbilia
Wasanye kawazengeya (ubeti 52)
na Wadahalo pamoya.

Mfalume kawambiya
Liyongo kunipatiya
Kitwa mukanieteya (ubeti 53)
T'awapa riale miya.

Taswira ya watu wanafiki inabainika kupitia usimulizi. Liyongo alipowasili katika milki ya Wagalla alikaribishwa kwa taadhima kuu na hata kutawazwa kuwa kiongozi wa Wagalla. Ni katika kipindi hiki ambapo kulikuwa na ukame mbaya. Wanaume waliunda kikoa ili kula kwa pamoja na kutafuta chakula cha kuwalisha wenyeji kwa zamu. Wakati huu wa uhaba wa chakula wenyeji walitumia makoma. Matunda haya yalikuwa juu sana na ilibidi wanaume kuikwea mikoma ili kuyatunda. Wagalla walipanga njama kuwa zamu ya Liyongo kukwea ifikapo wamfume kwa mishale akiwa juu kwa sababu hataweza kujikinga. Huu ni uhusika usio dhahiri. Ni kupitia tabia yao isiyokuwa ya mazungumzo ndipo uhusika unadhihirika. Hakuna maelezo ya watu hawa mahali popote kuhusu tabia yao ila ni kutokana na mpango wao wa kutaka kumwangamiza Liyongo ndipo sifa yao inadhihirika.

Usimulizi maizi unatambulisha uhusika wa Sultani kuwa alikuwa mfalme wa Pate. Aidha alikuwa wa nasaba moja na Liyongo. Kule kupata madaraka kwa Sultani huyu kunamfanya

Liyongo kuhisi kwamba amehiniwa haki yake. Sultani naye anaishi kwa hofu akichelea kupokonywa utawala na Liyongo hasa kwa vile Liyongo ni jitu lenye nguvu sana na linapendwa na watu wengi.

Ugomvi huu kati ya Liyongo na Sultani ulitiliwa nguvu nauchoyo na wivu wa Sultani. Hili linatokana na hali kwamba Liyongo aliweza kupata wafuasi sehemu za bara kutokana na umaarufu wake. Uhusika dhahiri na uhusika usio dhahiri umedhihrika hivi kwamba sifa na tabia ya Sultani inabainika. Uhusika dhahiri unadhihirika kupitia unenaji wa wahusika wengine kama vile Wagalla wanapozungumza kuhusu Liyongo. Uhusika usio dhahiri unaonekana kupitia njia mbalimbali anazotumia Sultani kumsaka Liyongo ili kumwangamiza. Baada ya kuona matumizi ya nguvu na makabiliano ya moja kwa moja na Liyongo hayamfikishi popote Sultani anatumia hila ambapo mwanawe Liyongo anamsaliti kwa sultani.

### 4.2.1.7 Kijakazi Saada

Jina Saada kwa Kiarabu linamaanisha furaha hivyo basi hili ni jina la kimajazi ambalo linadhihirisha sifa ya uchangamfu ya mhusika Saada. Huu ni uhusika usio dhahiri kwa sababu ni kupitia jina lake ndipo sifa inabainika. Saada amesawiriwa na mshairi kupitia usimulizi maizi kama mtumishi mwongofu na asiyekuwa na woga. Anadhihirisha ujasiri anapopewa mkate uliotiwa tupa katikati kumpelekea Liyongo kupitia askari wa gereza bila woga. Kijakazi Saada haogopi kuwa anaweza kugunduliwa na wale askari wa gereza na kukamatwa kisha kutiwa ndani. Mtunzi amemwasilisha mhusika huyu kama kielelezo cha mtu mtiifu katika jamii. Anatii anapotumwa bila kuonyesha kiburi. Japo ni hatari kijakazi anatekeleza wajibu kama mtumishi. Huu ni uhusika dhahiri kwa sababu amewasilishwa kupitia matendo yake ya utiifu. Mtunzi

anasimulia ujumbe na maagizo aliyopewa na Liyongo ili kumfikishia mamake. Katika ubeti wa 100 na 107 mtunzi anasimulia hivi:

Mfano 7. Na tumi wa Sultwani
akitoka kijumbani
kaya tumi wa nyumbani (ubeti 100)
chakula akimweteya.

Mkate huu sikiya
Pishi mbili hutumiya
Kati tupa katiya (ubeti 107)
Liyongo kampekeya.

Usimulizi uliyomo kwenye beti hizi unafafanua hali ilivyokuwa kabla mtumishi hajapewa chakula kumpelekea Liyongo. Mtunzi anatupa taswira ya mambo kabla ya Saada kufika pale kwenye gereza. Huu ni uwasilishaji dhahiri kwa kuwa mtunzi anaeleza waziwazi namna walivyopishana watumishi hawa wawili hivyo basi kuibua uhusika wao.

### 4.2.1.8 Askari

Hulka ya askari inayodhihirika bayana ni ulafi. Kupitia usimulizi maizi Kijumwa (1973), amewasawiri askari kama watu wenye uroho. Wafungwa walipoletewa chakula kupitia kwa askari walikila badala ya kuwapa. Ni kutokana na uroho wa wafungwa, Liyongo akaweza kutoroka kwa kukata minyororo akitumia tupa iliyowekwa kwenye mkate wa wishwa. Alifahamu kuwa mkate wa wishwa ni chakula ambacho hakina thamani na askari hawatakihitaji ila watakiwasilisha kwa mfungwa atakapoletewa. Chakula kilipoletwa walikiwasilisha bila kutambua kilichokuwa ndani. Liyongo alitumia hiyo tupa kukereza minyororo nakisha kutoroka.

Mfano 8. Na mamake kwa hakika
chakula chema kipika
asikari humpoka (ubeti 101)
chakula wakailiya.

Askari hawakuwa makini katika kazi hivyo basi hawakushughulika kufanya kazi ipasavyo. Mtunzi anatupa taswira ya watu wazembe. Hii inabainika tupa inapoingizwa gerezani ikiwa kwenye mkate wa wishwa. Kupitia usimulizi maizi mtunzi ameweza kuibua uhusika dhahiri unaopelekea kutambua hulka na mwenendo wa askari. Kama ilivyo katika masimulizi ya ngano msimulizi anaelewa kila kitu na hasa tabia zote za wahusika. Msimulizi ana uhuru mwingi sana. Anajua kila kitu na ana nafasi ya kuamua yale atakayotuambia na yale atakayoyaacha. Katika usimulizi huu, mwandishi ana uhuru kiasi kwamba tunamtarajia kuelewa hata mawazo ya wahusika wake. Kwa hivyo, msimulizi huingia katika akili ya mhusika na kufafanua mawazo yake, hueleza hata kile ambacho mhusika anakikumbuka, na pia msimamo wake kuhusu maswala mbalimbali. Hivyo basi mtunzi amewasawiri askari kwa kudhihirisha tabia hiyo ya ulafi na kuingia kwenye akili ya Liyongo kufunua yale aliyokuwa akipanga kutekeleza akilini mwake.

#### 4.2.1.9 Usimulizi Unavyoibua Uhusika wa nafsi katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*

Uhusika huu unaibuliwa katika mfumo wa uzungumzi nafsi wa ndani ama kwa kupitia taarifa halisi kupitia usimulizi wa nafsi ya kwanza. Gill (1985), anasema usimulizi huwa wa aina tatu. Ameainisha ifuatavyo; usimulizi wa nafsi ya kwanza, usimulizi wa nafsi ya pili na usimulizi wa nafsi ya tatu. Anasema matukio yote huelezwa kwa undani na huelezea fikra, hisia na imani ya msimulizi. Usimulizi wa nafsi ya tatu huwa wa aina mbili, msimulizi tambuzi na msimulizi dokezi. Msimulizi tambuzi hueleza matukio yote kwa undani na kwa uhakika. Aidha msimulizi huyu huingia katika nafsi ya mhusika yeyote wakati wowote ili kueleza fikra, hisia na imani

zake. Kutokana na hali hii usimulizi huu unaweza kutujulisha mengi na pia kuficha habari nyingi.

Msimulizi dokezi husimulia visa na matukio kupitia mhusika mmoja au mara nyingi wahusika kadha lakini si wote. Msomaji hudokezewa fikra na hisia za mhusika mmoja na huelewa visa na hadithi jinsi msimulizi anavyoelewa. Msimulizi huyu mara nyingi huwa ni mchunguzi au mtazamaji au mhusika katika tukio.

Usimulizi huhusiana na mhusika mwenyewe ambaye hubeba uhalisi wa kimaisha. Maneno huteuliwa baada ya uchunguzi, kulingana na uzito wa uwasilishi wa ujumbe unaotaka kuwasilishwa. Maneno hayo kwa ujumla wake huzaa lugha maalum ambayo inalandana na wahusika na miondoko yao.

Katika ubeti wa 53 uhusika wa nafsi uwili unabainika kwa kuwa kuna mazungumzo baina ya wahusika wawili. Sultani anatoa ahadi kwa Wagalla kwamba iwapo watamuua Liyongo na kumpelekea kichwa chake atawapa riale miya.

Mfano 1. Mfalume kawambiya
Liyongo kunipatiya
Kitwa mukanieteya (ubeti 53)
T’awapa riale miya.

Uzungumzi wa nafsi uwili unaibuka katika ubeti wa 65. Wagalla walipomtaka Liyongo kuukwea mkoma. Mtunzi anasimulia jinsi alivyowaambia na kile alichofanya.

Mfano 2. Akawambia ngojani
akatowa mkobani
chembe katia ngweni (ubeti 65)
makoma kiwanguliya.

Katika ubeti wa 67 mtunzi anaibua uhusika wa nafsi wingi. Katika uhusika huu mshairi huzungumza kwa niaba ya kundi fulani la watu ambalo yeye ni mmoja wao. Katika usimulizi huu mtunzi anasimulia yaliyonenwa na wahusika hao moyoni. Hivi ni kusema kwamba japo anasimulia matukio akiwa miongoni mwao aliweza kufahamu yaliyokuwa mioyoni mwao. Huu ni usimulizi maizi kwa sababu ameweza kuingia katika nafsi zao na kusimulia fikra zao.

Mfano 1. Wakanena kwa moyoni
amuwezao ni nani
huyu hawezekani (ubeti 67)
ni kutaka kwangamiya.

Kwa wanaume na wake
Liyongo mumwalike
naazimu nimshike (ubeti 81)
ni siri nimewambiya.

Katika ubeti huu mtunzi ameibua uhusika wa nafsi uwili. Nafsi ya kwanza ni Sultani anayezungumza na nafsi ya pili ambayo nimwanawe Liyongo. Sultani anamshawishi mwanawe Liyongo kumfahamishazilipo nguvu za babake. Anamuahidi uwaziri na hata kumuoza bintiye iwapo atakubali matakwa yake. Haya yanadhihirika mtunzi anapotumia kiwakilishi 'wewe' katika mshororo wa kwanza. Mbinu za uhusika zimeweza kutokana na mkusanyiko wa kanuni za maonyesho au tamthilia. Ujumbe unaotumika kusawiri mhusika umewasilishwa na mmoja wa viumbe na umeshirikishwa na nafsi ya mwandishi aliyedokezwa kama mhusika moja kwa moja.

Mfano 1. Au wewe wakiyuwa
nambiye sifanye tuwa
uwaziri utapewa (ubeti 83)
takuoza bintiya.

Uhusika wa nafsi uwili unaibuka katika ubeti 96. Kuna mazungumzo kati ya mtumishi wa Sultani na mwanawe Liyongo. Mtumishi alikuwa ametumwa kumrai mwanawe Liyongo kumweleza kile ambacho kingeweza kumwangamiza Liyongo.

Mfano 2. Watamani yambo gani
menituma Sultwani
utapewa yakini (ubeti 96)
ili uwage duniya.

Katika utenzi huu uhusika wa nafsi umejitokeza kwa uchache kama utafiti unavyodhihirisha. Mtunzi ndiye msimulizi anaposimulia hadithi kumhusu Liyongo. Huu ni usimulizi maizi kutokana na ufahamu wake wa mhusika huyu. Mtunzi anarejelea yaliyonenwa na wahusika kumhusu Liyongo katika sehemu chache tu katika hadithi.

### 4.2.10 Usimulizi Unavyoibua Vihusika Katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*

Kijumwa (1973), kupitia usimulizi ametumia vihusika mbalimbali katika utenzi kuwasilisha ujumbe wake. Kwanza kuna kihusika gereza ambamo Liyongo alifungwa. Gereza hili lina ulinzi mkali unaotokana na askari. Askari wanashika doria kwa zamu ili wafungwa wasiweze kutoroka. Huu ni uhusika dhahiri kwa sababu mtunzi anatoa maelezo waziwazi kuhusu kihusika kupitia unenaji. Kihusika hiki kimetumiwa kumtia adabu mtu au watu ambao wanaonekana kuwa kikwazo kwa utawala uliyoko. Masimulizi haya yako kwenye ubeti wa 76.

Mfano 1. Akatiwa gerezani
Kafungiwa kijumbani
Askari mlangoni (ubeti 76)
Kwa zamu wachangaliya.

Mtunzi anasimulia kimo cha miti anaposema ni mirefu sana. Matunda ya miti hiini makoma ambayo ni chakula muhimu cha binadamu wakati wa njaa. Huu ni uhusika dhahiri hivi kwamba maelezo yametolewa kupitia unenaji kuhusu vihusika hivi. Ijapokuwa miti hii ni mirefu mno, Fumo Liyongo anadhihirisha ushujaa wa kufuma matunda kwa mshale. Kupitia usimulizi huu ni dhahiri mhusika ana uwezo usioweza kuelezeka. Huu ni uhusika usio dhahiri kwa sababu ni

kupitia kwa matendo yake ndipo sifa zinazobainisha uwezo wake wa kufuma unaonekana. Hii ni mbinu ya uandishi ya kuifanya hadithi iwe na mvuto. Maelezo haya yanapatikana katika ubeti wa 63:

Mfano 2. Liyongo akiuona
ni mrefu mno sana
yakamwelea maana (ubeti 63)
yake alowadhania.

Kupitia usimulizi maizi mtunzi anaumba msitu. Hiki ni kihusika ambacho madhumuni ya mtunzi kukiibua ni kumsitiri Liyongo anapokuwa hatarini akisakwa ili kuangamizwa. Msitu ni eneo lililo na miti mingi na si rahisi kuona kilicho ndani yake. Msitu ni kihusika kisichokuwa dhahiri. Hakuna maelezo yanayohitajika kueleza sifa za msitu ndipo uweze kumsitiri Liyongo. Liyongo anapokimbilia huku ni dhahiri kwamba ameenda mafichoni asikoweza kuonekana kwa urahisi. Usimulizi huu unapatikana katika ubeti wa 52.

Mfano 3. Mfalume changaliya
mwituni mekimbilia
Wasanye kawazengeya (ubeti 52)
na Wadahalo pamoya.

Taswira ya mahali alipokimbilia Liyongo kujinusuru kutokana na hatari iliyokuwa imemkabili inabainika kpitia usimulizi.

Mtunzi ametumia uwasilishaji dhahiri kusimulia kifaa tupa. Ameeleza waziwazi kuwa baada ya mkate kupikwa tupa ilitiwa katikati. Tupa ni kihusika muhimu sana kwa kuwa ndicho alichotumia Liyongo kujinasua kutoka kifungoni. Mtunzi anaibua uhusika kwa kuhusisha tupa kupitia usimulizi maizi. Maelezo haya yamo kwenye ubeti wa 107 ufuatao.

Mfano 4. Mkate huu sikiya
Pishi mbili hutumiya
Kati tupa katiya (ubeti 107)
Liyongo kampekeya.

Kijumwa (1973) ametumia usimulizi maizi kuumba vihusika na wahusika wake. Tunapata taswira ya wenyeji ambao wana sifa ya usaliti kwa ajili ya tamaa ya madaraka. Ameonyesha kuwa tamaa na wivu dhidi ya wenzetu ndiyo hupelekea watu kutenda maovu. Aidha vihusika katika utenzi huu vimetumiwa kwa madhumuni ya kudhihirisha masuala fulani. Msitu ni kihusika alichoumba mshairi kitumike kumhifadhi Liyongo. Liyongo aliukimbilia msitu ili uweze kumhifadhi kwa kuhofia kuuawa. Sultani na utawala wa Pate wanatumia gereza kuwazuia watu waliokaidi maamuzi yake na utawala huo. Liyongo alizuiliwa humo ili asije akatoroka. Makoma yalitumiwa na wenyeji kama chakula wakati wa uhaba uliotokana na ukame na kiangazi. Usimulizi unatupa taswira ya kimo cha mikoma kuwa ni mirefu sana. Wagalla walitaka kumfuma Liyongo kwa mishale akiwa juu. Huu ni uhusika dhahiri kwa sababu mtunzi anasimulia kwa kutoa maelezo. Hivyo basi kupitia masimulizi uhusika unaibuka.

Mtunzi ametumia usimulizi wa nafsi ya tatu kuibua uhusika kwa kuwa ndiye msimulizi wa hadithi yote. Katika usimulizi huu mwandishi anajikita zaidi katika mhusika mmoja tu. Anajibana na kujipunguzia anayoyafahamu kwa kudhihirisha ufahamu wa mhusika mmoja peke yake. Yote anayoyajua ni kumhusu huyo mhusika na haonyeshi kuwafahamu wahusika wake wengine. Kwa hivyo, mawazo, mwelekeo na msimamo wa mhusika huyo mmoja ndio mwandishi anaoutambua kwa undani. Hapa mwandishi huwa amejipunguzia uhuru wake wa kuyaeleza yote anayoyajua kuihusu hadithi yake. Mhusika anayepewa nafasi hiyo aweza kuwa mhusika mkuu au mhusika mwingine yeyote hadithini. Msomaji analazimika kutazama mambo kupitia mhusika mmoja ambaye ni Liyongo.

Katika usimulizi wa aina hii mwandishi hutujuza mengi kuhusu mhusika mmoja kupitia usimulizi wake mwenyewe au kupitia masimulizi ya wahusika wenzake. Wahusika wengine hawashughulikiwi sana mathalan msomaji hawezi kufahamu mawazo ya wahusika wengine kupitia mwandishi ila anaweza kukisia tu sifa na mwenendo wa wahusika wengine kutokana na wanayosema wahusika wenzake hivyo basi kuibua uhusika husishi.

Nadharia ya usimulizi imewezesha kuibuliwa kwa uhusika na vihusika katika *Utenzi wa Fumo Liyongo.* Matukio katika utenzi huu yamehusu wahusika na vihusika. Ni wahusika ndio waliosababisha matukio yanayosimuliwa. Vipengele vya usimulizi vimetumiwa kubainisha, kuchunguza na kueleza uhusika unavyojitokeza katika utenzi huu. Sifa za wahusika zimefafanuliwa kupitia vipengele vya usimulizi. Kuna utoaji maoni ya kibinafsi ambao mhusika mmoja husimulia wazi jinsi anavyojiona mwenyewe kama alivyofanya msimulizi kuwahusu wahusika katika utenzi. Aidha kuna utoaji maoni kwa kando anavyofanya Sultani akimrejelea Liyongo hivyo basi kumwasilisha kama mhusika dhahiri. Mbinu za uhusika zinaweza kutokana na mkusanyiko wa kanuni za maonyesho au tamthilia. Mbinu zote za uhusika wa umbo-dhahiri huwa za mazungumzo. Uchanganuzi huu umebainisha maoni ya nafsi mbalimbali katika utenzi yanayomrejelea mhusika ambaye ni chombo kinachowasilisha ujumbe. Kulingana na Manfred (2005), tathmini ya uhusika huchunguza njia na mbinu za kuumba tabia za kibinadamu za wahusika dhahania. Utafiti huu umedhihirisha kwa kutathmini wahusika ama vihusika katika utenzi huu kwa kutoa maelezo kuhusu tabia na sifa za wahusika an vihusika. Utafiti huu umefafanua sehemu zinazochukuliwa na wahusika na vihusika katika mashairi na kudhihirisha utokeaji wa uhusika kama nani au nini.

## 4.3 Tathmini ya Usimulizi Unavyoibua Uhusika Katika Diwani ya *Kichomi*

Kezilahabi (1974) ametumia usimulizi maizi katika shairi lenye kichwa 'Dakika 15 za uzalendo' kuwaumba wahusika na vihusika. Wahusika waliosawiriwa katika shairi hili ni wakoloni, Nyerere, Bushiri, Mkwawa, Kinjeketile, Mirambo na Mbumi.

### 4.3.1 Wakoloni

Mtunzi kupitia usimulizi maizi anatujuza kuhusu kuja kwa wakoloni nchini Tanganyika. Mshairi anasimulia namna walivyoingia nchini katika ubeti wa kwanza. Sifa na hulka ya wakoloni inabainika kupitia usimulizi hivyo basi kuibua uhusika. Ni watu katili wasiokuwa na huruma kutokana na jinsi walivyowapiga makonde na hata kuwatemea mate nyusoni wenyeji. Mshairi amerudianeno wakoloni kusisitiza uchungu alio nao dhidi yao. Mtunzi ndiye msimulizi na anafahamu mengi kuhusu wahusika anaotujuza. Mtunzi ametumia usimulizi wa nafsi ya kwanza kufafanua tabia ya wakoloni. Katika mbinu hii ya usimulizi mwandishi hupotelea ndani ya mmoja wa wahusika wake ambaye husimulia hadithi yote. Mohamed (1995), anasema kuwa mbinu hii si rahisi kama inavyoonekana kwani mwandishi anapaswa kuwa makini asitumie 'ni' na 'mimi' kwa wingi hadi akawachosha wasomaji wake. Mbinu hii inawasilisha hadithi kama ambayo imesimuliwa na mmoja wa wahusika wake. Kuna matumizi ya kiambishi cha nafsi ya kwanza'ni'. Mtunzi anasimulia mienendo ya wakoloni bila kufafanua hadi pale mwisho inapobainika ni wahusika wenye sifa zilizotajwa.Katika ubeti wa kwanza anasimulia hivi:

Mfano 1. Wakoloni, wakoloni, wakoloni si walozi,
Wakoloni, wakoloni walipopiga mbizi,
Na bunduki mikononi, na midomo yao chini,
Walitupiga makonzi, tukatemewa nyusoni.

Katika mshororo wa nne ametumia kiambishicha nafsi 'tu' katika neno walitupiga akijirejelea yeye na wazalendo wengine waliokuwa wakipigwa na kuteswa.Huu ni uhusika dhahiri kwa

sababu mtunzi anatumia unenaji kutufafanulia tabia ya wakoloni. Kutokana na usimulizi wa mtunzi wakoloni ni watu wasiokuwa na utu. Mtunzi kupitia uzungumzi-nafsi ambayo ni aina ya usimulizi wa nafsi ya kwanza anatupa taswira ya maumbile ya wakoloni yanayotisha. Anasimulia waziwazi maumbile yao kudhihirisha maudhi aliyo nayodhidi yao kutokana na unyama waliowatendea wazalendo. Usimulizi huu unabainisha hulka ya wakoloDni, hivyo basi kuibua uhusika wa nafsi dhahiri. Katika ubeti wa tano anasimulia maumbile yao kwa kusema :

Mfano 2. Kumbukeni pua zao, zimechongoka zatisha
Kumbukeni ngozi yao, nyama mbichi yatisha
Uliza chakula chao, vyura nchini vyaisha,
Je, vipi walitushusha, tukawa watumwa wao!
Ala!

Msimulizi ni mmoja wa wale wanaoteswa na wakoloni jambo linalomfanya kuudhika kutokana na tabia yao. Uhusika wa nafsi dhahiri unaibuliwa kutokana na uhusika wake kwa sababu msimulizi ni mmoja wa wahusika. Anasimulia kuhusu maumbile ya wakoloni yasiyopendeza anapoeleza kuhusu pua zao zilizochongoka. Rangi ya ngozi yao ni nyekundu kama nyama mbichi wala si nyeusi kama ya wenyeji. Ni rangi geni ambayo hawakuizoea wenyeji, aidha unyama wao dhidi ya wenyeji unamfanya mshairi kuchukizwa hata zaidi na mienendo ya watu hawa. Chakula wanachokula si cha kawaida. Watu hawa wanakula vyura na haoni jinsi watu wa tabia kama hii waliweza kuwateka na kuwadunisha wenyeji kiasi cha kuwafanya watumwa. Kupitia usimulizi maizi taswira ya maumbile yaoinabainika. Hulka ya wakoloni ya kula vyakula visivyostahili inadhihirika kupitia usimulizi hivyo basi kuibua uhusika dhahiri. Mtunzi anatoa maelezo ya moja kwa moja kuhusu maumbile ya wakoloni kiasi kwamba ni rahisi kwa msomaji kupata picha ya wale wanaoelezwa.

### 4.3.2 Bushiri, Mkwawa, Kinjeketile, Mirambo na Mbumi

Mtunzi anatumia usimulizi maizi kutupa taswira ya wahusika jasiri. Kama ilivyokuwa katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* Wakoloni walikuwa katili kiasi kilichowafanya wazalendo kusimama kidete na kuongoza maasi dhidi ya utawala wao. Mtunzi amesimulia sifa za Bushiri, Mkwawa, Kinjeketile, Mirambo na Mbumi katika ubeti wa tano. Mtunzi anaeleza hadithi ambayo yeye haimhusu ila ni msimulizi tu wa matukio aliyoyaona. Anaelewa kila kitu kilichotendeka. Mtunzi ameibua uhusika kupitia unenaji na maelezo. Katika ubeti ufuatao anatoa maelezo kuhusu wahusika wenye sifa zilizofanya nchi isiweze kuharibika na kuwaliza wazalendo.

Mfano 1. Lakini tusijelia, nasana kusikitika
Nawaomba kutulia, muwajue wasifika,
Nguzo waloshikilia, nyumba isije anguka,
Nasi nje tukatoka, nchetu tukalilia

Katika beti zinazofuata anataja sifa za wahusika kwa majina hivyo basi kuibua uhusika kupitia uwasilishaji dhahiri kwa msomaji. Anaeleza sifa na matendo ya wahusika kwa kutumia njia ya ufasiri wa moja kwa moja.

Mfano 2. Ninaanza na Bushiri, liyeongoza maasi,
Mkwawa wetu mahiri, Mhehe mwenye makasi,
Kinjeketile tumkiri, na maji yake halisi,
Mirambo mkata rasi, Mbumi mke shuhuri,

Hao ni wetu wahenga, walopinga ukoloni,
Sasa kikia mtunga, aliyetutoa soni,
Wakoloni kuwafunga, kuwatosa baharini,
Kwa utulivu na amani, vizuri akatuunga.

Njia hii ya uwasilishaji dhahiri inamfanya msomaji asipate taabu kufahamu kiini cha kisa, wazo au dhamira kwa kutumia mhusika au wahusika kutoka mwanzo wa hadithi. Hivyo basi ni dhahiri katika utunzi huukuwa ni ujasiri wa wahusika waliotumiwa, walijitoa mhanga kupigania

ukombozi kwa udi na uvumba ndipo uhuru ukapatikana. Anasimulia haya katika ubeti wa tano, sita na saba.

### 4.3.3 Nyerere

Usimulizi wa mtunzi kwenye ubeti wa nane unatupa taswira ya mhusika kwa jina Nyerere. Ana sifa ya kujituma. Kupitia unenaji ulio wazi mtunzi anasimulia jinsi alivyowanusuru kutoka utumwani hivyo basi kuibua uhusika dhahiri. Anatutajia jina la mhusika na jinsi alivyoamua kuacha kazi ili kuwatetea wananchi. Kutokana na maelezo ya mtunzi ni rahisi kueleza sifa za Nyerere. Anasimulia haya katika ubeti wa nane anaposema :

Mfano 4. Ni Nyerere jina lake, simba dume dududmizi,
Liyeacha kazi yake, akawe wetu mlinzi,
Kila mtu awe na chake, na uhuru lake vazi,
Nyerere ni wetu mlezi, lisifike jina lake.

Mtunzi anamfananisha mhusika na simba katika mshororo wa kwanza kutokana na juhudi zake za kuwalinda baada ya kuacha kazi yake. Alifanya kila jitihada kuona kwamba kila mtu anakuwa huru na anaweze kumiliki kilicho chake bila ya kuhujumiwa. Hivyo basi uhusika wa Nyerere unabainika kupitia usimulizi.

Mtunzi ni mhusika katika shairi ‘Hadithi za kitoto’ kwenye ukurasa wa 42, anapochukua nafasi ya msimulizi. Hivi ni kusema kwamba ndiye mhusika mkuu. Kupitia usimulizi wake ni dhahiri kwamba ni mkongwe kwa kuwa ameketi na wajukuu wake. Wamemzunguka huku wakiota moto. Kupitia usimulizi wa nafsi ya kwanza katika mshororo wa tisa ubeti wa kwanza anasema:

Mfano 1. Wajukuu, wamenizunguka; maana nimezoea
Kuwasimulia hadithi za uwongo,

Utambaji wake huu unaibua uhusika nafsi. Aidha kupitia usimulizi msomaji anaweza kupata taswira ya umbo lake anapoanza kusoma shairi. Ni kutokana na umri wake mkubwa ndipo mgongo ukaweza kupinda kama anavyosimulia. Kupinda huku kwa mgongo ni dhihirisho la umri wa mhusika kuwa ni mkongwe.

Mfano 2. Nipo hapa, nimekaa, mgongo upinde,
Nikiyanung'unikia mawingu ya mashariki,
Nikiota moto, ambao naomba
Usizimike mpaka kesho asubuhi.
Mara kwa mara ninapapasa miundi,
Kupunguza joto.
Ninasonga nyuma na mbele
Kufuatana na ukavu wa kuni.
Wajukuu, wamenizunguka; maana nimezoea
Kuwasimulia hadithi za uwongo,
Lakini zenye ukweli.
Wanacheka wakati sicheki
Nacheka wakati hawacheki.

Anaeleza kuwa kusimulia hadithi ndiyo ada na watoto wanafurahia hadithi hizo kwa kumhimiza kuwasimulia hadithi kama wafanyavyo katika mshororo wa tisa ubeti wa pili. Uhusika simulizi unabainika katika shairi hili.

Mfano 1. "Tusimulie hadithi," wanasema
"Jana ulitueleza juu ya vidonda vyako
Leo tusimulie hadithi ingine!"

Wahusika wengine ni watoto ambao ni wajukuu wa msimulizi. Kinachodhihirika ni kwamba wanapenda kuketi na huyo babu akiwasimulia hadithi ambazo wao hufurahia japo nyingi huwa ni za uwongo lakini zilizo na ukweli. Maelezo haya yanadhihirisha ubunifu wake wa hali ya juu unaofanya masimulizi yake kuonekana kuwa kweli ilhali siyo hivyo.

Msimulizi anaanza kuwasimulia watoto hadithi ambayo ni utenzi unaoanza kwenye ukurasa wa 42. Msimulizi ambaye ndiye mhusika mkuu anatupa taswira ya wahusika na vihusika kwa maelezo.Kupitia usimulizi maizi uhusika dhahiri unaibuka. Msimulizi ambaye ni mmoja wa wahusika anatumia mbinu ya uwasilishaji dhahiri kuibua uhusika dhahiri hivi kwamba msomaji anapata kumwelewa mhusika anayezungumziwa ama wahusika wanaozungumziwa.

### 4.3.4 Wesema na Mumewe Kasinge

Msimulizi anatusawiria wahusika wawili, mama kwa jina Wesema na mumewe Kasinge ambao walijaliwa kupata mtoto msichana kwa jina Kanana. Kupitia usimulizi maizi uhusika waWesema, mumewe Kasinge na Kanana unadhihirika kutokana na matendo yao jinsi yanavyosimuliwa. Sifa za wahusika  hawa; ni washauri wema kutokana na namna ambavyo walivyomwelekeza binti yao. Walikuwa na mapenzi ya dhati kwa binti yao Kanana. Walimtunza vizuri kwa sababu alikuwa na tabia njema.  Aidha ni wazazi wanaothamini asasi ya ndoa kwa sababu hata baada ya binti yao kurejea nyumbani walimhimiza arudi kwa mumewe kwa kuwa ndoa ni kuvumiliana. Wanamshauri arudi kwa mumewe hadi kifo kiwatenganishe. Kanana anaridhia ushauri wao na kurudi kwa mumewe. Kutokana na masimulizi haya uhusika dhahiri unabainika. Uhusika unabainika kupitia maelezo ya mtunzi kuhusu wazazi wa Kanana.

Utafiti umeweza kutahtmini namna uhusika wa Wesema na Kasinge unavyojitokeza. Walikuwa na mapenzi ya dhati kwa binti yao kwa kumuadilisha kama wazazi na kumpeleka shule kupata elimu. Aidha utafiti umepambanua aina za uhusika pale ambapo hadhira inaonyeshwa mambo yanayotambulisha nafsi za watu hawa na taarifa inayobainisha tabia za watu hawa. Ni watu

wanyenyekevu wasiokuwa na pupa hususan kutokana na kitendo cha binti yao kuamua kurudi kwao. Badala ya kutafuta sababuya kutengana na mumewe wanamshauri binti yao arudi. Utafiti umechunguza namna taswira imeumba wahusika hawa kupitia usimulizi wa mtunzi.Usimulizi unatupa picha ya mawazo ya wazazi hawa, si watu wanaopenda vurugu ama mivutano hasa katika maisha ya ndoa kati ya binti yao na mumewe. Wamepitia maisha haya na wanahisi kwamba binti yao hana budi kuvumilia. Kutokana na tathmini ya namna uhusika unavyojitokeza katika ushairi utafiti ulifikia lengo lake kwa kuchunguza namna taswira huumba wahusika katika ushairi wa Kiswahili.

### 4.3.5 Kanana

Msomaji wa shairi anaweza kubaini uhusika wa Kanana kuwa ni mke wa Katili kupitia usimulizi maizi. Kanana hakuwa na stahamala kutokana na uchochole wa mumewe hali iliyomfanya kurudi kwao kwa kushindwa kuvumilia maisha magumu. Hali hii inadhihirisha ukosefu wa subira na mtu anayekata tama haraka. Katika ubeti ufuatao mtunzi anasimulia ifuatavyo:

Mfano wa 2. Mwezi mmoja kupita
Kanana karudi nyumbani
Akasema yule bwana
Hana vitu wala pesa,
Na maisha, ni magumu.

Sifa ya uchangamfu ya Kanana inabainika kupitia usimulizi maizi. Mtunzi anasimulia ifutavyo katika ubeti wa tisa wa utenzi kwa kusema:

Mfano 3. Kanana msichana mzuri
Akacheka na wavulana,
Njiani akawa nao, masomo
Kuyazungumzia. Lakini
Kamwe, hawakumvunjia
Heshima.

Alipojumuika na wavulana akitoka ama akielekea shuleni walijadili kuhusu masomo. Hakujihusisha na masuala mengine ambayo yangeweza kumharibia maisha yake ya siku za usoni. Sifa ya mhusika inayodhihirika hapa ni ya mtu aliye na msimamo thabiti.

Kanana anapokubali kurejea kwa mumewe ni dhihirisho la mtu mwepesi kushawishika na aliye na heshima kwa wazazi. Kanana hakuwa na budi kurejea kwa mumewe baada ya wazazi wake kumfahamisha katika ubeti wa kumi na nne kwamba hiyo ndiyo maana ya ndoa. Kwamba ndoa ni kuvumiliana hadi pale kifo kitakapowatenganisha. Iwapo angeshikilia msimamo wa kutorudi labda hadithi ingekamilika. Mtunzi amemuumba mhusika huyu na kumpa sifa hii makusudi kuendeleza hadithi.

Matatizo yanazidi pale ambapo wanajaliwa kupata mtoto. Kutokana na hali ngumu wanayopitia Kanana hana budi kukopa pesa kwa jirani mwanamme. Jirani naye anatumia fursa hii kumvunjia heshima kwa kuzini naye. Hali hii inamfanya Kanana kupoteza sifa yake yauadilifuhivyo basi kuwa mke duni. Hali inakuwa mbaya sana pale anapojifungua mtoto ambaye anafanana na jirani. Katika ubeti wa thelathini na nne, ukurasa wa 45 mtunzi anasimulia shauku ya mumewe kwa mwana aliyezaliwa ifuatavyo;

Mfano 4. Ilitokea siku moja
Katili akamwambia mkewe;
Mke wangu nina shaka,
Huyu mtoto wa pili
Anafanana na jirani.

Mtunzi anasimulia kitendo cha kikatili alichotekeleza Kanana kwa ajili ya kupata mtoto nje ya ndoa. Kanana anashindwa kustahimili, hivyo basi kuamua kumwangamiza mtoto kwa kuwa ni

mwanaharamu. Anashikwa na wazimu baada ya kutekeleza kitendo hicho hali inayomfanya kupagawa na kukimbia ovyo msituni.

### 4.3.6 Katili

Kupitia usimulizi inabainika kuwa Katili ni mumewe Kanana. Sifa ya Katili inayodhihirika ni fukara asiyeweza kufanya kazi. Ni mzembe, hivyo basi hawezi kukidhi mahitaji ya familia yake kama vile chakula.ifa ya Katili inaibuliwa na masimulizi ya mkewe anaporejea kwa wazazi wake. Inakuwa vigumu mkewe kustahimili maisha magumu na anarudi kwao.

### 4.3.7 Jirani

Vitendo vya mhusika huyu vinatupa taswira ya unafiki. Anamsaidia Kanana anapohitaji msaada lakini hakuwa na nia njema. Alitumia fursa hiyo ya matatizo anayokumbana nayo Kanana kudhihirisha sifa ya uzinzi. Kanana anashika mimba kutokana na uzinzi. Anamuua mtoto huyo baada ya mumewe kugundua kuwa mtoto aliyezaliwa hakuwa wake. Ni kinayamtunzi kumsawiri mumewe Kanana kama mtu mpole na kumpa jina Katili ilhali kuna mhusika katili aliyestahili jina hilo kutokana na vitendo vyake lakini hatutajiwi jina lake.

### 4.3.8 Sauti

Kihusika sauti kimeibuliwa na mtunzi kupitia usimulizi hakionekani ila sauti tu ndiyo inayosikika. Nafsi neni ni sauti. Sauti hii inajitokeza kuwa ni ya jitu lisiloonekana machoni mwa watu ila Kanana peke yake. Baada ya kupagawa Kanana anakabwa na hili jitu lisiloonekana linalomuuliza maswali. Katika ubeti wa arobaine na tano ukurasa wa 46 sauti inasema:

Mfano 5. Kanana mwana Wesema
Wapi sasa unatoka?
Na huko utokako
Umetenda jambo gani!
Ni mimi nakuuliza.

Sauti imetumiwa kimakausudi na mtunzi kuwakilisha nafsi inayotetea haki ya binadamu ya kuishi. Ni wazi kwamba baada ya kutekeleza mauaji ya mwanawe, Kanana hakuona raha maishani. Kupitia usimulizi wa sauti mtunzi anaibua uhusika nafsi. Huu ni uhusika wa nafsi uwili kwa sababu kuna mazungumzo baina ya sauti na Kanana. Kanana anakwenda kumtazama mwanawe iwapo alikuwa angali hai ili amchukue, lakini anakuta kuwa alikwisha aga dunia. Anapagawa na kukimbia peke yake. Kisa na maana ya kukimbia ni kwamba anafukuzwa na jitu lililobeba kisu mkononi. Baada ya miezi miwili ya matatizo ya akili na kukosa kupata chakula Kanana anakufa akiwa amekonda sana na macho kumwingia ndani. Kupitia uhusika simulizi tunaona hali ya Kanana inavyobadilika hadi pale anapoaga dunia katika hali ya kusikitisha sana. Katili mumewe Kanana anagundua kisa cha mkewe kurukwa akili.

### 4.3.9 Wajukuu

Kupitia usimulizi wa mtunzi inabainika kuwa wajukuu ni watulivu na wenye hamu ya kusikiliza hadithi. Kutokana na athari ya matukio katika hadithi wanabaki wamezubaa na kusikitika. Hakuna yeyote aliyeuliza swali kuhusu nani alimkaba roho Kanana au jitu lililomfukuza daima likiwa na kisu mkononi lilitoka wapi. Kisa hiki kinawafanya kusahau shughuli waliokuwa wakifanya ya kuchoma ndege motoni ili wale. Mtunzi anatupa taswira ya wahusika kupitia usimulizi kwa kutuchorea picha halisi ya mazingira yao.

Kezilahabi (1974) ametumia uhusika wa nafsi kudhihirisha hali halisiya siasa ya nchi ya wakati huo. Huu ni uhusika simulizi kwa sababu anashiriki katika matukio kupitia wahusika wengine. Anasisitiza kwamba hata kama walio na mamalaka watafanya jambo gani, iwe kuwaua wanasiasa kama vile kuwaua wanaharamu sauti ya haki ipo na itawaandama daima. Hakuna binadamu aliye na haki ya kutoa uhai wa binadamu mwenziwe ila mwenyezi Mungu pekee. Utafiti huu unadhihirisha uhusika katika ushairi kwa sababu kisa kimesimuliwa kupitia wahusika na kisa chenyewe kinawahusu watu. Msimulizi ametumia uhusika husishi ambapo mmoja kati ya wahusika ndiye msimulizi hivyo basi kupitia kwake tunapata maelezo kuhusu wahusika wengine. Anafafanua hali za wahusika wengine katika utenzi hivi kwamba msomaji anapata uelewa wa tabia na mwenendo wa mhusika anayewasilishwa .

### 4.3.10 Usimulizi Unavyoibua Vihusika Katika Diwani ya *Kichomi*

Kezilahabi (1974) ametumia vihusika vya aina mbalimbali katika mashairi ili kueleza ama kutoa taswira ya hali mbalimbali zinazoikumba jamii. Usimulizi huu ni tofauti na ule uliotumiwa katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Mtunzi ametumia sitiari katika usimulizi wa mashairi yake. Baadhi ya mashairi yake yanayohusu vihusika ni Jinamizi, Upepo wa Wakati, Mwamba Ziwani, Mto Nili, Mgomba, Uvuaji Samaki, Fasihi, na Mto wa Haki. Mtunzi ametumia vihusika hivi kimafumbo ili kuwasilisha ujumbe unaohusu jamii yake inavyodhulumiwa na watu ambao si wenyeji.Katika shairi 'Jinamizi' ukurasa wa 3 anasema:

Mfano1. Watu weusi na weupe
Mtumbwini walikuwa wamesimama, wametulia
Na fimbo ndefu mikononi mwao,
Na macho yao wameyakazia majini.
Samaki ambaye, kupata hewa,
Aliinua kichwa chake juu ya maji
Utawala wa chuma ulimtoboa fuvu
La kichwa na kutupwa mtumbwini

Halafu nilifikiri Afrika
Na siasa kwa ujumla
-Mafuvu!

Katika mishororo minne ya kwanza ya ubeti wa pili anaendelea;

Lakini mamba, kwa maelfu
Mtumbwi waliukimbilia kwa fujo,
Mtumbwi kupasuka wakatatuliwa
Vipande vipande.

Mtunzi ametumia usimulizi maizi kuibua vihusika mtumbwi, chuma, fimbo, samaki na mamba Kihusika mtumbwi ni himaya ya wenyeji hawa. Himaya hii ni bara la Afrika ambalo wenyeji wake ni watu wasio na uwezo kiuchumi.

Mtunzi ametumia rangi kama kihusika. Rangi nyeupe na nyeusi jumla ya uwezo kiuchumi kwenye himaya hiyo. Weupe ni uwezo ilhali nyeusi ni ukosefu wa uwezo. Wenye rangi nyeupe wameshikilia fimbo ndefu mikononi. Kihusika hiki ni kifaa cha kuwakandamiza wasiokuwa na uwezo. Samaki ni wenyeji wasiokuwa na uwezo kiuchumi, wamesakamwa na umasikini kiasi cha kukosa hewa safi ya kupumua, kila wanapojaribu kuinua vichwa ili wapate hewa safi hunaswa kwa kutumia chuma kinachotoboa mafuvu yao na kutupwa mtumbwini. Ndoano ni kifaa cha kunasa samaki na huwa na chuma kilicho na ncha kali. Ndoano huundwa kwa fimbo ndefu na chuma nchani mwake.

Mtunzi anasimulia kuhusu Afrika na siasa kwa ujumla anaposema:

Afrika na siasa zake ni mafuvu tu.

Mtunzi ametumia sitiara kama mbinu ya kisanaa kumaanisha Afrika ni bara lililojaa wafu. Anafananisha waafrika na mafuvu ya watu waliokufa. Aidha mtunzi ametumia wahusika

wanyama kama mamba na samaki kuwakilisha wananchi wa mabara mengine yalioendelea ambao hufaidika kwa kuwala hawa samaki baada ya mitumbwi yao kupasuka. Mamba ni wanyama wakali mno na wasiokuwa na huruma. Hawajali iwapo waafrika ni binadamu au la. Azma yao ni kupata mahitaji yao ili kuendeleza nchi zao. Baada ya kuzuka fujo na ghasia katika nchi za Afrika mataifa yalioendelea hukimbilia bara la Afrika ili kuligawanya zaidi kwa faida yao. Hivyo basi kupitia usimulizi uhusika unaibuliwa katika shairi hili kwa kutumia wanyama na vihusika vingine kueleza hali ilivyo katika bara la Afrika.

Kihusikamgomba kimeibuliwa kupitia usimulizi maizi katika shairi ‘Mgomba’ lililo kwenye ukurasa wa 8. Katika ubeti wa kwanza anasema:

Mgomba umelala chini:hauna faida tena,
Baada ya kukatwa na wafanyakazi
Wa bustani kwa kusita.
Watoto, kwa wasiwasi wanasubiri wakati wao
Bustanini hakuna kitu
Isipokuwa upepo fulani wenye huzuni,
Unaotikisa majani na kutoa sauti ya kilio.

Mgomba ni rasilmali ya nchi kama ilivyo ardhi. Ardhi ni  rasilmali inayozalisha mazao tunayopanda na madini vile vile hupatikana ardhini. Rasilmali hii imeharibiwa na watu waliotaka kufaidi kwa manufaa yao bila kuwajali wenyeji. Badala ya kuhifadhi mazingira kwa kulinda mazao yaliyomo  wanayaondoa ili kunyakua hiyo ardhi ama uwanja. Wafanyakazi hawa ni mabwanyenye.  Wananyakuwa mashamba na viwanja vilivyotengwa kwa minajili ya watoto kuchezea na watu wazima kupumzika wakipunga hewa safi. Baada ya kuondoa mazao haya bustani inabaki tupu bila kitu, hali inayochafua mazingira kwa kuvumisha upepo usiokuwa na manufaa ila huzuni kwa wenyeji. Upepo ni hali mbaya katika mazingira. Hivi ni kusema

kwamba kutokana na ukataji wa mimea kuna uchafuzi wa hewa. Mimea husafisha hewa na kuifanya iwe ya kuvutia.

Katika shairi 'Fasihi' lililo kwenye ukurasa wa 14 Kezilahabi (1974) ametumia vihusika kama vile boga, bustani, miti, magugu, matunda, jembe, wino, mikata, mitungi, mbegu, vikombe, dhahabu na glasi. Mtunzi ameibua uhusika nafsi kwa kutumia vihusika hivi katika nafsi ya kwanza kwa kujilinganisha navyo.

Mfano 1. Maneno yangu kumeza tena sasa siwezi.
Lakini kuonyesha ukweli na kuutafuta
Nitaendelea: mimi ni kama boga.
Nimepandwa katikati, bustanini,
Na kama boga nitatambaa chini
Zote pande, kuikwea miti ya hekima
Na yote magugu koo kuyakaba.
Bila woga, bila nyuma kurudi nitashambulia
Ya binadamu matendo bado yakihema.
Halafu wakati
Ujao utafika
Matunda nitatoa
Makubwa madogo
Mazuri mabaya
Wakati utafika watakapokuja wajuzi
Kwa jembe la wino kunipalia.
Wala mboga za majani watanichuma.
Utafika, wa maboga kuwa mikata.
Machafu na safi yatachotwa
Na nitaingia mitungi ya kila mji-shamba.
Watoto mikononi mwao watanichezea.
Chini wataniangusha na kunipasua.
Lakini mbegu, mbegu zitabaki.
Mimi ninajua
Hatari sina
Wajibu msomaji
Mjini na shamba
Vizuri kunichambua.
Halafu utafika ule wakati
Watumia vikombe dhahabu na glasi
Pembeni kwa chuki kunitupa,
Na nitakuwa nyuma ya wakati

Lakini wakisahau wahenga
Kata na mboga walitumia
Msingi wa wao utamaduni
Watakuwa wameutupa.
Kumbukeni, kumbukeni, kumbukeni.

Katika shairi hili mtunzi ametumia vihusika kimafumbo kupitisha ujumbe. Anaeleza jinsi ambavyo utamaduni, mila na desturi za Waafrika zinaweza kuangamia iwapo tutatupilia mbali fasihi yetu kama waafrika. Fasihi ni kioo cha jamii, hivyo basi Waafrika hawana budi kukumbuka na kuukumbatia utamaduni wao kwa hali na mali.

Boga limepandwa katikati ya bustani. Nafsi-neni ni boga. Kihusika hiki kimehuishwa kwa kutumia nafsi ya kwanza kutetea utamaduni. Boga linaeleza jinsi litakavyotambaa chini kila upande na kuikwea miti yote ya hekima kueneza umuhimu wa utamaduni kwa jamii nzima. Litakaba koo za magugu yote ambayo ni pingamizi katika udumishaji wa utamaduni.

Mtunzi anasema kwamba hatabadilisha nia ila ataendelea kushambulia matendo mabaya ya binadamu. Kutokana na mashambulizi wakati utafika na matunda yataonekana. Vihusika matunda ni mazao ya kazi yake nayatakuja kwa viwango tofauti. Kutakuwa na matunda makubwa na madogo. Matunda mengine yatakuwa kwa hali nzuri na mengine hali mbaya. Kuna wale watakaopata manufaa makubwa na wengine manufaa madogo. Cha muhimu hapani kwamba kila mmoja atanufaika kwa njia moja au nyingine japo si kwa viwango sawa.

Mtunzi anasimulia wakati ambapo watakuja watu wenye ujuzi. Wenye ujuzi ni watu wenye elimu ya darasani, wanaotumia kalamu. Kihusika jembe kinatumika badala ya kalamu. Awali

jembe limetumika kama kifaa cha kuzalisha mali lakini baada ya kuja elimu ya darasani kihusika kalamu kimechukua nafasi ya jembe. Umuhimu wa vihusika unategemea nyakati.

Boga linasema kuwa wanaokula mboga za majani watamchuma. Boga linamaanisha kuwa wataondoa majani yake kwa kutumiwa kama chakula lisiweze kunawiri. Baada ya kuchuma majani mikata ndiyo itakayobaki. Kata hizi ni vifaa vilivyo na manufaa kwa watu kwa kuwa vitatumiwa kuchotea maji. Maji ni kihusika kinachotumiwa kwa shughuli mbalimbali za kuendeleza maisha ya jamii. Maji yanapotiwa  mitungini hutumiwa na watu wanaoishi mijini kwa kupikia na kunywa. Shambani ni vilevile. Kwa kuwa kata ni kifaa kinachoweza kupasuka wakati wowote hapana budi wakati utafika na kitapasuka kwa kuchezewa na watoto. Mshairi anasema japo ataangamizwa mbegu zitabaki. Mbegu ni chembechembe za utamaduni. Anamaanisha kwamba utamaduni hauwezi kuangamia kabisa mradi kuna chembechembe zake katika jamii.

Katika ubeti wa mwisho mshairi anawakumbusha waja wanaotumia vyombo vya kisasa kama vile vikombe vya dhahabu na gilasi kuwa japo wamesoma, wakiwa mjini au shamba wanapofanya uchambuzi wao wafanye kwa makini. Wasimwone kuwa amepitwa na wakati na kutupilia mbali kata kwa sababu kabla ya kuvumbuliwa hivyo vyombo wanavyotumia sasa vilikuwepo vya kitamaduni. Kupitia usimulizi mtunzi ametumia vihusika kuwasilisha ujumbe unaohusu jamii na kwa kufanya hivi ameibua uhusika simulizi kwakuhuisha kihusika ambacho kinasimulia matukio anayoyatarajia.Aidha, Kezilahabi (1974) ameibua kihusika mwambakupitia usimulizi maizi katika shairi ‘Mwamba Ziwani’ kwenye ukurasa wa 6.

Mfano 2.	Hautingishiki, hauzungumzi: umekufa;
Lakini ninaweza kuusikia ukizungumza:
“Kijana mimi sicheki, uwe hivyo na wewe.
Tazama jinsi ndege walivyokifanya kichwa changu
Cheupe kama mchwa na fuvu, mimi nimetulia,
Sina wasiwasi ingawa naonekana mjinga.
Mawimbi yananigusa na kuvunjika
Kama upanga wa muuaji ushindwavyo kwa roho.
Mimi ni imara na sihamishiki.
Na mtu mwovu siumiziki.”
Huo mwamba umekwenda. Siwezi tena kuuona.
Hapa ndipo nilipo, melini, mtu mwovu,
Na mwenye wasiwasi
Nikisukumwa na mawimbi,
Nikitetemeshwa na mapaja ya huyu msichana
Mbichi karibu nami. Lakini ule mwamba,
Ule mwamba ulikuwa umekufa.
Wakati wote niishipo sitaweza, nao kufanana.
Nitakapokufa kama huo mwamba,
Huo mwamba nitaushabihi.

Mtunzi ametumia usimulizi kuibua uhusika wa nafsi-umoja. Nafsi neni katika utungo huu nimzee aliyekomaa kiumri. Japo msimulizi ni mmoja mazungumzo yanadhihirisha mazungumzo kati ya wahusika wawili hivi kwamba mhusika mmoja anarejelea kihusika mwamba. Uzungumzi halisi ulio kwenye alama za unukuzi unaoelekezewa nafsi nenewa unadhihirisha kuwepo kwa wahusika wawili. Kinachobainika katika mazungumzo haya ni nafsi neni ambayo ni mzee anayetoa wosia kwa kijana. Vihusika kama vile mchwa, ndege, mawimbi, mwamba, meli vimetumika kueleza hali mbalimbali. Mzee anajifananisha na mwamba ulio imara na hauhamishiki wala kuumizwa na mtu mwovu. Anasema kuwa hajafa hivyo basi hawezi kuwa kama mwamba ila tu pale ambapo atakuwa amekufa. Mawimbi ni kihusika kilicho na uwezo mkubwa kuburura chochote kilicho mbele yake. Mwamba umetumika kuwakilisha uthabiti wa mhusika ambaye kutokana na msimamo wake ni vigumu kumbadilisha kitabia ama kimatendo. Mshairi ametumia mbinu ya tashihisi kuvipa vitu hivi uhai kana kwamba ni wahusika wanadamu

hivyo basi uhusika wa kihisia unadhihirika katika shairi hili. Wahusika na vihusika hivi vinadhihirisha uhusika katika ushairi wa Kiswahili.

## 4.4 Usimulizi Unavyoibua Uhusika Katika Diwani ya *Malenga wa Vumba*

Boukheit (1981) ametumia usimulizi kutambulisha wahusika katika mashairi yake. Usimulizi nafsi umejitokeza katika baadhi ya mashairi kama vile katika shairi aliloliita 'Mwana Wacha Ufidhuli'. Kupitia usimulizi tunatambua hulka ya mwana anayerejelewa kuwa ni fidhuli, ana kiburi na hawatambui wazazi wake wala watu wa aila yake. Tabia hii inasababishwa na madaraka aliyo nayo mwana huyu na maisha ya anasa anayoishi. Anasahau kwamba hao wazazi anaowadharau ndio waliomzaa na kumtunza hadi hapo alipofikia. Usimulizi unaodhihirsha hulka hii umo katika beti zifuatazo:

Mfano 1. Huna ulichokijuwa, zaidi kwingi kulia,
Wali ukiinuliwa, mwenyewe wajiharia,
Kunena hujaelewa, hutambuwi kwashiria, (ubeti 2:59)
Wali ukiangaliwa, mahitaji kukisia,
Na leo wawaringia.

Madaraka yakufanya, ukatae utumishi,
Sibabu wala si nyanya, kabisa hakufundishi
Ijapo wangakuonya, waona ni tashwishi, (ubeti 3:59)
Maadamu leo wanya, kisha wapiga fulashi,
Hilo mwana halitoshi.

Kupitia usimulizi wa nafsi ya tatu mtunzi ametusawiria mhusika ambaye baada ya dhiki ya kumkimu na kumpa msingi anatokomea na kuwasahau walioshughulika na ulezi wake. Mtunzi amejikita katika mhusika mmoja tu. Anadhihirisha ufahamu wa mhusika mmoja peke yake. Watu wenye tabia za mhusika kama huyu hawakosi katika jamii hivyo basi ni kielelezo cha watu wa aina hiyo. Wahusika wanaweza kuwa wa aina nyingi katika mashairi kutegemea jinsi walivyowasilishwa. Katika shairi hili mtunzi anaibua uhusika wa nafsi umoja kwa sababu

msimulizi ni mtunzi mwenyewe akilalamika kuhusu tabia ya mwana dhidi ya mzazi. Huu ni uwasilishaji dhahiri kwa sababu mtunzi anasimulia kuhusu yale anayoyaona yakitendwa na mwana kwa mzazi wake. Anaibua uhusika wa mwana hivi kwamba sifa ya kiburi ya mwana inabainika waziwazi.

Katika shairi 'Huyo si mwenzio' kupitia usimulizi inabainika taswira ya mtu asiye na manufaa. Mtu huyu hafai kwa ajili ya kutaka kufaidika kutoka kwa mwenzake kwa sababu ya kumuona kuwa na mali. Anamuasa mwenziwe kuhusu mtu ambaye hafai katika ubeti ufuatao:

Mfano 2. Yule anakuthamini, kwa sababu una kitu,
Usambe akutamani, kwa kuwa mwema wa utu,
Kiwa huna humwoni, atakwacha mwanakwetu, (ubeti 2: 59)
Asikutishe si mtu, si shani kuwa fisi.

Mtunzi kupitia usimulizi wa nafsi ya kwanza ameibua uhusika simulizi hivi kwamba amechukua nafasi ya mhusika mmoja anayemuonya mwenzake dhidi ya mhusika mwingine anayetaka kufaidika kwa sababu ana mali.

Boukheit (1981) ametumia uhusika simulizi katika shairi 'Ufunguo wa Maisha' ukurasa wa 41. Katika shairi hili msimulizi ni mwalimu hodari wa kufunza watu utu, busara na tabia njema. Mtunzi ametumia mbinu za kutoa funzo la kuwakumbusha wazee wajibu wao wa kutoa mafunzo na nasaha bora kwa watoto wao. Vilevile katika shairi hili mzee anawafunza vijana pindi wajaliwapo kupata watoto. Funzo analowapa ni kuwapa wana wao mambo mawili muhimu katika maisha yao ambayo ni elimu na adabu njema. Mambo haya ni muhimu kwa sababu elimu bila ya adabu ni kama mtu aliyevaa tai na huku yu uchi!Katika ubeti wa tisa anampa nasaha kijana wa kileo kwa kumwambia:

Mfano 3. Mwanangu nakuadibu, babiyo nishachakaa
Wanao funza adabu, ujaliwapo kuvyaa,
Kukwambia ni wajibu, kabla yakwe fajaa,
Katika ya manufaa, mojawapo ni elimu

Mtu asiyewapa wanawe elimu atakuwa amewaua wakiwa wangali hai. Isitoshe, katika shairi 'Tamadunizo Siase' katika ukurasa wa 51, mtunzi ametumia uhusika simulizi kuwapa funzo wasomaji. Ni msimulizi mwenye busara kwa sababu anataka wasomaji wajue njia inayofaa na ile isiyofaa katika kuiga utamaduni wa kigeni. Anatoa waadhi katika ubeti wa 17 anapowaasa wasomaji waache kuiga maadili ya kigeni yasiyopendeza na kushikilia utamaduni wao utakaowaongoza kutenda yaliyo mema.Dhamira yake ni kuwa wasomaji waerevuke. jambo linalodhihirika ni kujiepusha na ukengeushi na kuuasi utamaduni wetu.

Twalonena si kidogo, mengi tumezungumza,
Tuipunguze miigo, kuiga yasopendeza,
Asili kuipa kisogo, utumwa twajifungiza,
Twige ya kutuongoza, kwenye tamaduni zetu.

## 4.5 Hitimisho

Katika sura hii uhusika simulizi umeibuliwa na mtunzi kwa kuwasawiri wahusika tofauti wakisimulia yale anayotaka wasomaji wajue na kufanya. Uhusika umeibuliwa kwa njia ya majibizano kati ya wahusika kisha mwisho wanafikia suluhisho. Kupitia usimulizi, tofautiza kitabia na mienendo inabainika kati yao. Kudhihirika huku kwa wahusika ndilo lengo kuu la uchunguzi huu. Kutokana na mifano hii ni bayana kwamba dhana ya usimulizi imeweza kuibua uhusika kwa njia mbalimbali na hivyo kudhihirisha kuwa uhusika unaweza tu kujitokeza kupitia usimulizi wa yale yanayonenwa ama yanayotokana na wahusika wanaposimulia matukio fulani katika mahusiano na mitagusano kati yao.

# SURA YA TANO

# AINA ZA UHUSIKA NA TASWIRA INAVYOIBUA UHUSIKA NAFSI

## 5.1Utangulizi

Sura hii imechambua na kudadavua vipengele mbalimbali vinavyoibua uhusika katika ushairi wa Kiswahili. Lengo la uchanganuzi huu ni kuweka bayana uwepo wa uhusika katika ushairi wa Kiswahili. Sura hii imegawanywa katika sehemu tatu. Kwanza uhusika nafsi unavyoibua uhusika katika ushairi, pili, ujenzi wa aina za uhusika katika ushairi kupitia taswira na tatu,lugha inavyoibua taswira ya wahusika katika ushairi wa Kiswahili.

## 5.1 Uhusika Nafsi Unavyoibua Uhusika Katika Ushairi

Katika sehemu hii utafiti umeshughulikia madhumuni ya tatu ambayo ni kubainisha aina za uhusika katika ushairi wa Kiswahili hivyobasi kueleza jinsi uhusika katika ushairi wa Kiswahili unavyoainishwa. Katika usimulizi wa nafsi mtunzi mwenyewe huwa anaongea na nafsi yake. Inaweza kuwa ni kwa madhumuni ya kuuasa moyo wake, kujifariji ama kujipa imani katika kutenda jambo.

### 5.1.1 Uhusika wa Nafsi Unavyoibua Uhusika Katika *Malenga wa Vumba*

Mtunzi amebainisha uhusika wa nafsi-pekee kupitia usimulizi. Katika ukurasa wa 44 ametunga shairi la beti kumi alilolipa anwani ‘Narudia nitokako’. Katika shairi hili mshairi amegusia mazingira wanamoishi binadamu hasa ya watu wa pwani. Ametunga juu ya kilio cha mfanyikazi

wa nyumbani, Kazungu, aliyeamua kurudi kwao maana kazi ni ngumu na mshahara wa shilingi hamsini kwa mwezi ni kidogo na haumtoshi.

Mfano 1. Kazungu yamenichosha, leo nayasimulia,
Hayano ya kutaabisha, kulla kiyafikiria,
Ndugu zangu nawapasha, mpate nihurumia, (ubeti 1)
Nishabadilisha nia, narudia nitokako.

Katika shairi hili mtunzi amewapa wasomaji wake mwongozo mzuri wa kuzingatia kwa huruma, hali ya wenzetu wanaotufanyia kazi. Mtunzi kupitia usimulizi ameonyesha waziwazi jinsi mtu ambaye ni tajiri mbaya na asiyekuwa na huruma anavyomtesa mfanyikazi wake kwa kumpa kazi hii na ile bila ya kumpa nafasi ya kupumzika; hivyo Kazungu hulia na kulalamika. Mtu mmoja analilia nafsi yake kutokana na madhila anayokumbana nayo. Kupitia usimulizi wa mjakazihuyu uhusika nafsi unadhihirika katika ubeti ufuatao:

Mfano 2. Muda kirudi nyumbani, huwa hali taabani,
Mama bado kitandani, ajipinda kwa makini,
Na jua li upenuni, lachoma pasi imani, (ubeti 8)
Dhiki hino ni ya nini, nisorudi nitokako?

Katika ubeti wa tano usimulizi wa mtunzi unaibua mhusika kwa jina Kazungu akisikitikia hali yake ya udhaifu na unyonge inayosababishwa na dhuluma kutoka kwa tajiri.

Mfano 3. Shati langu ndio mto, nalivaa kwa ghadhiba,
Kisha nichochee moto, nipike chai ya baba,
Chai mbali ya watoto, nayo nipike yashiba, (ubeti 5)
Nauasi mkataba, nirudie nitokako.

Uhusika wa nafsi-uwili unaibuliwa na mtunzi katika baadhi ya mashairi kupitia usimulizi wa wahusika mbalimbali. Katika uhusika wa aina hii mshairi huchukua nafasi ya mhusika mmoja akijibizana na mhusika mwingine. Au pengine panaweza kuwa na watu zaidi ya mmoja katika upande mmoja na upande mwingine hali kadhalika. Mradi panakuwa na pande mbili

zinazojibizana. Uhusika huu hudhihirika zaidi aghalabu katika ngonjera na malumbano. Makundi yanayohusika katika ngonjera hubishana kuhusu jambo fulani. Ngonjera ni shairi ambalo pande mbili au zaidi zina misimamo tofauti kuhusu jambo. Lengo lao huwa ni kutoa misimamo yao hadharani, kupima ubishi wa kila mmoja na hivyo kupata msimamo mmoja kwa pande hizo zote. Katika shairi 'Ufunguo wa maisha' kwenye ukurasa wa 41, mshairi ametumia uhusika huu kisha msimamo unaokubalika na wahusika wote unapatikana. Kuna majibizano baina ya wahusika wawili ambao ni mtoto na baba. Mtoto hafahamu umuhimu wa elimu hivyo basi haoni haja ya kusoma ama kwenda shule. Katika ubeti wa sita mtoto anasimulia ifuatavyo:

Mfano 1.
Nauza pasi janaa, naomba tena jawabu,
Kichwani haijakaa, elimu ilo wajibu,
Ni yoyote ya kufaa, u sharuti Kiarabu?
Kwani hicho Kiarabu, chuoni kina vikoto!

Wahusika hawa wanapambanua misimamo yao. Mtoto haoni elimu kama kitu cha muhimu kwa sababu huko shuleni wanafunzwa Kiarabu kwa kupigwa viboko. Kila mmoja anatoa sababu zake za kuchukua msimamo wake. Msimamo wa baba ni kwamba hakuna kilicho bora na chenye manufaa kama elimu. Katika ubeti wa kwanza anasema:

Mwanangu njoo karibu, nikupe ya manufaa,
Uyajue ya wajibu, uepukwe na balaa,
Usije kupata tabu, dunia ina hadaa,
Katika ya manufaa, mojawapo ni elimu.

Baba anampa nasaha mtoto anaposema asisahau mambo mawili yaliyo muhimu ajaliwapo kupata watoto. Mambo haya ni elimu na mafunzo ya adabu, kwani elimu bila ya adabu ni kama mtu aliyevaa tai huku akiwa yu uchi! Baba na mtoto wanakubaliana mtoto anakubali elimu ni muhimu. Hivyo basi anamtakia babake mema kutoka kwa Muumba kwa kumpa mawaidha yaliyo mazuri katika maisha yake. Mtoto anasimulia katika ubeti wa 10 ifuatavyo:

Tuzo njema ja ridhaa, nazikubali sababu,
Muhali kuikataa, zawadi yako ratibu,
Manenoyo yatakaa, kesho ni kwako thawabu,
Ujinga jama adhabu, elimu ndiyo shifaa.

Katika shairi hili mtunzi ameibua uhusika wa nafsi-uwili kuwasilisha ujumbe. Kuna nafsi neni mbili zinazowasiliana. Mshairi anatumia viambishi ‘ni’ na ‘u’ katika neno **ni**kupe na **u**yajue mtawalia kama viwakilishi vya nafsi hizo. Kiambishi ‘ni’ katika neno **ni**kupe kinamrejelea mzazi ilhali kiwakilishi ‘u’ katika maneno **u**yajue na usije yanamrejelea mtoto. Kwa kusawiri nafsi mbili zikisimulia mtunzi ameibua uhusika hivyo basi kuthibitisha uwepo wa uhusika katika ushairi wa Kiswahili. Mtoto anaridhika na maelezo ya mzazi katika ubeti wa kumi anapoeleza katika mshororo wa pili ubeti wa kumi kwamba ameikubali zawadi yake. Hapa zawadi ikiwa ni ule wosia anaopewa na baba mzazi. Hivyo basi kupitia usimulizi mtunzi ameibua uhusika wa nafsi-uwili na kudhihirisha uwepo wa uhusika katika ushairi.

Uhusika wa nafsi-wingi unaibua wahusika kupitia usimulizi katika mashairi kadha. Katika uhusika huu mshairi huzungumza kwa niaba ya kundi fulani la watu ambalo yeye ni mmoja wao. Mtunzi anatumia nafsi ya kwanza wingi na huzungumzia jambo linalomhusu yeye na hao ambao yeye ni mmoja wao. Mshairi ametunga mashairi kadha yaliyo na uhusika wa aina hii. Uhusika huu unapatikana katika shairi ‘Uhaba wa kazi’ lililo katika ukurasa wa 42. Mshairi amechukua nafasi ya msemaji wa wanawake. Hivyo basi yeye ni mhusika akizungumza kwa niaba ya kina mama. Madhumuni ya shairi hili ni kuwapa mwamko kina mama. Mtunzi anapinga ile dhana ya babu zetu kuwa mke makazi yake ni jikoni au nyumbani kumhudumia mume. hii ni dhana iliyopitwa na wakati. Mtunzi amewasawiri wanawake kuonekana kama watu waliozinduka na wanaojua haki zao. Mtunzi anajitokeza katika nafsi ya wingi katika ubeti ufuatao:

Mfano 1.     Baba mbele mama nyuma, yamekuwa simulizi,
Muradi sote twasoma, soteni tuwe walezi,
Wake haturudi nyuma, tunataka mapinduzi,     (ubeti 15)
Maisha ya siku hizi, watu ni bega kwa bega.

Katika mshororo wa tatu anasema :

Wake haturudi nyuma, tunataka mapinduzi

Mtunzi ni mwanamke akizungumza kwa niaba ya kina mama au wanawake wengi ambao wamejitokeza kuleta mapinduzi kwa vyovyote. Kinachodhihirika katika shairi hili ni kwamba wanawake wamekataa ile dhana ya kuwa wao ni watu dhaifu. Jamii isidhani kuwa wanawake ni watu duni. Wanawake wana uwezo wa kutenda kama wanavyotenda wanaume katika nyanja zote za maisha. Ndiposa kwenye mshororo wa mwisho ubeti wa kumi na tanomshairi anasema,

Maisha ya siku hizi, watu ni bega kwa bega.

Uhusika wa nafsi wingi unadhihirika katika ukwapi wa mshororo huu anapotaja 'watu' kujirejelea 'yeye mwenyewe na wenzake' hivyo dhana ya wingi kudhihirika.

Uhusika wa nafsi-kikundi unadhihrika katika shairi 'Bidhaa zakosa soko' lililo katika ukurasa wa 30. Mshairi anasimulia kuhusu ukosefu wa bidhaa sokoni. Nafsi neni ni wakulima hivyo basi dhana ya wingi inaibua uhusika wa nafsi - kikundi. Katika utungo huu msimulizi ni mmoja wa washiriki wanaolalamika kuhusu bidhaa zao kukosa soko. Kuna matumizi ya viambishi viwakilishi vya nafsi ya wingi kama vile 'tu' kinachorejelea wingi katika neno '**tu**liyozaa' kwenye mshororo wa kwanza na 'za**tu**pa misukosuko' katika mshororo wa mwisho. Katika shairi hili mshairi amechukua nafasi ya wakulima hivyo basi usimulizi wake ni wakulima walio wengi wakilalamika kuhusu bidhaa kukosa sokoni. Katika ubeti wa pili anasema :

Mfano 1. Mazao tuliyozaa, mema yenye nang'aniko,
Yavutia matufaa, maembe na matomoko,
Maghalani yamejaa, tamaa tembe haiko, (ubeti 2)
Zatupa misukosuko, bidhaa kukosa soko.

Usimulizi huu unadhihirisha uhusika katika ushairi wa Kiswahili hivi kwamba tunawaona wahusika katika mazingira yao halisi wakiteta kuhusu ukosefu wa bidhaa sokoni.

Uhusika wa nafsi-umoja hubainika pale ambapo mambo ayasemayo mshairi huwa yanamwelekea mhusika mmoja tu. Mambo haya yanaweza kuwa maonyo, maelekezo, mawaidha , au pengine yanaweza kuwa ni sifa za huyo mtu. Katika *Malenga wa Vumba* uhusika huu umetumika katika utungo 'Ishi tashufu ghulamu' katika ukurasa wa 40. Mshairi anamuonya kijana mwenye dharau kwa watu wa umri mkubwa. Kijana huyu ana majivuno kwa kufikiria kwamba yuko sawa kwa ajili ya madaraka au mali aliyo nayo. Mshairi anasimulia katika ubeti wa kwanza ifuatavyo:

Mfano 1. Watupita kwatukwatu, mijiatu kuiliza,
Na kuwadharau watu, kujiona wapendeza,
Vyaja kutoka viatu, urudi hali ya kwanza,
Dunia yazongomeza, ishi tashufu ghulamu.

Mshairi kupitia uhusika wa nafsi-umoja anatoa ujumbe wa maonyo kwa kijana. Hii inadhihirisha usawiri wa mhusika mwenye tajriba ya maisha kinyume cha kijana ambaye hajayaona mengi ya dunia. Katika shairi hili ni nafsi moja inayozungumza. Huu ni uzungumzi nafsi lakini ulioelekezewa wahusika vijana. Mhusika huyu ananena na nafsi yake kutokana na tabia ya kiburi walio nayo vijana ambao wamebahatika katika maisha kwa kuwa wana uwezo wa kuvaa viatu. Viatu ni kihusika kinachoashiria utajiri ama neema. Mhusika huyu anamtahadharisha kijana kwamba utafika wakati ambapo viatu vinavyomfanya kuringa vitakuja kumtoka na abaki miguu

mitupu. Kutoka kwa viatu hapa ni ishara ya hali kubadilika kutoka katika hali ya utajiri na kuishia kuwa masikini. Katika ubeti wa sita mshairi anatoa tahadhari anaposema dunia siyo ya kuchezea na iwapo hatasikiliza waadhi dunia itamwangamiza kwa kusimulia hivi:

Yaweza kakupa tabu, na kisha ikakukuza,
Ukawa mustaarabu, au ikakuchakaza,
Kiandama matulubu, juwa itakupoteza,
Dunia huangamiza, ishi tashufu ghulamu.

Katika shairi hili mhusika anatoa maonyo kwa kijana asije akafuata matakwa yake pasipo kujua yanamwelekeza wapi. Kuna uwezekano wa mhusika kufuata matilaba yake ambayo yanaweza kumfikisha pabaya. Kwa kuwa mhusika huyu ameishi kwa miaka mingi na ameshuhudia mengi anayo tajiriba ya maisha hivyo anawaonya vijana ambao wanakua. Uhusika unaoibuliwa katika shairi hili unadhihirisha uwepo wa uhusika katika ushairi wa Kiswahili.

### 5.1.2 Uhusika wa Nafsi Unavyoibua Uhusika Katika Diwani ya *Kichomi*

Kezilahabi (1974) kupitia usimulizi anaibua uhusika wa Nafsi-Pekee katika shairi 'Nimechoka'ukurasa wa 34 na shairi 'Dhamiri Yangu' katika Ukurasa wa 45. Katika shairi 'Nimechoka' msimulizi ambaye ndiye nafsi inayorejelewa analilia nafsi yake. Uhusika huu unadhihirisha mhusika aliye katika kifungo na hawezi kujinasua. Japo kuna wanadamu wenye huruma wanaoweza kumuokoa hawafanyi hivyo ila wanainamisha vichwa vyao chini. Katika ubeti wa tatu mtunzi anasimulia hivi:

Mfano 1. Mikono inaniuma, na waya imekwishanikata vidole.
Damu imetirirka hadi kwapani; kujipangusa siwezi.
Nimechoka. Kadiri niendeleavyo kuning'inia, ndivyo
Sura yangu ionyeshavyo vizuri alama za uchovu.
Ninatazama huku na huko kuwatafuta wenye huruma,
Lakini wanadamu wote wazima wanainamisha vichwa
Chini kama kwamba hawanijui;hata jamaa zangu!

Katika ubeti huu mtunzi ametumia uzungumzi nafsi kuibua vihusika vingine. Mtunzi anasimulia kuhusu waya. Kuna uwezekano kwamba waya huu umetumiwa kumfunga mikono. Waya ni kihusika ambacho kimetumiwa kumthibiti asiweze kuponyoka. Wahusika wengine ambao ni jamaa zake na wale wanaomjua wamemsaliti, hawamwonei huruma japo wanashuhudia masaibu anayoyapitia.

Mfano 1. Katika ubeti wa nane anasimulia kwa kusema:

Ninaendelea kuning'inia. Nimechoka. Mikono
Inaniuma; hatari ya vitimbo.Vinacheka. Wanasali
Sasa wanaimba.Sitaki nyimbo zao; maana
Mimi bado nimening,inia na vitimbo having'oki.

Lakini polepole ninaanza kutabasamu.
Sijafika hatua ya kucheka; maana nimechoka,
Kichomi kimenipata na sijaondoka.

Kati ya vitimbo, vichwa vyeupe vinazuka ardhini.
Ukweli wa maisha unakuwa kama ndoto ya uwongo.
Kichwa kimoja kinasema kwa sauti "Mnaliona Hilo!"
Halafu vichwa vyote vyeupe vinacheka. Ninashangaa.
Ninashangaa zaidi kusikia sauti ya baba
Ikicheka miongoni mwa vichwa hivyo vyeupe.
Siyaamini macho, siyaamini masikio, sikiamini kichwa.

Mshairi ametumia usimulizi kuibua uhusika wa nafsi-umoja. Nafsi-neni katika shairi hili ni mtu anayetatizika kwa ajili ya upweke. Ni mtu anayetafuta mwokozi kutokana na shida na hali ya maisha lakini hapati usaidizi. Msimulizi ametumia vihusika kama vile vitimbo ambavyo having'oki, vinacheka huku wakisali kuwasilisha ujumbe. Katika shairi hili mtunzi ametumia usimulizi kusawiri mazingira ya mfungwa. Mtu huyu yuko kifungoni kutokana na dhuluma za wanadamu wenzake. Taswira tunayoipata hapa ni ile ya mtu kutendewa unyama na wale anaodhani wana hekima kama vile watu walio na mvi yaani wazee. Inapokuwa kwamba wao wanacheka tu badala ya kumsaidia anashangaa. Dhamira ya mtunzi ni kutujuza ukweli wa maisha na ameonyesha kupitia uhusika huukwamba hiindiyo hali halisi. Kupitia uhusika huu

mshairi anadhihirisha kuwa kuna watu wasio na huruma hata kidogo. Japo mja atajikuta katika mateso yasiyoelezeka kwao hayatawatonesha kidonda, ila wataendelea na shughuli zao kama kwamba hakuna kinachoendelea.

Uhusika wa nafsi-uwili umeibuliwa katika sehemu ya pili ya shairi ‘Dakika 15 za Uzalendo’. Katika shairi hili kuna nafsi mbili zinazosimulia. Mtunzi anachukua nafasi ya Kijana kwa upande mmoja na kwa upande mwingine anachukua nafasi ya Mzee kuwepo kwa majibizano kati ya mhusika Kijana na Mzee kunalifanya shairi hili kuchukua muundo wangonjera. Kupitia usimulizi tunapata taswira ya nafsi mbili. Nafsi ya kwanza ni ile ya watu wasiokuwa na ufahamu wa Azimio la Arusha kama vile Mzee. Mhusika huyu anawakilisha wananchi katika nchi ya Tanzania ambao hawakufahamu maana ya Azimio la Arusha. Nafsi ya pili ni ile ya Kijana ambaye anaunga mkono mabadiliko yaliyotokana na Azimio la Arusha. Katika ubeti wa tano japo kuna nafsi kadha ambazo zinabainika utafiti ulijikita katika nafsi mbili ambazo ni Kijanana Mzee.

Mfano 1. Msimulizi anasema:

Kalitangaza Arusha, Nyerere Mheshimiwa,
Wote kupe kuwarusha, wawe kama wafiwa,
Wasije Taifa pofusha, uvivu kuachilia,
Tukala cha kupimiwa, hatima chakula kwisha.

Katika ubeti huu usimulizi wa nafsi unaibuka pale ambapo mhusika anaeleza kuhusu hali ilivyokuwa hapo awali. Uhusika simulizi unadhihirika mtunzi anapochukua nafasi ya mhusika hivyo basi uhusika nafsi unabainika mhusika anaposimulia matukio yaliyotokana na mabadiliko ya kisiasa katika dola ya Tanzania. Aidha uhusika wa nafsi-umoja unabainika mtunzi anapomrejelea mhusika Nyerere. Anarejelea rais wa kwanza wa Tanzania. Uhusika wa nafsi

wingi unadhihirika mtunzi anapowarejelea wakoloni kwa kuwafananisha na kupe. Anawaita kupe kutokana na tabia yao ya kufaidi kutoka kwa jasho la wenzao. Anasema;

Wote kupe kuwarusha, wawe kama wafiwa,
Wasije Taifa pofusha, uvivu kuachilia,

na anapowarejelea wazalendo yeye akiwemo anaposema;

Tukala cha kupimiwa, hatima chakula kwisha.

Aidha kihusika taifa kimehusishwa kwa kuwa ni eneo lenye mipaka ambamo wananchi huishi. Hivyo basi anaponadi kuondolewa kupe anawatia shime wananchi ili waweze kufanya kazi kwa bidii taifa lisije kuathirika kutokana na ukosefu wa chakula. Mshairi ameibua wahusika tajiri waliokasirishwa na mpango wa kutaifisha mali yao. Matajiri walinyang'anywa mali yao ikafanywa kuwa mali ya taifa. Kwao hii ilikuwa dhuluma na ukatili uliokithiri kwa sababu walifanya kazi kwa bidii ndipo wakaweza kupata mali hiyo. Katika ubeti wa ishirini na tatu Tajiri anasema hivi:

Wewe zalendo sikia, niliyo nayo moyoni,
Nyumba nimesumbukia, haikutoka hewani
Sementi mejinunulia, maji katoa tangini,
Nayo TANU yabwakia, jengo kuwa mikononi!

Mshairi ametumia usimulizi kuibua vihusika kutilia mkazo malalamishi ya mabwanyenye hawa. Ametumia vihusika mathalan nyumba, maji na chama cha T.A.N.U. Mhusika huyu mkwasi anasimulia vitu alivyomiliki kwa kueleza kwamba hakuvipata kwa urahisi. Amejenga nyumba ya aushi kwa kutumia saruji. Ametaja hewa kutoa rai kwamba japo kuna vitu vinavyoanguka kutoka hewani haikuwa hivyo kuhusu nyumba yake. Alihifadhi maji tangini kwa madhumuni ya ujenzi. Aligharamia tangi wakati wa kulijenga ilikuhifadhi maji yasipotee wakati wa ujenzi wa nyumba yake. Mshairi anasimulia kuhusu chamacha siasa kiitwacho T.A.N.U. Hiki ndicho chamakilichokuwa kikitawala. Mshairi ametumia usimulizi kuonyesha namna chama hiki

kiliendeleza dhuluma dhidi ya wazalendo kwakuyatwaa majengo na mali yao. Chama hiki kimehuishwa hivi kwamba ni chama dhalimu kutokana na dhuluma zake dhidi ya wazalendo. Katika ubeti wa ishirini na sita tajiri anakubali shingo upande mali yake kutwaliwa kwa sababu hana hiari. Mshairi anasawiri mhusika ambaye hana hiariila kutii maazimio yaliyofikiwa kufuatia Azimio La Arusha.

Mshairi ametumia usimulizi kuibua mhusika mwenye sifa ya uzalendo. Maelezo ya Mzalendo yanamshtuwa anapobadili nia kwa kukubali wito. Japo hapo awali aliikejeli serikali hana budi kuafikiana na mapendekezo yaliyoafikiwa. Ni dhahiri kutokana na masimulizi ya mzalendo kuwa hana budi kuzingatia methali isemayo, mkono usioweza kuukata ubusu. Huwezi kupigana na mamlaka. Hali hii inatupa mwanga wa uwepo wa uhusika katika hali mbalimbali katika ushairi.

Lo! TANU uliitukana, ukasema yabwakia!
Kajivutia ubwana, na pesa ukasifia,
Sasa waafikiana, na wito kuitikia,
Mi naona wajibana, mkaa wajipalia,
TANU yetu yenye nia, huwezi nayo lumbana.

Uhusika wa nafsi-wingi umeibuliwa katika shairi ‘Vipanya’ kwenye ukurasa 49. Katika shairi hili mtunzi anazungumza kwa niaba ya wananchi wenzake. Katika mishororo miwili ya ubeti wa kwanza anasema:

Mfano 1. Nchi yetu yaja kwa shairi, kwa sauti ikilia:
Jamani nyumba yetu imeingiliwa
Nipeni viboko nivichape
Vipanya vilamba vikombe.

Ametumia vihusika nchi, nyumba na vipanya. Kihusika nchi kimehuishwa hivyo basi kinalalamika kwa niaba ya wanaoishi ndanimwe. Mshairi anataja nyumba inayowasitiri

kuvamiwa na vipanya anazungumza kwa niaba ya wenzake wanoishi kwenye nyumba hiyo. Kihusika nyumba kinarejelea nchi. Kihusika nchi kinawakilisha mwananchi ambaye anatanabahi kabla wananchi wenzake kuvamiwa na vipanya. Vipanya ni wanyama waharibifu sana. Vipanya hapa ni vinyama vinavyoharibu mazingira au uchumi wa nchi. Panapotokea hali kama hii lazima tahadhari ichukuliwe kuviangamiza vipanya hivi kabla havijazua balaa kubwa. Kuviangamiza vipanya hivi utumizi wa mbinu mbalimbali unaweza kutumika. Kiboko ndicho kinatumiwa kuviondoa hivi vipanya. Kiboko ni kihusika ambacho kinatumika kuleta amani. Hivyo basi nchi ni chombo ambacho kinatumiwa na wahusika wengine kupitisha ujumbe. Mshairi ameibua uhusika wanafsi-wingi anapozungumza kwa niaba ya wananchi ambao hawawezi kuzungumza. Tujuavyo nchi haiwezi kulia na kwamba tunapozungumza kuhusu nchi tunamaanisha wananchi wanaoishi katika nchi hiyo. Vipanya katika shairi hili ni wahusika wasiokuwa na nia njema ila kuharibu mazuri yaliyomo nchini.

Uhusika wa nafsi-kikundi hubainika wakati mhusika huwa ni kikundi cha watu. Yaani mshairi huwa anazungumza na kikundi cha watu. Mshairi hutumia vivumishi vya pekee vya wingi kurejelea kikundi cha watu.Katika shairi ‘Dakika 15 za Uzalendo’ mshairi anarejelea wahusika ambao wanawakandamiza kwa kuwaita kupe baada ya kutangazwa kwa Azimio la Arusha. Mshairi anasema;

Mfano 1.

Kalitangaza Arusha, Nyerere Mheshimiwa,
Wote kupe kuwarusha, wawe kama wafiwa,
Wasije Taifa pofusha, uvivu kuachilia,
Tukala cha Kupimiwa, hatima chakula kwisha

Mshairi anawarejelea wahusika hawa kwa kutumia kiambishi cha ngeli cha wingi ‘wa’ katika maneno kama vile ku**wa**rusha, **wa**sije, **wa**we na **wa**fiwa. Kikundi hiki amekiita kupe. Kupe ni wahusika wanyonyaji.

Uhusika wa nafsi-umoja umeibuliwa katika shairi ‘Nenda Ukanywe!’ Uhusika huu umeibua mhusika anayewazia hali yake. Mhusika anatenda yale anayoyatenda kama vile kukimbia na kuwashambulia watu. Anagonga kuta za chuma kutokana na mafunza kumwingia bongoni. Usimulizi huu umo katika ubeti wa kwanza. Mafunza kumwingia bongoni ni kupagawa hali inayomfanya kutenda mambo yasiyoeleweka.

Mfano 1. Mafunza wameniingia
Nao wakati wa joto wachezapo mchezo
Wao ndani ya nyumba hii ya mawazo
Hunifanya kama mwehu
Nikimbie na kuwashambulia watu hao
Na kama nguruwe mwitu
Kugonga kuta hizo za chuma
Ziwafungazo wanadamu

Mshairi anajirejelea anapotumia kiambishi ‘ni’ katika neno wame**ni**ingia, Hu**ni**fanya na **Ni**kimbie. Kwa kutumia viambishi hivi anaibua uhusika wa nafsi umoja hivyo basi anakuwa mhusika katika huu usimulizi. Mtunzi anatoa mawaidha na maonyo kwa wahusika wengine kwamba hapana haja ya kuingiwa na kiwewe kwa yale tunayokumbana nayo kila siku. Mtunzi kupitia uhusika huu anajaribu kutoa hoja kwamba yote yanayotendekaduniani ni ya kawaida isipokuwa tu kifo. Katika ule ubeti wa mwisho anahoji iwapo kuna yule aliyekufa na akarudi.

“Nenda ukanywe!”
Kwani
Nani alikula asile tena!
Nani aliruka hewani asitue?
Lakini nani alikufa akarudi?

Mshairi anaibua uhusika wa nafsi-umoja anaporejelea nafsi yake. Anawaonya wanajamii wanaofikiria kwamba wataishi tu na hawatakufa. Anatuma mhusika mtu kwa kusema kuwa hakuna siku ambayo mtu atawacha kula, daima awapo mzima mtu hula. Chakula ni kihusika kinachomwezesha binadamu kuishi. Bila chakula binadamu hawezi kuwa hai. Mshairi anasimulia kuhusu mtu aliyeruka hewani.

Mtunzi ameibua vihusika vingine katika shairi hili ambavyo ni hewa, ardhi na kifo. Hewa imetumiwa kama kihusika ambacho kinaweza kumsaidia mwanadamu katika usafiri akitumia vyombo vinavyopaa angani. Japo ataruka hewani kwa ndege ama chombo kingine hawezi kukaa huko, lazima atarudi ardhini. Aidha hewa humsitiri mwanadamu na kumfanya aweze kuishi. Japo hewa ina manufaa mbalimbali kwa mwanadamu haitakusaidia kwa mambo yote. Mtunzi anasimulia kihusika ardhi. Ardhini ndipo mahali ambapo viumbe hai hupatikana. Ardhi ni kihusika kinachomwezesha binadamu kuishi na kutekeleza majukumu yake akiwa hai na hakuna mahali pengine popote. Anaposimulia kihusika kifo anaeleza ndicho kihusika pekee ambacho kimemshinda mtu kuthibiti. Hakuna hata mtu mmoja aliyekufa na kurudi kusimulia aliyoyaona. Kifo ni kihusika kisichoweza kuthibitiwa na binadamu. Hivyo basi kupitia usimulizi uhusika wa nafsi-umoja unabainisha kwamba hakuna haja ya kujitia wazimu kwa yale yanayotutendekea. Uhusika unaibuliwa kutokana na masimulizi, hivyo basi kudhihirisha uwepo wa uhusika katika ushairi wa kiswahili.

Uhusika wa nafsi-kikundi umeibuliwa katika shairi ‘Kumbe’ lililo kwenye ukurasa wa 37.

Mfano 1. Kwamba elimu waliotupa wale wakoloni
Kama suruali ilyopasuka matakoni,
Kweli kama ng’ombe wailostushwa
Na siafu, tumetambua dhahiri.

Katika ubeti wa kwanza wa shairi hili msimulizi ni mmoja wa wahusika waliodhulumiwa. Anasimulia hali yao akijilaumu jinsi walivyokuwa wajinga na hawakujua walichokuwa wakifanyiwa na wakoloni. Amegundua ilikuwa ni fedheha lakini hawatakata tamaa ila atavumilia kama anavyosema kwenye ubeti wa mwisho kuwa,

Aaa! kumbe ndoo maana wazee
Tulipokuwa tukitembea na vitabu
Mabarabarani kwa huruma walitucheka
Lo! Lo! Lo! Tulikuwa tukichezewa!
Lo! Nini basi tutafanya tupate
Kurudisha heshima yetu ya utu
Tuliyopoteza kwa kuvaa kitu
Wao walichotupa jalalani?
Sikilizeni. Simba aliyeumizwa,
Bila haya alijikokota kwa unyonge
Mpaka nyumbani, vidonda vikalambwa
Vikapona kwa mate ya nyumbani.

Nafsi-neni katika shairi hili ni mzee. Anazungumza kwa niaba ya kikundi cha wazee wenzake. Anatoa maelezo haya katika mishororo mitatu ya kwanza;

Aaa! kumbe ndoo
Tulipokuwa tukitembea na vitabu
Mabarabarani kwa huruma walitucheka

Katika ubeti wa mwisho anatoa nasaha kwa niaba ya wenzake akijifananisha na simba aliyeumizwa. Anasimulia hivi:

Sikilizeni. Simba aliyeumizwa,
Bila haya alijikokota kwa unyonge
Mpaka nyumbani, vidonda vikalambwa
Vikapona kwa mate ya nyumbani.

Ametumia istiara kudhihirisha hali ambapo japo waweza kuwa na nguvu na uwezo wa kukabiliana na hali ngumu huenda ukajeruhiwa kwa kukosa zana bora za kukabiliana na adui.

Anatoa nasaha kuwa jambo kama hili halistahili kukufanya kuona haya badala yake utajikokota hadi kwa jamii yako ambao watakuonea huruma na kukutibu.

Uhusika wa nafsi kupitia mifano iliyotolewa katika baadhi ya mashairi yaliyotumiwa umetambulika. Aidha kupitia usimulizi katika matapo matano ya uhusika usawiri wa wahusika umeweza kudhihirika. Hii ni ithibati tosha kwamba uhusika upo katika ushairi wa Kiswahili na unapaswa kushughulikiwa kama unavyoshughulikiwa katika tanzu zingine za fasihi na kuhakikiwa kama kipengele cha fani.

Mbinu mbalimbali za usimulizi zimewezesha kuibuliwa kwa uhusika katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*, diwani ya *Malenga wa Vumba* na *Kichomi* hivyo basi kudhihirisha ufaafu wa nadharia ya usimulizi kwa mujibu wa Manfred (2005). Mihimili mikuu ya nadharia hii ambayo ni dhana ya uhusika na usimulizi ndiyo kiini cha uchunguzi katika utafiti huu. Mihimili hii imewezesha kuelewa vihusika, tabia na mienendo ya wahusika, wasifu wao, hisia na fikra zao, mahusiano yao, mazingira yao na falsafa zao. Sifa na wasifu wa mhusika hubainika kutokana na matendo yake au maelezo yanayotolewa na mwandishi mwenyewe au mhusika mwingine.

## 5.2 Ujenzi wa Uhusika KupitiaTaswira Katika  Ushairi wa Kiswahili

Wamitila (2003) anasema taswira ni dhana inayotumiwa kuelezea neno, kirai au maelezo ambayo yanaunda picha fulani katika akili ya msomaji. Taswira zinaweza kuwa za kimaelezo yaani maelezo fulani yakaunda picha au za ki-ishara zinazounda picha ambayo inaashiria jambo fulani au imeficha ujumbe fulani. Taswira zinaweza kuundwa kwa matumizi ya tamathali za usemi hasa tashbihi na sitiari. Ingawa taswira nyingi ni za uoni yaani, zinazomchochea msomaji

kuona picha fulani inawezekana pakawa na taswira za aina nyingine. Ametaja aina kadha za taswira lakini kwa madhumuni ya utafiti huu siyo aina zote alizotaja zitafaa. Ametaja taswira za harufu ambazo humletea msomaji picha zinazohusiana na harufu. Aidha ametaja taswira za kimaelezo ambazo ni taswira zinazojengwa kutokana na maelezo ya mwandishi au lugha anayoitumia mwandishi. Mwandishi anatumia lugha ambayo ina uwezo wa kujenga picha fulani katika akili ya msomaji wake. Taswira zingine ambazo ametaja ni taswira za kiishara, taswira za joto, taswira za mguso taswira za mwendo, taswira za mwonjo na taswira za usikivu.

Picha husaidia sana kuvuta hisi na kuleta mguso wa hali ya juu kwa upande wa mhusika anayefikiwa na ujumbe. Mhusika hapa ni mmoja wa wale waliomo kwenye kazi ya msanii ambalo ni shairi lenyewe. Aidha mhusika anaweza kuwa yule msomaji wa shairi kwani yeye hupata athari fulani kutokana na shairi analosoma. Picha inayorejelewa hapa ni ile ya akilini inayotokana na masimulizi ama maelezo ya msanii. Iwapo ni wahusika katika shairi maelezo ya mhusika mmoja kuhusu mhusika mwingine itambainikia haraka. Maelezo yanaweza kutoa sifa za umbile ama hata matendo na tabia ya mhusika hivyo basi ikawa rahisi kwa huyu mhusika kumweleza kama ni mfupi au mrefu kwa kimo ama ni katili aliyejaa kiburi.

Baada ya wahusika kuumbwa, msomaji anaweza kupata picha ya makundi tofauti ya wahusika kutokana na hadithi katika shairi moja au mashairi mawili. Kuibuka kwa uhusika kupitia picha umeafikia madhumuni ya utafiti ya kutathmini uhusika unavyojitokeza katika ushairi, hivyo basi, kujibu swali kuhusu namna ambavyo uhusika katika ushairi wa Kiswahili hujitokeza. Utungaji wa picha ya mawazo ya watu waliobuniwa kwenye hadithi, kiasi ambacho kwa msomaji

wanaelekea kama ni hai kwenye mipaka ya hadithi hiyo, ndio uumbaji wa wahusika. Hii picha ya mawazo ndiyo inayoibua uhusika ambalo ni swala kuu katika utafiti huu.

Kezilahabi(1974) amezungumza kuhusu maswala mbalimbali ya kijamii, ya kisiasa na ya kisaikolojia ambayo ni ya kawaida katika fasihi ya Kiafrika ya siku hizi, lakini mshairi huyu ni mtunzi wa pekee kwa jinsi yake ya kutumia sitiari na mafumbo. Watafiti wengi wametaja umuhimu wa picha katika tungo za Kezilahabi. Graziell (2004:69) anaeleza kuwa ni sitiari na mafumbo ndiyo yanayofanya mashairi ya Kezilahabi kuwa tofauti. Mlacha (1987) anaona picha kuwa muhimu katika kazi zake kwa kuwa zinasawiri mtindo unaoendeleza muundo wa riwaya zake.

Picha ni muhimu katika ushairi wa Kezilahabi hivi kwamba picha zingine katika kazi zake zina mvuto zaidi. Ametumia viumbe walio hai kama vilendege na wanyama. Katika ushairi wake anaumba wahusika na vihusika kupitia njozi. Njozi za ulimwengu zinazojitokeza katika ushairi wa Kezilahabi zinafanana sana na zile za mtu anayeweweseka akiwa usingizini. Njozi hizi ni kama maonyesho ya fujo yanayotoka ndani na ukengeuko wa binadamu.

### 5.2.1 Taswira ya usikivu

Wamitila (2003) anasema huu ni usemi ambapo msanii anaunda picha ambazo hulenga hisia ya kusikia yaani anajenga picha zinazohusiana na sauti. Katika shairi ‘Wimbo wa Mlevi’ ukurasa 64: Kezilahabi(1974) ametujengea picha kupitia usemi ifuatavyo:

Mfano 1. Kama Mungu angewauliza wanadamu
Wanataka kuwa nani kabla ya kuzaliwa,
Hilo ndilo lingekuwa swali gumu maishani.
Na watu wangeishi kujutia uchaguzi wao. (ubeti 1)
Wote wangetamani kuwa kinyume cha walivyo.
Sijui nani angekuwa nani.

Lakini mimi mlevi ningependa kuwa ye yote
Mradi tu niruhusiwe kunywa pombe yangu
Hapo nyumbani kwa baba Madaka hamjambo! (ubeti 2)
Ni usiku mi napita nakwenda zangu

Mshororo wa kwanza katika ubeti wa kwanza mtunzi ametoa kauli kuwa iwapo Mungu 'angewauliza' wanadamu. Hivi ni kusema kwamba kutokana na yanayosemwa kuna msikilizaji hivyo basi kuibua taswira ya usikivu. Mtunzi anaibua taswira ya usikivu kupitia uzungumzi nafsi wa mlevi anayesikiliza maswali anayouliza Mungu na kuyajibu.

Msomaji anaweza kupata sifa za wahusika mbalimbali mathalan, walevi wakiendelea na shughuli zao katika hali halisi kwa sababu yanayosimuliwa yanahusu watu na vitu vinavyoonekana. Katika shairi hili mtunzi anatupa taswira ya mhusika mlevi mwenye busara kutokana na jinsi anavyojibu maswali. Japo ni mlevi anasema kuwa binadamu wengi wangejutia uchaguzi wao kabla ya kuzaliwa. Katika mshororo wa saba anasema yeye angekuwa yeyote ila tu aruhusiwe kunywa pombe. Jibu hili la mlevi linatupa taswira ya mhusika mwenye kiburi. Ni mtu asiyejali hata kama watu watamdharau kwa kuwa yeye ni mlevi. Taswira ya usikivu inaibua uhusikawa mzungumzaji kutokana na maneno anayoyasema kwa sauti yake ya kilevi hata bila kumuona.

Sauti kama kihusika imetumiwa kuzua hisia fulani. Katika shairi 'Nimechoka' kwenye ukurasa wa 34 mshairi anasema:

Mfano 1. Sauti ya baba inasema kwa msisitizo:
“Najua utafika wakati itakulazimu kudondoka,
Lakini endelea kushikilia hiyo waya (ubeti 4)

Taswira ya usikivu imetumika hapa kudhihirisha hali ya uchovu kutokana na matendo ama mwenendo unaoudhi. Msisitizo huo ni wa kuonya kwa sababu huenda si mara ya kwanza ndiposa sauti inasisitiza.

Ndoto ina maana ya mawasiliano kati ya wakati wa kale na ule wa sasa, pamoja na kuwa kama tamthilia ya maisha halisi; ndoto inaweka jukwaani nyakati na kumbukumbu mbalimbali ambazo nje ya ndoto zingetambuliwa na binadamu kama ishara za fujo. Mtunzi anasikiliza sauti ya babu yake inayotoka ndani yake mtunzi kama tunavyoweza kusoma katika shairi ‘Nimechoka’ ukurasa 34:

Mfano 1. Nilivyofikishwa hapa, na juu kupandishwa.
Na kwa hila gani, au zilipofungwa
Ncha za waya hii ngumu ya maisha, sijui.
Lakini najiona nimening’nia kama ndege
Aliyenaswa na mtego wa mtoto mdogo.
Mimi, lakini, ni mwanadamu na akili zangu
Timamu. Ninaweza kudondoka, kama nikipenda.
Lakini ninaogopa chini yangu naona miti
Iliyochongwa ikifuata usawa wa waya hii,
Ikingoja kwa hamu, kama mshikaki kunichoma,
Kunitoboa na kufurahia kimya kimya
Uzuri wa kupita katika mwili mwororo wa binadamu.
Lazima nishike kwa nguvu nisianguke kama kifurushi
Cha pamba chaa motto mdogo kilichokwisha pimwa
Mikono inaniuma, na waya imekwishanikata vidole.
Damu imetiririka hadi kwapani; kujipangusa siwezi.
Nimechoka. Kadiri niendeleavyo kuning’inia, ndivyo
Sura yangu ionyeshavyo vizuri alama za uchovu.
Ninatazama huku na huko kuwatafuta wenye huruma,
Lakini wanadamu wote wazima wanainamisha vichwa
Chini kama kwamba hawanijui; hata jamaa zangu!

Ninaendelea kuning’inia kama picha iliyotundikwa
Katika shamba la mawele, na mwenye shamba
Huvuta waya kutoka nyumbani, itingishike kuwatisha ndege.
Machozi yananitoka, kuyapanugsa siwezi.
Ninajitahidi kutoa sauti kwa nguvu:
“Jamani e! Nisaidie! Ng’oeni hivyo vitimbo!’’
Lakini wanadamu wameinama. Wanaanza sasa kusali.

Katika kusikiliza sauti ya ndani mtunzi anaibua taswira ya uoni hivyo basi kuibua mhusika aliye taabani akitafuta usaidizi. Mateso anayoyaona yanadhihirika kupitia sauti inayosimulia matukio ya hali anayokumbana nayo katika ulimwengu wa ndoto. Mshororo wa nne ubeti wa kwanza msimulizi anajiona akiwa amening’nia kama ndege. Mshororo wa kwanza ubeti wa pili msimulizi anasema;

Lakini ninaogopa chini yangu naona miti.

Mshororo wa tano ubeti wa tatu anasema;

Ninatazama huku na huko kuwatafuta wenye huruma,

Kisha katika ubeti wa nne mshororo wa tano, sita na saba anasema;

Ninajitahidi kutoa sauti kwa nguvu:
“Jamani e! Nisaidie! Ng’oeni hivyo vitimbo!’’
Lakini wanadamu wameinama. Wanaanza sasa kusali.

## 5.2.2 Taswira ya Mguso

Wamitila (2003) anasema hizi ni taswira ambazo hujenga picha ya kitu thabitiau kitu kinachoweza kugusika. Kugusa ni hali ya kukaribiana hadi kushikana. Kezilahabi (1974) katika shairi ‘Nimechoka’ukurasa wa 34 amehuisha ‘sauti’ kama kihusika kumhimiza mhusika kuendeleakushikilia waya katika mshororo ufuatao. Kuna hali ya mkono kugusana na waya hivyo basi kuibua picha ya mgusano kati ya waya na mkono.

Lakini endelea kushikilia hiyo waya

Kihusika waya ni tabia au mwenendo usiobadilika. Mtunzi ametumia taswira ya mguso kusisitiza kwamba kuna siku ambapo itabidi mhusika kubadilika kwa hiari au pasipo hiari.Waya ni kifaa kisichoweza kukatika bila kutumia nguvu hivyo basi anayeshikilia anahimizwa kuendelea kushikilia kwa sababu hakuna anayeweza kubadilisha hali yake. Taswira ya mguso inaibua uhusika wa mtu mkakamavu au mwenye msimamo thabiti.

Katika shairi 'Wanadamu Tunawajueni' (ukurasa 61) mtunzi ametumia taswira ya mguso kwa namna mbalimbali kuibua uhusika.

Mfano 2. Mimi ni nguo ya ulimwengu
Huvuliwa nikawekwa pembeni
Mimi ni sabuni ya Ulimwengu
Nimepapasa miili ya watu wengi
Mimi ni chakula cha Ulimwengu (ubeti 1)
Nimepapaswa na ndimi nyingi, nimeumwa.
Nimekaa ndani ya matumbo kila aina
Yaliyokwanyuka na pengine nilielea
Mwenye bia pengine hukumbana na tegu.

Mshairi ametumia vihusika nguo, sabuni, ndimi na bia. Katika mshororo wa kwanza anasema:

Mimi ni nguo ya ulimwengu
Huvuliwa nikawekwa pembeni.

Kihusika nguo kimeibuliwa kupitia taswira ya mguso. Nguo inapovaliwa hukaribiana na mwili hivyo basi kugusana. Nguo huvaliwa kisha huvuliwa ikawekwa kando na ingine ikavaliwa. Mtunzi anasimulia kuhusu maisha ulimwenguni, kwamba hufika wakati mhusika mmoja akaondoka kwa kuchoka ama kuaga dunia na mwingine mwenye siha, nguvu na uwezo ama tajiriba inayohitajika kujaza nafasi iliyoachwa. Uhusika umeibuliwa kupitia taswira ya mgusokwa njia ya usimulizi. Nguo huvaliwa na kuvuliwa na viumbe ambao ni watu. Hivyo basi

kwa kurejelea nguo mtunzi anabainisha mabadiliko yanayotokea kwa binadamu wawapo ulimwenguni kama wanavyobadilisha nguo kila mara. Katika mshororo wa tatu anasema :

Mimi ni sabuni ya Ulimwengu
Nimepapasa miili ya watu wengi.

Mtunzi kupitia usimulizi anaibua uhusika kupitia taswira ya mguso anapojifananisha na sabuni. Kama binadamu katika ulimwengu amepitia hali nyingi tofauti kama vile kukwaruza miili tofauti. Mtunzi ametumia taswira ya mguso kuibua sabuni ikigusana na miili ya watu. Sabuni inapotumiwa na watu kupaka miili yao hutoa uchafu na kuinadhifisha. Kwa kutumia taswira ya mguso mtunzi anaibua kihusika. Taswira tunayoipata ni ya hali ambazo wanadamu hupitia wakiwa katika maingiliano yao na watu wa matabaka tofauti kutegemea rangi, kimo na hata kiuchumi. Sabuni hugusana na miili tofauti ya watu.

### 5.2.3 Taswira ya Mwonjo

Wamitila (2003) anasema hizi ni taswira ambazo hulenga kwenye hisia ya kuonja. Hali hii inaweza kupatikana pale ambapo pana maelezo yanayohusiana na chakula. Kezilahabi (1974) katika shairi 'Wanadamu Tunawajueni' (ukurasa 61) kuanzia mshororo wa sita hadi ule wa tisa anasema :

Mfano 1. Mimi ni chakula cha Ulimwengu
Nimepapaswa na ndimi nyingi, nimeumwa.
Nimekaa ndani ya matumbo kila aina
Yaliyokwanyuka na pengine nilielea

Mtunzi anajifananisha na chakula. Chakula hutumiwa na kila kiumbe kilicho hai. Chakula kinaweza kuwa majimaji au kisichokuwa majimaji mathalan sima au wali. Aidha chakula kinaweza kuwa cha kutafunwa au cha kumega kwa meno. Chakula hapa ni hali mbalimbali alizopitia mhusika. Anajilinganisha na chakula pale anaposema amepapaswa na ndimi nyingi,

ameumwa na kukaa ndani ya matumbo ya kila aina.Munzi anaibua taswira ya mguso anaposimulia kuhusu kupapaswa na ndimi. Ili chakula kiweze kuingia tumboni ni lazima ulimi uweze kukaribiana na chakula hicho. Ndimi zimehuishwa kudhihirisha ule mtagusano anaopitia mwanadamu awapo ulimwenguni. Kuumwa anakosema mtunzi kunamaanisha matatizo aliyokumbana nayo. Kifaa chochote kikiumwa hubadilika. Hakiwi jinsi kilivyokuwa katika umbo la awali. Kisha katika mshororo wa tisa anasema :

Mfano 2. Mwenye bia pengine hukumbana na tegu.

Katika mshororo huuanasimulia kuhusu matatizo yanayoweza kumkumba mwanadamu akiwa katika pilkapilka zake duniani. Kuna uwezekano wa kupata minyoo au tegu iwapo atatumia vyakula fuani.Vyakula vingine vinaweza kusababisha ugonjwa wa tumbo. Mtunzi ametumia aina tofauti za taswira kuibua uhusika katika shairi hili. Aidha kupitia usimulizi ameibua taswira hizi kwa sababu ni maelezo yake ndiyo yanatupa hali mbalimbali ambazo mwanadamu anapitia akiwa duniani. Katika mshororo wa mwisho ametaja mwenye bia akimaanisha mtu anayetumia kileo. Hivyo basi kupitia taswira ya mwonjo mtunzi ameibua mhusika anayetumia pombe kama chakula na maafa yanayompata kutokana na kuonja ama kunywa bia.

### 5.3.4 Taswira ya Uoni

Wamitila (2003)anasema kimsingi taswira nyingi ni za kiuoni akimaanisha kuwa ni taswira ambazo humchochea msomaji kuona picha fulani. Katika shairi ‘Kisu Mkononi’ kwenye diwani ya *kichomi* ukuarsa 13 mtunzi anasimulia ifuatavyo:

Mfano 1. Mbele chui mweusi, nyuma mwanga
Nionako kwa huzuni vifurushi maelfu vya dhambi.
Sasa kama Simba-Mtu shauri nimekata.
Ya nyuma sana nisijali, ya mbele sana niyakabili.

Kwa ujasiri na uangalifu nitazunguka (ubeti 2)
Nikifuata kamba kama ng'ombe aliyefungwa,
Kila mpigo wa moyo wangu
Huu mpigo muziki wa maisha.

Mtunzi katika shairi hili ametumia taswira ya uoni kuibua mhusika jasiri ambaye yuko tayari kukabiliana na hatari. Mhusika hana jingine kwa kuwa anapotazama mbele anakokwenda kuna chui ilhali nyuma anakotoka kuna maelfu ya vifurushi vya dhambi. Hana budi kukabiliana na yaliyo mbele yake kwa ujasiri. Katika mshororo wa mwisho mtunzi anaibua mhusika jasiri kupitia taswira ya usikivu kwa kuwa binadamu anaweza kuishi iwapo moyo utaendelea kupiga kama unavyofanya na huo ndio mpigo wa muziki wa maisha.

Kihusika 'maji' kimetumiwa kama kioo kinachotupa mambo mbalimbali ya nafsi iliyobadilika, katika shairi 'Mto wa Haki' ukurasa 17.

Mfano 2. Pole pole alianza kujiona mjinga kwa kuogopa
Maji yaliyokuwa yakimtakasa mwenzake. (ubeti 4)

Alisikia sauti ya haki na usawa wa binadamu:
kwa mda wa dakika moja alielewa ukweli (ubeti 5)
Ambao vitabu vyote vilikuwa vimeshindwa kumweleza.
Alikuwa ameona kivuli chake majini.

Unafanya nini? Sauti iliuliza (ubeti 6)
Hakuweza kujibu: mwili wake ulikuwa umeganda

Nafsi-neni katika shairi hili ni mwanadamu. Anajikuta katika hali ya kutojielewa kutokana na hali fulani anayoishuhudia kwenye kioo. Anayoyaona akifanyiwa mwenzake yanamfanya kuogopa. Ni dhahiri katika ubeti wa tano kuwa mhusika huyu hakuwa akiwatendea wenzake haki. Alikuwa dhalimu na aliendeleza dhuluma kwa waja kama kwamba aliyokuwa akifanya yalikuwa sawa.

Kihusika sauti kinaibua taswira ya usikivu inayomzindua na kumtanabahisha mhusika kuwa aliyokuwa akitenda si haki. Katika ubeti wa kwanza kuna mhusika ambaye anapitia mabadiliko. Si mabadiliko mazuri kwa sababu yanamwogofya hasa anaposhuhudia mwenzake anavyoteseka.

Katika ubeti wa sita mtunzi anaibua kihusika kivuli. Msimulizi anakiona kivuli chake majini. Kivuli hiki ni kiwakilishi cha watu wenye tabia kama yake. Anaangamia kwa kichapo ama mshtuko anaoupata. Taswira ya uoni inaibua kivuli ambacho ni kihusika hivyo basi kutilia mkazo uwepo wa uhusika katika ushairi wa Kiswahili.

Katika shairi 'Mganga' ukurasa wa 10 Kezilahabi (1974) ametumia taswira ya uoni kuibua wahusika wanaobainika kitabia na hali waliyomo kutokana.

Mfano 1.

Akiwa na manyoya yake, viraka na kengele
Anaruka huko na huku
Anajiviringisha chini kuonyesha ujinga wake
Anafungua mdomo wake wa kishetani,
Na kuyatoa meno yake
Na akisaga meno yake ya kiimbwa
Anamwendea mgonjwa wake mwenye hofu,
Anamvuta nywele, anamtingisha kwa nguvu.
Na kumpiga teke tumboni mpaka
Anazimia; halafu anamkalia
Na kucheka Ha! ha! ha!
Akionyesha meno yake mabaya,
Hali akijitahidi kuonyesha ukweli fulani.
Kazi bure.

Anaidhihaki tu sanamu bora
Iliyochongwa na Mungu;
Na wakati wake, umepita.

Mshairi anasimulia kisa cha mganga kwa kutumia nafsi ya tatu kwa maneno yanayojenga picha ya hali au jambo fulani kwa msomaji. Mtunzi ametumia usimulizi wa moja kwa moja kueleza

sifa za huyu mganga. Kutokana na mambo anayoyafanya sifa ya mhusika anayoipata msomaji ni ya mtu mjinga. Katika mshororo wa tatu mtunzi anasema :

‘Anajiviringisha chini kuonyesha ujinga wake’.

Kupitia taswira ya uoni mtunzi anaibua mhusika mwenye umbile linalotisha. Katika ubeti wa kwanza anataja mdomo wake wa kishetani, meno yake mekundu, meno yake ya kiimbwa, meno yake mabaya hivyo kuibua mhusika anayetisha.

Taswira mbalimbali za usemi alizotumia mtunzi zimewezesha lugha kuibua uhusika katika *Kichomi.* Aidha ametumia hali mbalimbali za mazingira kutuchorea picha ya mahali. Katika shairi ‘Fungueni Mlango’ ukurasa wa 23 anadhihirisha utumizi wa picha ifuatavyo :

Mfano 1. Hewa kunikosa
Na jasho kunitoka ndani ya chumba
Kwa upweke
Ninajiona nimefungiwa.
Sioni madirisha lakini
Mlango wa karatasi uko mbele yangu
Ninaugonga kwa mikono
Kichwa na mabega
Mlango unatoa mlio kilio,
Lakini mwanadamu hatanifungulia.

Katika shairi hilimtunzi kupitia mseto wa taswira mbalimbali anaibua mhusika aliye hatarini hasa anapolia kwa sauti kubwa.Msimulizi ndiye mhusika mkuu kwa sababu anasimulia hadithi namna alivyofungiwa chumbani. Katika mshororo wa pili mhusika anatumia nafsi ya kwanza kujitambulisha anaposema;

‘Na jasho ‘kunitoka’ ndani ya chumba

Chumba alimofungiwa hakina madirisha ila mlango mmoja wa karatasi. Mazingira ya chumba hiki ni ya kutatanisha kwa sababu hakina hewa. Anatumia viungo vyake vya mwili: mikono, kichwa na mabega kuugonga mlango ambaounatoa mlio unapogongwa. Mlio huu ni wa kuwatanabahisha walio karibu ili waweze kuufungua. Ni kinaya kwamba mlango ni wa karatasi lakini hawezi kuufungua na hakuna anayeweza kumfungulia. Malalamishi ya msimulizi yanadhihirika kupitia kilio. Katika mshororo wa kumi msimulizi anatumia nafsi ya tatu kumtambulisha mhusika mwanadamu. Anasema hivi :

Lakini ‘mwanadamu’ hatanifungulia.

Katika shairi hili taswira ya uoni inaibua mhusika ambaye haoni madirisha, kupitia taswira ya mguso anaibua mhusika ambaye anatumia mikono na mabega kuugonga mlango, na kupitia taswira ya usikivu anaibua kihusika mlango ambacho kinatoa sauti ili kusikika lakini hakuna anayesikia na kumfungulia mlango. Hivyo basi mtunzi kupitia usimulizi anaibua uhusika kupitia mseto wa taswira katika shairi hili kudhihirisha uwepo wa uhusika katika ushairi wa Kiswahili.

Katika ubeti ufuatao mtunzi kupitia uzungumzi nafsi ametumia taswira ya uoni kuibua uhusika.

Mfano 1. Damu

Damu puani, damu mdomoni,
Damu kichwani itumikayo kama wino
Mikono, kichwa, mabega uchovu.
Kwa kichwa kama cha mbuni
Mchangani, tena ninaugonga
Lakini mwanadamu hatanifungulia.
Ninaona kizunguzungu
Ninapiga kelele kama
Ng’ombe machinjioni;
Fungueni mlango!
Mlango fungueni!
Lakini mwanadamu hatanifungulia.

Uhusika wa nafsi unaibuliwa mtunzi anapotumia nafsi ya kwanza kwa kurudia neno damu kusisitiza kutokwa kwa damu kwenye viungo vyake. Hajakata tamaa kwani kama mbuni

aliyeficha kichwa mchangani anaugonga mlango tena. Mtunzi ametumia taswira yahisi kuibua uhusika wa mtu anayeteseka. Mhusika anasimulia mateso anayopitia hivyo basi kuibua uhusika-nafsi. Aidha taswira ya uoni inaibua uhusika wa mtu anayepitia dhuluma kwa kuwa anaona damu ikimtoka kudhihirisha maumivu ya mwili anayohisi. Katika muktadha huunafsi neni ni mwanadamu na nafsi nenewa ni wanadamu kwa kuwa mtunzi kupitia usimulizi anawaamrisha waliomfungia ndani 'Fungueni mlango!' Mtunzi ametumia taswira ya usikivu kuibua uhusika kutokana na kelele anazopiga msimulizi ili mlango uweze kufunguliwa. Uhusika unaibuliwa katika shairi hili kupitia taswira ya uoni na taswira ya usikivu. Aidha mtunzi anaibua vihusika ambavyo ni chumba alimofungiwa ili ateseke kwa kuwa hakina hewa na mlango wa chumba hicho umefungwa ili kumzuia kutoka nje.

Mtunzi ametumia usimulizi kuweka wazi uovu utendwao na wanadamu dhidi ya wanadamu. Kupitia taswira anuai ameibua mhusika mtu kwa madhumuni ya kudhihirisha kuwa ni wanadamu ndio wenye uwezo wa kuzungumza. Msimulizi ametumia uzungumzi nafsi kipengele cha usimulizi kuweka wazi dhuluma anazotendewa na wanadamu wenzake. Binadamu ndio viumbe walio na akili inayoweza kupambanua unyama na utu. Ni kinaya kuwa wao ndio watendao unyama dhidi ya wanadamu na viumbe wengine hata kuwaangamiza.Hivyo basi mshairi anaibua uhusika wa binadamu kupitia usimulizi unaotokana na uzungumzi nafsi.

## 5.3 Lugha Inavyoibua Taswira ya Wahusika Katika Ushairi wa Kiswahili

Mbinu mbalimbali za lugha hutumiwa na watunzi kufanikisha kazi ya fasihi na ambazo huchangia uibuaji wa wahusika na vihusika katika mashairi ya Kiswahili. Fasihi ni sanaa itoayo maudhui yake kwa kutumia lugha ya maneno ambayo hutamkwa ama kuandikwa. Kipengele cha

lugha ni muhimu sana katika fasihi kwani ndicho hutenganisha fasihi na sanaa nyinginezo. Msokile (1993) anasema lugha ndio wenzo au malighafi ya fasihi, ni rasilmali ambayo huzalisha sanaa ya fasihi. Ni mtambo anaoutumia mtunzi kusafirisha maudhui yake kwa hadhira yake. Humsaidia katika usawiri wa wahusika wake, kudhihirisha dhamira yake na kutoa mguso mwafaka. Kwa hivyo kazi ya fasihi ni kama ujumbe unaotolewa na mtunzi kwa hadhira yake kupitia kwa lugha. Lugha ni kipengele muhimu sana katika kuijenga kazi ya fasihi yoyote ile kama vile ushairi. Hapawezi kuwepo fasihi bila lugha kwa sababu mwandishi wa fasihi hutumia lugha kujieleza. Huwapa wahusika maneno ambayo wao huyasema kwa niaba yake na mwandishi huwa na maana ambayo ameisuka katika lugha.

Wahusika hupewa lugha ambayo inawasaidia kueleza yale yanayokusudiwa na msanii. Lugha anayoitumia mhusika huambatishwa na picha zilizojengwa za mawazo ili kuweza kuleta athari kwa msomaji. Jinsi mhusika anavyozungumza na kuyaeleza kwa kikamilifu yale anayoyafikiria ndivyo anavyozidi kueleweka kitabia. Kadri lugha inavyokua ndivyo wahusika wanavyokuza lugha yao na ndivyo wanavyoweza kujieleza vyema zaidi. Mintaarafu mazungumzo ya wahusika msomaji anaweza kupata picha ya mahusiano yao kijamii na kiutamaduni hasa baada ya kuzisoma na kuzichunguza fikra zao.

Jamii ina matabaka mbalimbali ya watu. Kuna tabaka la wazee na lile la vijana, la waliosoma elimu ya shule na la waliokosa elimu hiyo ya shule. Lugha inavyotumiwa na matabaka haya hutofautiana. Tabaka moja linapowasiliana na tabaka jingine lugha itakayotumika ni tofauti na lugha itakayotumika kati ya watu waliomo kwenye tabaka moja. Lugha wanayotumia wanawake aghalabu huwa ni ya upole na iliyojaa tasfida. Wanaume lugha yao ni ya haraka na hutumia

maneno yenye makali bila kujali. Hivyo basi ni rahisi kubainisha uhusika kwa kuchunguza lugha inayotumiwa na aina mbalimbali ya watu katika jamii kwa kuzingatia maneno yanayotumiwa.

Vijana wanapojumuika pamoja ama wanapokuwa katika mazingira ambamo hakuna wazee hutumia lugha iliyojaa mizaha, kejeli na dhihaka. Wazee hutumia maneno yaliyojaa busara na hekima wawapo peke yao. Hivyo basi uhusika unaweza kudhihirika kupitia lugha inavyotumiwa na matabaka tofauti ya watu. Huwa rahisi kueleza sifa za mhusika kutegemea lugha iliyotumika. Ni vyema ieleweke kwamba kufaulu au kushindwa kwa mwandishi hudhihirishwa kwa dhima za kila mhusika. Kwa ujumla kazi yoyote ya fasihi hufaulu kutokana na muumano uliopo kati ya wahusika na vipengele vingine vinavyoijenga.

Wamitila (2003) ameeleza tamathali za usemi kuwa fungu la maneno au hata neno ambalo limegeuzwa maana yake ya kiurejelezi au asilia na kuwa na maana nyingine. Tamathali za usemi katika fasihi ni za aina mbalimbali, kuna misemoau nahau, takriri, tashbihi, sitiari,methali. Aidha lahaja za wahusika, uchaguzi wa msamiati, mishororo na mishata ni masuala ya lugha yanayoweza kutumika kuibua uhusika.

### 5.3.1 Utumizi wa Misemo na Nahau Kuibua Wahusika Katika Ushairi

Nahau ni misemo iliyojengwa kwa kwa kutumia maneno ya kawaida. Nahau huwa na undani wa kimaana kuliko baadhi ya misemo inayopatikana katika lugha fulani. Huwa na maana tofauti na ile iliyobebwa na maneno (Msokile 1993). Kwa hivyo misemo na nahau huonyesha maana fiche. Kimuundo nahau huwa na kitenzi na jina. Kezilahabi (1974) ametumia nahau katika shairi ‘Mzee na Mzigo’ katika ukurasa wa 38 kama vile, ‘kuona mengi’, ‘kula chumvi’ kuibua uhusika wa

nafsi. Utumizi wa semi hizi unaibua taswira ya mzee aliyechoshwa na tabia ya vijana wanaomlazimisha kutembea haraka. Nafsi-neni ni mzee. Katika ubeti wa nne anasema :

Mfano 1. Kula nimekula na sasa mwasema
Niko nyuma ya wakati.
Lakini kama mungepita mbele
Na uso wangu kuutazama (ubeti 4)
Ningewambia siri ya miaka yangu.

Aidha mtunzi ametumia semi 'kuona mengi', 'kula nimekula' kuibua uhusika wa mtu ambaye ameishi na kupitia hali tofauti katika uhai wake. Mshororo ufuatao unadhihirisha hali hii.

Mzigo wangu, mzigo mzito mno

Ni mtu aliyekomaa kiumri anaposimulia kuhusu mzigo alioubeba. Mhusika anajuta vijana wanaposema yuko nyuma ya wakati. Aidha sifa ya ushamba inajitokeza vijana wanapomuona kama mtu ambaye bado hajazinduka. Katika ubeti wa nne anasema:

Kula nimekula na sasa mwasema
Niko nyuma ya wakati.

Maana mbalimbali zinazojitokeza kutokana na nahau na misemo anayotumia msimulizi zinaibua uhusika. Anaposema 'kula nimekula' anamaanisha kuishi kwa muda mrefu hivyo basi ni mzee. Wanapoeleza kuwa 'yuko nyuma ya wakati' wanamaanisha hajazinduka hivyo basi ni mshamba. Anapotumia nahau 'pita mbele' anawaeleza watangulie ilhali anapozungumzia kuhusu 'kutazama uso' anamaanisha wamuangalie vizuri kabla ya kukata kauli. Kwa kutumia nahau 'siri ya miaka' anamaanisha wasifikiri umri wake ni mdogo kama wanavyodhani hivyo basi wanastahili kumpa heshima.

Katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* maumbile na hata tabia za wahusika wengine zimeweza kubainika. Nahau kama vile 'pande la mtu' lisilokuwa na mfano kama alivyoelezewa Liyongo.

‘Mwenye tamaa’ kama alivyoelezewa mwanawe Liyongo zimeibua uhusika kwa kutoa sifa za watu hawa. Tamaa ndiyo inayomfanya mwana huyu kumwangamiza babake. Saada ni mtu karimu na wa kutegemewa. Anapotumwa na Liyongo kupeleka ujumbe kwa mama ili amtengenezee mkate kisha atie ndani tupa anafanya hivyo. Mamaye Liyongo ana moyo wa huruma. Liyongo anapoaga dunia kama mama mzazi anasikitika sana. Sultani Mringwari ni katili asiyetaka upinzani wowote ama hali inayotishia utawala wake. Hali hii ndiyo inayomfanya kumhangaisha Liyongo. Ni kupitia tamathali mbalimbali za lugha ndipo uhusika katika ushairi wa Kiswahili umeweza kuibuka.

### 5.3.2 Utumizi wa Takriri Kuibua Wahusika Katika Ushairi

Takriri ni tamathali ya usemi ambayo huhusu kusisitiza au kushadidia ujumbe ili msomaji apate athari ya msisitizo huo kwa kurudia neno au kifungu cha maneno (Wamitila 2003). Mtunzi ametumia takriri katika mishororo mitatu ya mwanzo ya shairi ‘Mzee na Mzigo’ ukurasa wa 38.Maneno haraka na mzigo yametumiwa kusisitiza ustahimilivu wa mtu asiyekuwa na pupa. Japo mzigo ni mzito hataki kuuweka chini, yuko radhi kuwapisha waende wanakoenda. Hivyo basi kwa kutumia tamathali hii mtunzi anaibua uhusika wa mtu asiyetaka kuharakishwa. Anasema hivi:

Mfano 1. Mimi haraka, haraka sina.
Mzigo wangu, mzigo mzito mno
Na chini sitaki kuuweka.

Mtunzi ametumia tamathali za lugha kuibua wahusika wenye sifa za watu waliojaa dharau, maudhi na kiburi. Haya yanatokana na maneno wanayotumia yasiyokuwa na heshima. Katika mshororo wa tatu hadi wa tano mtunzi ametumia semi zinazoashiria waadhi.

Wana haraka lakini hawafiki mbele.

Wanataka kupita haraka ilhali hawajui alikotoka mhusika huyu au ni muda gani amekuwa safarini. Wanapomwona wanadhaninimtuwaumri kama wao. Ndiposa anasema katika mshororo wa tano:

Lakini kama mungepita mbele
Na uso wangu kuutazama (ubeti 4)
Ningewambia siri ya miaka yangu.
.

Msimulizi anajifahamu kwa sababu anajua anakotoka ilhali anaowarejelea hawajui watokako na wanakoenda. Wanapapia mambo bila kuuliza. Kupitia tamathali za lugha mtunzi ameibua uhusika wa mzee na uhusika wa vijana.

## 5.3.3 Utumizi wa Sitiari Kuibua Wahusika Katika Ushairi

Sitiari ni tamathali ya usemi ielezayo sifa za kitu fulani kwa kusema kuwa ni kingine.ni mbinu ya kiulanganishi kama tashbihi lakini ulinganishi huo haujitokezi waziwazi. Sitari huhusisha vitu viwili ambavyo ni tofauti kitabia na kimaumbile (Wamitila 2003). Katika shairi ‘Mganga’ ukurasa wa 10 wa nne mtunzi anaufananisha mdomo wa mganga na ule wa shetani, anasimulia kuhusu meno yake mekundu ambayo anayasaga kama mbwa.

Mfano 1. Anafungua mdomo wake wa kishetani,
Na kuyatoa meno yake mekundu.
Na akisaga meno yake ya kiimbwa

Mtunzi ametumia sitiari kuibua mhusika mwenye sifa na tabia za kutisha. Uhusika unaodhihirisha tabia na sifa ya unyama ya mganga kwa mgonjwa wake umo katika mshororo wa saba hadi kumi na moja. Mtunzi anasimulia namna anavyomwendea mgonjwa wake mwenye

hofu. Ukatili na ukosefu wa utu unaonekana anapomwendea mgonjwa na kumvuta nywele huku akimtingisha kwa nguvu. Anampiga teke tumboni mpaka anazimia kisha anamkalia na kucheka.

Kupitia sitiari uhusika unaoibuliwa ni wa binadamu mgonjwa asiyekuwa na hiari ila kustahimili madhila anayopitia. Siha yake si nzuri, hajiwezi na kuna uwezekano wa kiumbe huyukukata roho. Mtunzi kupitia usimulizi wa moja kwa moja kuanzia mshororo wa kumi na tatu hadi ule wa mwisho anasema :

Mfano 2. Anaidhihaki tu sanamu bora
Iliyochongwa na Mungu;
Na wakati wake, umepita.

Mtunzi ametumia stiari kumfananisha mgonjwa na sanamu. Ni sanamu kwa kuwa hawezi kufanya chochote ila kufanyishwa.

## 5.3.4 Mishororo na Mishata Inavyoibua Uhusika Katika Ushairi

Mshororo ni mstari wa utungo wa kishairi. Mistari hii ikiwa mingi ni mishororo. Mshata ni mshororo ambao unaendelea kimaana kwenye mstari unaofuatia. Mshata ni kipande cha mstari ambacho hakijakamiliki kimaana. Msomaji analazimika kuusoma mstari unaofuata ili aweze kuipata maana kamili. Mishororo na mishata ilivyotumiwa katika shairi ‘Mzee na Mzigo’ukurasa wa 38, inadhihirisha mhusika aliye na masuala mengi anayoyashughulikia akilini mwake. Hivyo basi taswira tunayoipata ni ya mhusika asiyetaka kusumbuliwa. Neno mzigo limerudiwa mara mbili kusisitiza dhiki aliyo nayo. Katika ubeti wa kwanza anasema :

Mfano 1. Piteni jamani, piteni
Nendeni, nendeni huko mwendako.
Mimi haraka, haraka sina. (ubeti 1)
Mzigo wangu, mzigo mzito mno
Na chini sitaki kuuweka.

Aidha miundo ya mishororo na mishata katika ubeti huu inaibua sifa ya mzee huyu. Ni mzee mvumilivu, mwenye busara, stahamala na hekima na asiyependa vurumai. Anaposema 'Mzigo wangu, mzigo mzito mno' anamaanisha kuwa japo anapitia shida ataendelea kung'ang'ana na hali hiyo hadi mwisho. Uhusika unaibuliwa kutokana na utumizi wa lugha.

Miundo ya mishororo anayoitumia mtunzi inabainisha wahusika wasiokuwa na subira. Hawana haja kujua alikotoka wala uzito wa mzigo alioubeba. Hawajali hali ya mhusika huyu hivyo basi kuibua sifa za wasimulizi wenye kiburi na wasiojali maslahi ya wenzao. Anasema:

Mfano 2. Kula nimekula na sasa mwasema
Niko nyuma ya wakati.
Lakini kama mungepita mbele
Na uso wangu kuutazama (ubeti 4)
Ningewambia siri ya miaka yangu.

Mtunzi anatumia nafsi ya kwanza anapojirejelea katika mshororo wa tatu kuwa hana haraka na mzigo alioubeba ni mzito mno na hataki kuuweka chini.

Tamathali za lugha kama vile tashbihi, takriri, misemo na nahau zinaweza kuibua wahusika na vihusika au nafasi yao kama wahusika na vihusika. Kupitia tamathali hizi taswira anayoipata msomaji ndiyo itamfanya kutambua sifa za mhusika iwapo ni mtu mwema, mzuri au mstaarabu. Matendo ya mtu yanatokana na lugha na jinsi yanavyosimuliwa na mshairi. Masimulizi yanaweza kutolewa kiasi kwamba tunapata picha ya mtu huyo au hali ya mahali fulani barabara. Msomaji anaweza kutoa maelezo kuhusu mtu kutokana na masimulizi na kueleza ni wa aina gani. Hivyo basi ni bayana utumizi wa tamathali mbalimbali za lugha umewezesha utafiti kutathmini namna uhusika unavyojitokeza, kupambanua aina za uhusika na kuchunguza namna

taswira huumba wahusika katika ushairi wa Kiswahili. Utafiti umedhihirisha uwepo wa uhusika katika ushairi wa Kiswahili.

Mashairi yote tuliyoyachunguza yametumia kipengele hiki cha lugha kuibua uhusika katika njia mbalimbali kama ifuatavyo. Kwanza uchunguzi wa diwani mbili umedhihirisha utumizi wa lugha ya kishairi. Kama isingekuwa hivyo hayangeitwa mashairi. Lugha ya kishairi huwa ya mkato iwe ni mashairi ya arudhi au mashairi huru. Kazi zilizochunguzwa zimetumia lugha ya mkato na kwa kufanya hivyo kuibua uhusika ambao tumejadili katika mashairi tuliyochanganua.

Pili, lugha ya wahusika pia imeibua uhusika kwa namna mbalimbali. Kutokana na mazungumzo ama usemi wa wahusika wakati wanapojibizana. Uhusika ulibainika katika ngonjera zilizomo katika diwani ya *Malenga wa Vumba* na diwani ya *kichomi* na kupitia usimulizi wa wahusika mbalimbali katika *Utenzi wa Fumo Liyongo.* Kupitia tamathali mbalimbali za usemi mtunzi ameibua uhusika

## 5.4 Hitimisho

Sura hii imechambua uhusika unavyojitokeza katika ushairi kwa kurejelea diwani mbili na utenzi mmoja. Uhusika umechambuliwa kwa kuzingatia usimulizi, uhusika nafsi na matumizi ya picha. Dhana ya uhusika katika ushairi imeangazwa ili kuupa uchambuzi uzito unaostahili. Usimulizi kama njia ya kuibua usemezano imepambanuliwa. Maana ya usimulizi imefafanuliwa hususan kuleta uelewa wa kipengele cha uhusika. Uumbaji wa wahusika kupitia lugha umejadiliwa. Lugha ni msingi, nguzo na mhimili wa kazi ya fasihi. Lugha ndiyo humchora, kumuumba na kumuumbua mhusika. Kwa kuwa ushairi ni sanaa inayotumiwa katika kusema mambo mengi

kwa kutumia maneno machache ni dhihirisho tosha kutueleza kuwa ushairi una lugha yake maalum. Utafiti huu umeonyesha jinsi uhusika unavyojitokeza katika ushairi wa Kiswahili kwa kutumia lugha.

Utafiti huu kwa jumla ni wa kiuchanganuzi, ni kwa kupitia maelezo, utafiti huu umeweza kujibu maswali yaliyolenga kutambua: Namna uhusika hujitokeza, aina za uhusika na taswira ya wahusika katika mashairi. Maelezo yameonyesha kufaulu kwa utafiti huu kwa kuonyesha matumizi ya dhana ya uhusika katika uumbaji wa wahusika. Ufafanuzi huu unadhihirisha namna ambavyo maswali ya utafiti yalijibiwa, suala kufumbuliwa na madhumuni kuthibitishwa.

# SURA YA SITA

# MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 6.1 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa tasnifu, matokeo, mahitimisho na mapendekezo ya utafiti huu. Inatoa muhtasari kwa kurejelea suala la utafiti, maswali ya utafiti, nadharia na madhumuni ya utafiti. Sura hii imeeleza kwa muhtasari matokeo ya utafiti yaliyotokana na data zilizochanganuliwa. Data hizi zimechanganuliwa kwa minajili ya kuonyesha njia zilizotumiwa na watunzi wa diwani mbili na utenzi mmoja kuumba wahusika katika ushairi. Aidha sehemu hii inatoa mapendekezo ambayo yanaweza kutumiwa na watafiti wengine kushughulikia uhakiki na uchanganuzi wa wahusika katika tanzu zingine za fasihi.

## 6.2 Muhtasari wa Tasnifu

Azma ya utafiti huu ilikuwa kuchunguza uhusika katika ushairi wa Kiswahili. Mashairi ishirini na matatu kutoka diwani mbili *Kichomi* (1974) na *Malenga wa Vumba* (1981) na *Utenzi wa Fumo Liyongo* (1973) yamechunguzwa. Malengo ya utafiti yalikuwa:kutathmini namna uhusika unavyojitokeza katika ushairi wa Kiswahili, kupambanua aina za uhusika katika ushairi wa Kiswahili na kuchunguza namna taswira huumba wahusika katika ushairi wa Kiswahili. Utafiti umeweza kubainisha uhusika na namna watunzi wanavyowaumba wahusika katika tungo zao kama njia ya kujibu maswali ya utafiti huu. Ili kutimiza madhumuni ya utafiti  nadharia ya usimulizi ilitumiwa kama dira.

Tasnifu hii imegawika katika sura sita: Sura ya kwanza ndio msingi wa utafiti. Sura hii imeshughulikia masuala muhimu yanayohusiana na utafiti huu. Haya ni pamoja na usuli, yaliyoandikwa kuhusu mada, suala la utafiti, maswali na malengo ya utafiti na sababu za kuchagua mada. Aidha, mbinu, muundo na mahali pa utafiti ni mambo yaliyojadiliwa katika sura hii. Pia njia za kukusanya, kuchanganua na kuwasilisha data zimeelezwa. Mbinu za kukusanya data zilizotumiwa katika utafiti huu ni kusoma kwa kina na kuchanganua mbinu za kuibua uhusika zilizotumika katika mashairi teule. Data ilikusanywa kutoka kwa mashairi teule na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo. Vilevile, sura ya kwanza imejadili nadharia iliyoongoza utafiti huu ambayo ni nadharia ya usimulizi. Maelezo yametolewa kuhusu mwasisi wa nadharia hii na kuonyesha mihimili muhimu iliyoongoza utafiti wenyewe.

Utafiti umeonyesha kuwa uhusika unavyoibuliwa katika utanzu wa ushairi ni tofauti na unavyoibuliwa katika tanzu zingine. Hali hii inatokana na umbo la shairi. Mashairi hutumia lugha ya mkato na maelezo yasiyokuwa marefu. Ni jukumu la msomaji wa shairi kuunganisha maelezo mbalimbali katika shairi ili kuibua aina ya mhusika ama kupata taswira ya mhusika kutokana na maelezo. Kwa kutathmini namna uhusika unavyojitokeza, kupambanua aina za uhusika na kuchunguza namna taswira huumba wahusika katika ushairi wa Kiswahili utafiti umebainisha kwamba uhusika hujitokeza katika ushairi wa Kiswahili kupitia usimulizi na tamathali za usemi.

## 6.3 Matokeo ya Utafiti

Utafiti ulizingatia kipengele cha uhusika na utokeaji wake katika ushairi wa Kiswahili. Ili kufikia lengo hili utafiti  ulijikita katika madhumuni matatu. Kwanza, utafiti ulitathmini namna uhusika

unavyojitokeza katika ushairi wa Kiswahili.Hivyo basi, utafiti kwa kutumia nadharia ya usimulizi kama dira umefasiri usimulizi kuwa ni nafasi anayoichukua msimulizi katika hadithi yenyewe. Usimulizi ni njia kuu ya mtunzi ya kudhibiti na kujenga maudhui yake. Usimuliaji huelekeza ujenzi wawahusika, matukio na kila kinachowasilishwa katika shairi.

Kwa msomaji usimulizi hudhibiti hisia zake juu ya yote yanayosemwa. Usimulizi hutufanya tuone, tusikie, tunuse na hata kuonja hadithi iliyo katika maandishi tu. Hutufanya tupate hamu au matamanio, woga na kuchukua msimamo kutokana na yale tuliyoyasoma. Hadithi yoyote ile husimuliwa na msimulizi ambaye anaweza kushiriki katika matukio anayoyasimulia yeye mwenyewe, kupitia kwa wahusika wake au kutoshiriki kabisa. Utafiti kwa kutoa mifano kadha umegundua kuwa uhusika hudhihirika kupitia matendo ya wahusika, tabia zao na hali kama anavyosimulia mtunzi.

Dhumuni la pili lilikuwa kubainisha aina za uhusika katika ushairi. Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kuibuliwa kwa uhusika kupitia matapo matanoya nafsi. Kwanza ni lile tapo la uhusika wa nafsi-pekee. Katika tapo hili mtunzi mwenyewe huwa anaongea na nafsi yake.

Tapo la pili la uhusika huu ni la nafsi-umoja.  Katika tapo hili ayasemayo mtunzi huwa yanamwelekea mtu mmoja. Usimulizi huelekezewa mtu mmoja wakati mtunzi anapompa mawaidha au maonyo au kueleza sifa za nafsi inayorejelewa.

Uhusika wa nafsi-uwili ni tapo la tatu. Katika tapo hili nafsi neni ni mtunzi mwenyewe anapojibizana na nafsi nenewa, hivyo basi kuibua nafsi mbili zinazojibizana. Panaweza kuwa na

usimulizi wa nafsi zaidi yamoja kumaanisha upande mmoja ulio na wasimulizi zaidi ya mmoja hivyo kuwa nafsi mbili zinazojibizana.

Tapo la nne ni nafsi-wingi. Nafsi neni katika tapo hili huzungumza kwa niaba ya kundi fulani ambapo yeye ni mmoja wao. Usimulizi katika uhusika huu huwa katika wingi. Viambishi vinavyorejelea wingi wa nafsi kama vile ‘sisi’,‘nyinyi’, ‘wao’ na ‘tu’ hutumika.

Tapo la tano ni tapo la uhusika wa nafsi-kikundi. Msimulizi katika tapo hili huwa ni kikundi. Mshairi huwa anazungumza na kikundi cha watu. Uhusika unaoibuliwa katika tapo hili hubainika kutokana na viambishi vya ngeli husika. Hivyo basi viambishi vinavyorejelea wingi katika ngeli za nafsi hutumika. Utumizi wa viambishi kama vile ‘tu’ katika neno **tu**liyozaa ndio hubainisha wingi

Kupitia matapo haya uhusika katika ushairi umeweza kuibuliwa. Uhusika katika ushairi unaweza kuwahusisha wahusika wengi ama mhusika mmoja ambaye ni msimulizi. Mbali na wahusika walioumbwa mshairi mwenyewe huweza kuwa mhusika katika shairi. Nadharia ya usimulizi iliwezesha data kuchanganuliwa vilivyo. Mihimili mikuu ya nadharia hii ni dhana ya usimulizi na dhana ya uhusika. Kulingana na dhana ya uhusika wahusika wanatazamwa katika misingi ya matendo na mazungumzo ya watu. Mwenendo wa mtu fulani utaweza kuelezwa kutegemea hisia, matamanio na maadili kama unavyobainika katika kuzungumza na matendo yake. Neno mhusika limetumika kumaanisha tofauti iliyoko katika mazungumzo ya watu, tabia, matendo na maingiliano yao na watu wengine. Ufafanuzi huu unamweleza mhusika kuwa kile

kinachomfanya mtu mmoja kuwa tofauti na mwingine. Ni kutokana na mihimili miwili ya dhana ya usimulizi utafiti uliweza kuibua uhusika.

Dhumuni la tatu la utafiti huu lilikuwa kuchunguza taswira ya wahusika katika ushairi wa Kiswahili. Kupitia taswira kama vile uoni, usikivu, hisi, mwonjo sifa mbalimbali kama vile wivu, usaliti, ukatili na utovu wa nidhamu wa wahusika zimeweza kuibuliwa. Mtunzi huweza kusawiri na kudhihirisha sifa na tabia za wahusika mbalimbali. Migogoro miongoni mwa wahusika kama vile tabia za wivu, tamaa, wizi, mauaji, usaliti, mapenzi na upelelezi imeweza kubainika. Sifa za wahusika fulani zimejitokeza kuwaathiri wahusika wengine. Uhusika katika ushairi ulikuwa ndiyo hoja ya kimsingi na kwamba hudokezwa tu, wala haufafanuliwi na watunzi wa mashairi. Utafiti uliweza kudadavua dokezi hizi kwa kuelekezwa na nadharia ya usimulizi. Mbinu za uhusika zimefaulisha kuibuliwa kwa uhusika. Ujumbe uliotumika kusawiri mhusika uliwasilishwa na mmoja wa viumbe katika baadhi ya mashairi. Katika mashairi mengine ujumbe ulishirikishwa na nafsi ya mwandishi aliyedokezwa ndipo tabia na sifa za wahusika zikaweza kubainika na hivyo kutilia pondo uwepo wa uhusika katika ushairi wa Kiswahili.

## 6.3 Mahitimisho

Kutokana na utafiti huu madhumuni yamefanikishwa kwa njia kadha. Utata na uvulivuli unaozingira suala la uhusika katika ushairi wa Kiswahili umeweza kutatuliwa, hivyo basi kufumbua swala la utafiti. Utafiti ulikuwa na madhumuni matatu mahsusi.

Kwanza, utafiti ulitaka kutathmini namna uhusika unavyojitokeza katika ushairi wa Kiswahili. Matokeo kutokana na tathmini hii ni kwamba utafiti umedhihirisha kuwa sauti inayosikika katika mashairi ni sauti ya mazungumzo ya mshairi ama wahusika katika shairi. Nafsi-neni ni msanii mwenyewe au mhusika akiwakilisha watu ama tabaka fulani katika jamii. Kutokana na sauti hii utafiti huu umeibua uhusika simulizi. Uhusika huu unadhihirika kwa kuwa ushairi ni hadithi. Hadithi ni mfululizo wa matukio yanayohusu wahusika. Uhusika hujumuisha wahusika na vihusika. Wahusika na vihusika huwezesha ujumbe kupitishwa hivyo basi kupitia usimulizi uhusika umeweza kujitokeza.

Pili, utafiti ulidhamiria kupambanua aina za uhusika katika ushairi teule wa Kiswahili. Matokeo ya utafiti yamebainisha aina za uhusika kupitia usimulizi. Uhusika uliweza kubainika kupitia masimulizi ya moja kwa moja ya mtunzi, masimulizi ya mhusika katika shairi, masimulizi ya wahusika wengine kuhusu mhusika katika shairi na uzungumzi nafsi. Hivyo basi utafiti huu uliweza kubainisha aina za uhusika zipatazo sita ambazo ni : uhusika nafsi, uhusika umbo, uhusika dhahiri, uhusika usio dhahiri na uhusika husishi.

Tatu utafiti ulitaka kuchunguza namna taswira huumba wahusika katika ushairi wa Kiswahili. Utafiti ulifichua kuwa uhusika unaweza kubainika kupitia taswira mbalimbali. Taswira ya wahusika katika ushairi wa Kiswahili inaweza kubainika kupitia taswira ya usikivu ambapo msanii huunda picha ambazo hulenga hisia ya kusikia kwa kujenga picha zinazohusiana na sauti, taswira ya mguso ambayo hujenga picha ya kitu thabiti au kitu kinachoweza kugusika, taswira ya mwonjo ambayo hulenga hisia ya kuonja kutokana na maelezo yanayohusiana na chakula, na

taswira ya uoni ambayo humchochea msomaji kuona picha fulani. Kutokana na taswira hizi utafiti uliweza kuibua uhusika.

Uchanganuzi wa mashairi ukiongozwa na Nadharia ya Usimulizi umeonyesha kuwa ni kupitia mihimili ya nadharia hii ndipo uhusika hudhihirika. Dhana ya uhusika na dhana ya usimulizi huwezesha kuwasilisha matendo na tabia za wahusika. Mihimili hii miwili imewezesha kubainisha aina za uhusika na taswira ya wahusika katika mashairi. Suala la usimulizi ni la kimsingi sana katika uwasilishaji wa kazi mbalimbali za fasihi. Hatukosi kuisikia sauti ya msimulizi angalau katika akili zetu iwapo si katika masikio yetu pale tunapoifuatilia katika shairi. Kule kuwepo msimulizi ni ithibati kuwa uhusika upo. Katika shairi mtunzi anaweza kuwa mhusika anaposimulia matukio. Kupitia unenaji wake, sifa na matendo yake au ya wahusika na vihusika hubainika. Wakati mwingine mtunzi anaweza kujiwasilisha kama mhusika kupitia usimulizi au wahusika kutegemea nafsi ambamo wahusika wamewasilishwa. Mtunzi anapojiwasilisha hivi matapo matano ya uhusika wa nafsi huibuka. Sifa na hulka ya wahusika na vihusika hubainika, hivyo basi swala la utafiti kufumbuka.

## 6.4 Mapendekezo

Utafiti uliweza kubaini kuwa uhusika katika ushairi ni kipengele muhimu. Hivyo basi uhusishwe katika uchambuzi wa mashairi. Uhusika usipuziliwe mbali kwa sababu ni kupitia uhusika ndipo ujumbe uliodhamiriwa hupitishwa. Sifa, tabia, mwenendo wa mtu, mwingiliano wa watu na vihusika katika jamii ndio hujenga jamii. Ni kupitia tabia, matendo na mafunzo mbalimbali yanayotokana na wahusika katika shairi na fasihi kwa jumla ndipo vizazi vinavyofuata huweza kujifunza kurekebisha tabia zao.

Utafiti unapendekeza utafiti linganishi wa uhusika katika utafiti wa baadaye. Ni kutokana na ulinganishi huu ndipo dhana ya uhusika inaweza kueleweka zaidi. Kwa jinsi hii, mchango mkubwa utakuwa umetolewa katika fasihi. Utafiti unapendekeza *Utenzi wa Fumo Liyongo* ufanyiwe uchunguzi wa jinsi fani ya uhusika imefanikishwa na mtunzi. Madhumuni ya utafiti huu yameafikiwa na hivyo wachambuzi wanapaswa kushughulikia suala la uhusika wanapochambua mashairi.

Mapendekezo yafuatayo yametolewa na utafiti huu.

- Utafiti huu unapendekeza uchunguzi wa uhusika na usawiri wa wahusika katika diwani zingine za Kiswahili ambazo hazijafanyiwa utafiti.
- Utafiti huu unapendekeza utafiti wa uhusika kupitia vipengele vingine katika mashairi ya Kiswahili ambayo hayajafanyiwa utafiti.

## MAREJEO


Abdalla, A. (1973). *Sauti ya Dhiki*, Nairobi. Oxford University Press.

Abdulaziz, M. H. (1979). *Muyaka: 19th Century Swahili Popular Poetry*. Nairobi: K.L.B.

Abeid, S.K.A (1954). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: E.A.L.B.

Abrams, M.H (1981). *A Glossary of Literary Terms* (4th ed.). USA: Holt Rinhart and Winston,

Akilimali, K. H.A (1980). *Diwani ya Akilimali*. Nairobi:K.L.B

Allen J. W. T. (1971). Trans. *Tendi; Six examples of a Swahili classical verse form.* London: Heineman.

Aristotle (350 B.C.E). *Poetics.*(S. H. Butcher, Trans.). Oxford:Clarendon Press.

Atkins. G. D. (1989). *Contemporary Literary Theory*, U.S.A. Macmillan.

Attenbernd, L na Lewis, L. L (1963). *Introduction to LiteratureStories,* New York. Macmillan Company.

Barthes, R. (1984). *The Pleasure of The Text*.Translated by Richard Miller.France. Farrar, Straws and Giroux. Editions du Seuil.

Berger, P. (1997). *Redeeming Laughter. The Comic Dimension of Human Experience*, Walter de Gruyter, ISBN

Bhalo, A. (1974). *Malenga wa Mvita.* Nairobi: Oxford University Press.

Boukheit, A. (1981). *Malenga wa Vumba*. Nairobi: Oxford University Press.

Butler, S. (1969). *The Oddyssey* of Homer. Red and Black Publishers.(Original work published 800 KK).

Carpenter, J na Neumeyer. P (1974). *Elements of Fiction: Introduction to The Short Stories*. Dubuque, Iowa.W.M.C Brown Company Publishers.

Caudwell, C. (1947). *Illusion and Reality*: A Study of The Sources of Poetry,New York: International Publishers Co.

Chacha, N.C. (1977). 'Ushairi wa Abdilatif Abdalla'. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Nairobi. Haijachapishwa.

Chiari, J. (1960). *Realism and Imagination*,London: Barrie and Rockliff Ltd.

Chiraghdin Shihabudin (Mh.) (1980). *Malenga wa Mrima: Tungo za Mwinyihatibu Mohamed*. . Nairobi:Oxford University Press

Chiraghdin S, Sheikh, A. N, na Abdalla, B. (1977). "Tarehe ya Ushairi wa Kiswahili". *Mulika* 7:59-67.

Cook, D. (1977).*Literature. A Critical View*. London: Longman.

Emenyonu, E. N. (1987). *Critical Theory and African Literature*. Nigeria: Heineman Educational Books Ltd.

Enon, J. C. (1998). *Education Research, Statistics and Measurement:* Tanzania. Educational Psychology.

Forster, E. M. (1972). *Aspects of the Novel,* London: Penguin Books.

Genette, G (1988). *Narrative Discourse. An Essay in Method*. Itacha: Cornel University Press.

Gibbe, A. G. "Fasihi na Jamii: Baadhi ya Washairi wa Kiswahili". *Kiswahili* 48/1 (1978): 1-25.

Graziell, A. (2004:69). "Jazanda ya Njozi Katika Baadhi ya Mashairi ya Euphrase Kezilahabi". *Swahili Forum II* edited by Rose Marie Beck, Lutz Diegue. Thomas Geider, Utah Reuster Jahn. Department of Anthropology and African Studies. Mainz, Germany.Johannes Gutenberg University.

Hameren, G. (1975*). Advance In Art and Literature,* New Jersey: Princetone University Press.

Indede, F. (2011). 'Mwanamke Angali Tata Katika Ushairi wa Kisasa'. Swahili Forum 18.

Jackson, N. M na Richard M. I. (2017).**"**Uhakiki wa Utendi wa Fumo Liyongo Kwa KutumiaVigezo Vya Aristotle Vya Kitanzia" Idara Ya Lugha na Isimu, Chuo Kikuu Cha Laikipia, Kenya

Jahn, M. (2005).Narratology: *A Guide to The Theory of Narrative*. Cologne: English Department, University of Cologne.

Jones, E. (1987). *African Literature Today (Vol.14*), Heineman Educational Books, New York. Kahigi, K. K, Ushairi: Mtazamo wa Kisayansi. *Kiswahili* 45/4 (1976). TUKI. Chuo Kikuu Cha Dar- es- Salaam.

Kahigi, Kulikoyela. 'Swahili Poetry. London: *Kiswahili*. 45/1 (1975). 35-50.

Kezilahabi, E. "The Development of Swahili Poetry" 18-20$^{th}$ Century. *Kiswahili.* 42.2 (1973). 62-67.

Kezilahabi, E. (1974). *Kichomi*, London: Heinemann.

Kijumwa, M. (1973). 1st ed.1911). *Utenzi wa Fumo Liyongo*.Dar-es-Salaam: Institute for Kiswahili Research.

Kitsao, J. (1975). "Astylo-stylistic Approach Adopted For The Study of Written Swahili Prose Texts". M. A. Thesis. University of Nairobi.

Knappert, J. (1967). *Traditional Swahili Poetry*. Leiden.

Kothari, C. (1992). *Research Methods: Methods and Techniques*, New Delhi: New Wiley Eastern Publishers.

Kyallo, A. (1992). "Style: The Vision of the Writer". Unpublished M.A Thesis, Kenyatta University.

Larkin, M. (1977). *Man and Society in Nineteenth Century Realism*, London. Mcmillan Press Ltd.

Leberman, M. M. & Forster,E.E. (1968).*Narratology: Introduction to The Theory of Narratology.* Atlanta: Foresman Lothe & Co.

Lugano, S. R. (1989)."Mwanamke katika Riwaya za Kezilahabi"Tasnifu ya Uzamili. Haijachapishwa. Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Lukacs, G. (1972).*Studies in European Realism,* London: The Marlin Press.

Manfred, J. (2005). Narratology A Guide to The Theory of Narrative. Part III of *Poems, Plays, and Prose: A Guide to the Theory of Literary Genres*. English Department. University of Chicago.

Massamba, D.P.B. (1983) "Utunzi wa Ushairi wa Kiswahili." *Fasihi*. [*Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III*],Mhar. Taasisi ya Uchunguziwa Kiswahili Chuo Kikuu Cha Dares Salaam: uk 55-94.

Mayoka, J. (1986). *Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka*. Dar-es- Salaam: Tanzania Publishing House.

Miruka, O. (1994). *Encounters With Oral Literature*. Nairobi. East African Publishers.

Mlacha S.A.K. (2003). "Wahusika Katika Riwaya za Kiswahili Tanzania". *Mulika*. Dar-es-Salaam: TUKI.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*.Nairobi: East African Educational Publishers.

Mohamed, K. A. na J.S. Madumula. Uchambuzi wa Mashairi na M. M. Mulokozi. *Mulika* 6 (1989): 30-40.

Mohammed, K. K (1981). *Mashairi Yetu.*Mhar. M. K. Khan. Nairobi: Afro Press Ltd.

Mohamed, S. A. (1984). Makala `Kupatana na Riwaya Zangu katika *MWAMKO* Toleo la Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mohamed, S.A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili*, Nairobi. East African Educational Publishers,

Momanyi, C. (1991). "Matumizi ya Taswira Kama Kielelezo cha Uhalisi katika *Utenzi wa Al Inkishafi".* Tasnifu ya M.A.Haijachapishwa. Chuo Kikuu Cha Kenyatta.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi.*Nairobi:East African Educational Publishers.

Mugambi, P. J. (1982). "Uhakiki wa Maudhui katika Tamthilia za Kiswahili za Kikenya zilizochapishwa". Tasnifu ya Uzamili.Haijachapishwa. Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Mugenda, O. M & Mugenda A.G. (1999). *Research Method : Quantitative and Qualitative Approaches.* Nairobi:Centre for Technology.

Muindi, A. (1990). "Usawiri wa Wahusika Wanawake Katika Riwaya za Said A. Mohammed". Tasnifu ya Uzamili.Haijachapishwa. Chuo Kikuu Cha Kenyatta.

Mule, K. (199). Swala la Mwanamke Katika Tamthilia ya Kiswahili: Waandishi wa kike katika njia panda. Tasnifu ya Uzamili.Haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Muleka, J. (2000). "Portrayal of Girl Characters in Selected Children's Books in Kenya". Unpublished M.A Thesis, KenyattaUniversity.

Mulokozi, M. M. (1975). "Revolution and Reaction in Swahili Poetry*", Kiswahili*.45/2 pp 46-65.(1989), "Tanzu za Fasihi Simulizi" *Mulika* 21, 1-24

Mulokozi, M. na K. K. Kahigi. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar-es-Salaam: Tanzania Publishing House.

Murungi, G. K. (2013)."Mtindo Unavyoendeleza Maudhui Katika *Natala"* Tasnifu ya Uzamili. Haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mutiso, K (1982). "Uhakiki wa *Malenga wa Mvita*". Tasnifu ya Uzamili. Haijachapishwa. Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Mwai, W. (1988). "New Trends in Ushairi". Unpublished M.A. Thesis. University of Nairobi.

Mwenda, N. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi.* Augustana College, Rock Island.

Ndumbaro, E (2013). *Uhakiki wa Fumo Liyongo kama Utendi wa Afrika* . Imepakuliwa kutoka chomboz.blogspot. com/p/fasihi-4html.

Ndumbaro, E(2013). *Fasihi Simulizi ya Kiafrika.* Imepakuliwa kutoka chomboz. blogspot. com/p/fasihi-4html.

Njogu, K (2004). *Reading poetry as Dialogue.* Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K na R. Chimera (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi, Kiswahili Tertiary Publishing Project.

Obura, K. (1991). *Changing Images-Portrayal of Girls and Women in Kenyan Texts*. Nairobi: Acts Press.

Pfister, M. (1977). *The Theory and Analysis of Drama*. Trans. John Halliday. Cambridge: Cambridge UP.

Reeves, J. (1965). *Understanding Poetry*.London: Heineman.

Richards, I. A. (1970). *Principles of Literary Criticism*. Routledge and Keegan Ltd. London:

Richardson, L. (1994). 'Writing: a method of inquiry' in Denzin, N. and Lincoln, Y. *Handbook of Qualitative Research,* London and New York, Sage.

Robert, S. (1962). "Hotuba juu ya Ushairi," Harries Lyndon, *Swahili Poetry*, London:Oxford, uk 272-84.

Senkoro, F.E.M.K. (1988). *Ushairi: Nadharia na Tahakiki*. Dar-es-Salaam: Dar-es-Salaam University Press.

Shariff, N. I. (1988). *Tungo Zetu.* New JerseyTrenton. The Red Sea Press. Inc.

Simala, I. (1991). *Utenzi wa Wadachi Kutamalaki Mrima*. Tasnifu ya Uzamili. Haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Moi.

Stern, J. P. (1973). *On Realism,* London: Routledge and Kegan Paul.

Stromberg, R. N. (1968). *Realism, Naturalism and Symbolism*: Modes of Thought and Expression in Europe 1848-1914, New York: Walker and Company.

Styan, J. L. (1960). *Elements of Drama.* Cambridge. Cambridge University Press

Taine, P. (1968). *Five Approaches of Literary Criticism: 123,* New York: Cooler Books.

Topan, F. M. (Mhar). (1977). *Mashairi ya Kiswahili: Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili. Kitabu cha 2*. Nairobi:Oxford University Press.

Wamitila, K. (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publications Ltd

.

Wamitila, K. (2008). *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*.Nairobi. Sitima Printers & Stationers Ltd

http://haldjas. folklore.ee/folklore

http://www.en Wikipedia.org/wiki/category:filmgenres

https://study.com/.../methods-of-characterization-in-literature.html

www.literacydevices.com/characterization.

**KIAMBATISHO**

**ORODHA YA UCHUNZAJI**

| MBINU ZILIZOIBUA UHUSIKA | *KICHOMI* | DIWANI YA *MALENGA WA VUMBA* | *UTENZI WA FUMO LIYONGO* |
|---|---|---|---|
| Usimulizi | ✓ | √ | ✓ |
| Uhusika nafsi | ✓ | ✓ | ✓ |
| Uzungumzi nafsi | ✓ | ✓ | |
| Taswira ya<br>- usikivu | ✓ | ✓ | |
| Taswira ya<br>- mguso | ✓ | ✓ | ✓ |
| Taswira ya<br>- mwonjo | ✓ | ✓ | |
| Taswira ya<br>- uoni | ✓ | ✓ | ✓ |
| Tamathali za Lugha | | | |
| -misemo | ✓ | | |
| - nahau | ✓ | | |
| - takriri | ✓ | ✓ | ✓ |
| - methali | ✓ | ✓ | ✓ |
| -uchaguzi wa msamiati | ✓ | | |
| -miundo ya mishororo | ✓ | | |